**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA KUMI NA SABA**

**Kikao cha Nne – Tarehe 1 Novemba, 2024**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa tuketi.

Katibu.

**NDG. BARAKA I. LEONARD – KATIBU WA BUNGE:**

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI:**

Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa unaokusudiwa kutekelezwa na Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA:**

Mapendekezo ya Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

**MHE. ZAYTUNI S. SWAI K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI:**

Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti kuhusu Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 pamoja na Mapendekezo ya Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

**SPIKA:** Ahsante sana.

Katibu.

**NDG. BARAKA I. LEONARD – KATIBU WA BUNGE:**

## MASWALI NA MAJIBU

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, maswali; tutaanza na Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta, Mbunge wa Urambo sasa aulize swali lake.

Na. 48

### Hitaji la Ofisi ya Mkuu wa Wilaya na Ofisi za Halmashauri – Urambo

**MHE. MARGARET S. SITTA** aliuliza:-

Je, lini Ofisi ya Mkuu wa Wilaya pamoja na Ofisi za Halmashauri ya Wilaya ya Urambo zitajengwa?

**SPIKA:** Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Dkt. Dugange, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imeanza maandalizi ya kujenga Ofisi ya Mkuu wa Wilaya pamoja na Ofisi za Halmashauri ya Wilaya ya Urambo ambapo eneo lenye ukubwa wa mita za mraba 25,000 limetengwa kwa ajili ya ujenzi wa jengo la halmashauri na eneo la mita za mraba 25,000 kwa ajili ya ujenzi wa Ofisi ya Mkuu wa Wilaya.

Mheshimiwa Spika, aidha, halmashauri imeshaandaa na kuwasilisha andiko la jengo la ofisi za halmashauri lenye thamani ya shilingi bilioni 5.75 Ofisi ya Rais, TAMISEMI kwa hatua zaidi.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2025/2026 Serikali itatenga shilingi milioni 200 kwa ajili ya kuanza ujenzi wa Ofisi ya Mkuu wa Wilaya. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Margaret Sitta, swali la nyongeza.

**MHE. MARGARET S. SITTA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi kuuliza maswali; nina maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kwanza, ninamshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu aliyotoa. Swali la kwanza; kutokana na ile hali ya Ofisi ya Mkuu wa Wilaya kuwa ndani ya majengo ya Halmashauri ya Wilaya. Je, Serikali haioni kuwa, kuna umuhimu wa kujenga haraka sana ili kutenganisha mamlaka hizi mbili? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili; kutokana na majengo yaliyopo sasa hivi yaliyojengwa mwaka 1974 maana yake ni miaka 50 iliyopita. Je, Serikali haioni kuna umuhimu sasa wa kutujengea majengo ya kisasa? Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, kwanza ninamshukuru Mheshimiwa Mbunge amefuatilia mara kadhaa kuhusiana na uhitaji wa kujenga majengo haya mawili; Ofisi ya Mkuu wa Wilaya Urambo, pamoja na jengo la halmashauri.

Mheshimiwa Spika, kwa bahati nzuri Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa amewahi kuwa Mkuu wa Wilaya ya Urambo, kwa hiyo, lile jengo la ofisi Mheshimiwa Waziri Mkuu amelitumia na sisi tumetoa kipaumbele kuhakikisha kwamba mwaka ujao wa fedha tunaanza ujenzi wa

jengo la Ofisi ya Wilaya ya Urambo ili liwe la kisasa na kutoa huduma bora kwa wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pili, nimhakikishie tu kwamba, jengo la halmashauri litakalojengwa pamoja na jengo la Mkuu wa Wilaya ni majengo ya kisasa na ndio maana ombi la fedha shilingi bilioni 5.75 ni majengo yale ya kisasa ya ghorofa ambayo tunaamini yatatoa huduma bora kwa wananchi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Almasi Maige, swali la nyongeza.

**MHE. ATHUMAN A. MAIGE:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru sana. Kwanza ninatoa shukrani nyingi kwa Mama Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kutujengea jengo jipya kabisa la halmashauri na ukumbi wa mikutano. Sasa ni lini Serikali itajenga Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Uyui? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, Serikali imeweka mpango mkakati wa ujenzi wa majengo ya Wakuu wa Wilaya kote nchini na mpaka sasa zaidi ya majengo 127 ya halmashauri pamoja na ofisi za Waheshimiwa Wakuu wa Wilaya zinajengwa na mpango huu ni endelevu.

Mheshimiwa Spika, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, kwamba Halmashauri ya Wilaya ya Uyui ni moja ya halmashauri ambazo pia zimewekwa kwenye mpango kwa ajili ya kujengewa majengo ya Wakuu wa Wilaya. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Mwita Waitara, swali la nyongeza.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Spika, ahsante! Halmashauri ya Tarime *DC* ina vijiji 88 na vitongoji 500, Serikali ya Mama Dkt. Samia imetupa gari zuri kwa ajili ya afya. Mkuu wa Wilaya hana gari, kwa hiyo, kwa sasa lile gari la afya linafanya kazi za Mkuu wa Wilaya. Nini hatua ya haraka ya Serikali kumpa

*DC* wa Tarime gari, ili gari hilo lihudumie wananchi wangu wa Tarime Vijijini? Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Sasa swali la msingi lilikuwa linahusu Ofisi ya Mkuu wa Wilaya, hapa naona ni swali linalohusu gari na mimi sitaki kumweka Mheshimiwa Naibu Waziri katika mazingira ambayo anaweza asijibu swali hilo kikamilifu na kanuni zinataka ajibu kikamilifu. Mheshimiwa Naibu Waziri swali linaweza kuja kama swali la msingi, lije kama swali la msingi?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ndiyo.

**SPIKA:** Sawa, basi litaenda kama swali la msingi ili alete majibu ambayo yanatosheleza kwa mujibu wa kanuni zetu. Mheshimiwa Aziza Sleyum Ally, Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake.

Na. 49

**Muda wa Utoaji wa Vibali vya Ujenzi Nchini**

**MHE. AZIZA S. ALLY** aliuliza:-

Je, Vibali vya Ujenzi hutolewa baada ya muda gani tangu mwombaji aombe kupewa kibali?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, upatikanaji wa vibali vya ujenzi unasimamiwa na Mwongozo wa Utoaji wa Vibali vya Ujenzi na Usimamizi wa Ujenzi wa Majengo wa Mwaka 2018. Mwongozo huo umeweka muda na taratibu za utoaji wa vibali kulingana na aina ya jengo linaloombewa kibali.

Mheshimiwa Spika, Serikali imekamilisha Mfumo wa Kielektroniki wa Utoaji wa Vibali vya Ujenzi wa *TAUSI* na umeanza kutumika Julai, 2024 kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa, ambapo halmashauri 47 tayari zinatumia katika kutoa vibali vya ujenzi na halmashauri nyingine zitaanza kutumia. Kupitia mfumo huo, muda wa kutoa vibali umepungua, ambapo kwa sasa kibali kinaweza kutolewa ndani ya siku moja.

**SPIKA:** Mheshimiwa Aziza Sleyum Ally, swali la nyongeza.

**MHE. AZIZA S. ALLY:** Mheshimiwa Spika, swali la kwanza; kwa kuwa kuna utaratibu mpya wa kielektroniki wa kupata hivi vibali; je, kibali hicho, kitadumu kwa muda gani tangu kimetolewa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili; je, wameshatoa elimu katika maeneo mbalimbali kwa wananchi ili waweze kujua kama kuna mfumo mpya; wale wananchi wa Mbeya Mjini waweze kufahamu, wananchi wa Tabora na maeneo mengine waweze kufahamu? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa swali hilo muhimu sana.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Mfumo wa Utoaji wa Vibali vya Ujenzi siku za nyuma tulikuwa tunatumia mfumo wa kawaida ambapo mwombaji aliwasilisha makabrasha, ramani na viambatisho muhimu kwa ajili ya kupata vibali.

Mheshimiwa Spika, vibali hivyo vinachukua kati ya siku saba hadi 14 kwa majengo ya kawaida na kati ya siku 14 hadi ya 30 kwa majengo ya ghorofa. Hata hivyo, baada ya kuona kuna maeneo vibali hivi vinacheleweshwa, Serikali ikaanzisha Mfumo wa Kielektroniki wa *TAUSI* ambao mwombaji ana uwezo wa kupata kibali ndani ya siku moja, lakini kibali hicho kitadumu muda wote wa ujenzi wa jengo husika.

Mheshimiwa Spika, pili, kuhusiana na elimu, tunaendelea kutoa elimu kwa wananchi, kwanza kutambua kwamba kuna mfumo huu na namna ya kuutumia. Lakini pia wataalam wote katika halmashauri zetu wamepewa maelekezo ya kuendelea kutoa elimu na kuwasaidia wananchi ili waanze kuutumia mfumo huu muhimu. Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Joseph George Kakunda, Mbunge wa Sikonge, sasa aulize swali lake.

Na. 50

**Kujenga Zahanati kwenye Vijiji vyote Nchini**

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itatekeleza mkakati wa kujenga Zahanati kwenye Vijiji vyote nchini?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kutekeleza Mpango wa Maendeleo ya Afya ya Msingi kwa lengo la kusogeza huduma za afya karibu na wananchi. Aidha, katika kipindi cha Mwaka wa Fedha 2020/2021 hadi Septemba, 2024, Serikali imejenga na kukamilisha jumla ya zahanati 980 kote nchini.

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa zahanati katika vijiji na mitaa umefanyika kimkakati kwa kuzingatia idadi ya watu na umbali kutoka kijiji na kijiji au mtaa na mtaa badala ya kila kijiji na kila mtaa kujenga zahanati. Hivyo, Serikali inaendelea kutenga fedha katika bajeti, kwa ajili ya ujenzi wa zahanati za kimkakati katika maeneo yote nchini.

**SPIKA:** Mheshimiwa Joseph Kakunda, swali la nyongeza.

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA:** Mheshimiwa Spika, nimepokea hii taarifa ya zahanati 980 katika kipindi hicho ambacho katika Halmashauri ya Sikonge tulipata Zahanati tatu za Kidete, Mwamayunga na Mkola. Sasa tumebakiza maboma 13 ambayo wananchi wameyafikisha kwenye lenta na tunahitaji milioni 650. Swali la kwanza; je, lini tutapewa hizo fedha ili kukamilisha maboma 13 yaliyobaki?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; sera ya kila kijiji zahanati na kila kata kituo cha afya ni ya mwaka 2007, ni ya Serikali. Sasa leo tunaambiwa umbali, badala ya kila Kijiji; hii sera imebadilishwa lini na Serikali? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, Kwanza niwapongeze wananchi wa Jimbo la Sikonge kwa namna ambavyo wameendelea kuchangia nguvu zao katika ujenzi wa zahanati na kuwa na maboma 13 ambayo yamekwishapauliwa na kwa mujibu wa Mheshimiwa Mbunge yanahitaji takribani milioni 630 kwa ajili ya ukamilishaji.

Mheshimiwa Spika, ninaomba tu nimhakikishie kwamba Serikali hii ya Awamu ya Sita, inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan imeweka kipaumbele cha hali ya juu katika kuchangia nguvu za wananchi kukamilisha maboma haya na ndio maana maboma 980 yamekamilishwa na Sikonge imepata maboma matatu. Tutaendelea kutenga fedha hizo kwa awamu ili kukamilisha majengo hayo.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kumwelekeza Mkurugenzi wa Sikonge kutenga fedha kwenye mapato ya ndani, kuweka vipaumbele kwenye zahanati ambazo zinahitajika kwa haraka zaidi na wananchi kwa ajili ya ukamilishaji.

Mheshimiwa Spika, pili, Mpango wa Maendeleo ya Afya ya Msingi ni mpango uliobuniwa na ulibuniwa mwaka 2006, ulipangwa kukamilika mwaka 2017. Mpango huu ulikuwa unaelekeza; kujenga hospitali ya halmashauri kwa kila

halmashauri, ujenzi wa kituo cha afya kwa kila kata, ujenzi wa zahanati kwa kila kijiji na ujenzi wa zahanati kwa kila mtaa.

Mheshimiwa Spika, kiuhalisia, tuna vijiji zaidi ya 12,000, mitaa zaidi ya 4,000, kata zaidi ya 3,500 na halmashauri zaidi ya 184. Kiuhalisia hatuwezi kujenga zahanati kwenye kila mtaa, iko mitaa mingine ni midogona iko jirani sana, itakuwa ni *misuse of resources* kujenga zahanati kila mtaa, lakini pia itakuwa ni *burden* kubwa sana kwa Serikali kwa maana ya *wage bill* kuwa na zahanati kila kijiji, mtaa na kata kuwa na kituo cha afya.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tume-*review* ule Mpango wa Maendeleo ya Afya ya Msingi wa 2006 – 2017, sasa tunakwenda kimkakati, tunaangalia *factors* kwa maana ya idadi ya wananchi na umbali kutoka kituo cha jirani cha huduma na ndiyo maana tunajenga kimkakati. Hii itakuwa na faida zaidi kwa vituo hivyo kuliko kujenga kila sehemu kituo ambacho hakitokuwa na tija. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Twaha Mpembenwe, swali la nyongeza.

**MHE. TWAHA A. MPEMBENWE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana, kumekuwa na changamoto kubwa sana kwenye Zahanati ya Nyamisati, kwenye Kata ya Salale ukizingatia kwamba zahanati ile inahudumia Wilaya mbili za Mafia pamoja na Kibiti. Je, nini kauli ya Serikali katika kuhakikisha wanajenga Kituo cha Afya kwenye Kata ya Salale?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, kata zote ambazo zinakidhi vigezo kwa ajili ya ujenzi wa vituo vya afya tulishafanya kazi ya kuziainisha katika halmashauri zetu zote 184, ikiwemo Halmashauri ya Kibiti.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ninaomba tu nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge ikiwa hii kata ambayo Zahanati ya Nyamisati ipo, kwenye kata ambazo zimeainishwa, tutaipa kipaumbele, lakini kama haipo na unahitaji kujenga kituo cha

afya, basi nimwombe Mheshimiwa Mbunge ashirikiane na Mkurugenzi na *DMO* waweze kuwasilisha ili iingizwe kwenye mpango wa kujenga vituo vya afya. Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Salim Alaudin Hasham, Mbunge wa Ulanga, sasa aulize swali lake.

Na. 51

**Ujenzi wa Daraja Linalounganisha Kata ya Mwaya na Mbuga – Mahenge**

**MHE. SALIM A. HASHAM** aliuliza:-

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa Daraja linalounganisha Kata ya Mwaya na Mbuga lililovunjika tangu mwaka 2023?

**SPIKA:** Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Zainab Katimba, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imekamilisha usanifu wa daraja la kudumu litakalounganisha Kata ya Mwaya na Mbuga ambapo inakadiriwa kugharimu shilingi bilioni 3.724 na kuwekwa kwenye mpango wa fedha za matengenezo ya dharura chini ya wabia ambao ni Benki ya Dunia. Kwa sasa, Serikali ipo kwenye hatua za mwisho kwenye mchakato wa manunuzi na utakapokamilika ujenzi wa daraja hilo utaanza mara moja.

**SPIKA:** Mheshimiwa Salm Alaudin Hasham, swali la nyongeza.

**MHE. SALIM A. HASHAM:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Kwanza ninashukuru sana Serikali kwa kuwa tayari kujenga daraja hilo, lakini ili daraja liwe na tija zaidi ni lazima kukamilisha ujenzi wa

barabara kwa kutoboa ili kuunganisha kati ya barabara ya Wilaya ya Liwale pamoja na Ulanga inayopita katikati ya Mbuga ya Mwalimu Nyerere. Sasa ni lini Serikali itakuwa tayari kufungua barabara hiyo ili kuunganisha Mikoa ya Kusini pamoja na Morogoro?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, je, ni lini Serikali itaunganisha barabara ya kutoka Makanga – Mafinji ili kuunganisha Wilaya ya Ulanga na Malinyi na kurahisisha usafiri, kwa sababu sasa hivi wananchi wanazunguka kilomita 80 ili kufika Wilaya ya Malinyi? Ila barabara hiyo ikiisha itakuwa inapitika kwa kilomita 30 peke yake. Je, ni lini Serikali itaona umuhimu wa kumalizia barabara hiyo? Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa sasa hilo ni la tatu, umeshauliza mawili tayari.

**MHE. SALIM A. HASHAM:** Mheshimiwa Spika, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Spika, kwanza ninaomba nimpongeze sana Mheshimiwa Mbunge, kwa kweli amekuwa akifanya ufuatiliaji mkubwa sana katika masuala haya ya kupata barabara katika jimbo lake, lakini pia katika maeneo mengine.

Mheshimiwa Spika, katika swali la kwanza la Mheshimiwa Mbunge, ametaka kujua ni lini na mkakati wa Serikali ni upi katika kuhakikisha kwamba inajenga barabara ile ambayo itaunganisha Wilaya ya Liwale pamoja na Wilaya hii ya Ulanga ambayo kimsingi ni Mkoa wa Morogoro na Mkoa wa Lindi.

Mheshimiwa Spika, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba taratibu ambazo zinahitajika hapa ni kuhakikisha kwamba barabara hii inapandishwa hadhi, ili sasa iweze kuwa barabara ya mkoa ambayo inaunganisha mkoa mmoja na mkoa mwingine.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kupitia *Road Board*, waanzishe mchakato huu ili barabara hii iweze kupandishwa hadhi, lakini pia iweze kufanyiwa upembuzi yakinifu, kwa sababu barabara itapita katika eneo la Hifadhi ya *Selous*. Kwa hiyo, inahitajika upembuzi yakinifu kwenye upande wa mazingira. Baada ya kukamilisha taratibu hizo barabara hii itajengwa ili iweze kuwa na tija kubwa kwa ajili ya wananchi.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na swali lake la pili, Mheshimiwa Mbunge anauliza kuhusiana na ujenzi wa Barabara ya Makanga na Mafinji ambayo kimsingi ina kilometa 35 tofauti na barabara inayotumika sasa hivi ile njia ya Lupilo ambayo ina urefu wa kilometa 80. Ninaomba kumtaarifu Mheshimiwa Mbunge kwamba barabara hii kwa kilometa 30 tayari imeshafunguliwa katika mwaka wa fedha 2021/2022 na 2023/2024 kwa gharama ya shilingi bilioni 1.061.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2024/2025, Serikali imetenga shilingi 200,000,000 kwa ajili ya ujenzi wa ma-*culvert* makubwa mawili. Ninamhakikishia Mheshimiwa Mbunge mchakato wa manunuzi unaendelea na pindi utakapokamilika, barabara hii itajengewa ma-*culvert* hayo makubwa mawili.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na kilometa tano zile zinazobakia katika kilometa hizi 35, katika Mwaka wa Fedha 2025/2026, tumeweka katika Mpango ujenzi wa ma-*culvert* 15, lakini pia itatengewa fedha shilingi 900,000,000 kwa ajili ya kukamilishwa. Kwa hiyo ninakuhakikishia Mheshimiwa Mbunge, Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ipo kazini kuhakikisha kwamba katika jimbo la Mheshimiwa Mbunge, wanapata miundombinu ya barabara iliyo bora.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora, Mheshimiwa Omar Ali Omar, Mbunge wa Wete, sasa aulize swali lake.

Na. 52

**Kufanya Mapitio katika Kubaini Kaya Maskini**

**MHE. OMAR ALI OMAR** aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kufanya mapitio katika kubaini kaya maskini ili kuondoa malalamiko?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Utumishi na Utawala Bora, Mheshimiwa Deus Sangu, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, *TASAF* imekuwa ikitumia utaratibu wa kutambua na kuandikisha kaya maskini kupitia Mkutano Mkuu wa Kijiji, Mtaa au Shehia kwa usimamizi wa watendaji kutoka maeneo ya utekelezaji kwa kuzingatia vigezo vilivyoainishwa na jamii husika.

Mheshimiwa Spika, katika kushughulikia malalamiko ya walengwa, wananchi na viongozi kuhusu utekelezaji wa Mpango wa *TASAF* imekuwa ikitumia njia mbalimbali ikiwemo kufanya uhakiki ili kuziondoa katika Mpango kaya zilizoimarika kiuchumi. Katika mapitio yaliyofanyika kwenye kaya 750,000 kutoka vijiji, mitaa na shehia 12,000 ilibainika kuwa kaya 394,505 zimeimarika kiuchumi na hivyo kukidhi vigezo vya kuhitimu na kutoka katika Mpango. Aidha, kwa sasa Serikali ipo kwenye maandalizi ya usanifu wa Mpango utakaofuata baada ya Mpango wa sasa kufika katika ukomo hapo Septemba, 2025. Ninashukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Omar Ali Omar, swali la nyongeza.

**MHE. OMAR ALI OMAR:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; kwenye Jimbo langu la Wete kuna wananchi ambao wametolewa katika mfuko huu kimyakimya. Je, Serikali inafahamu mpango huo?

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili; Mheshimiwa Waziri yuko tayari kuongozana nami baada ya kumalizika kwa Bunge hili ili kwenda kuona na kutatua changamoto ambazo zimejitokeza katika jimbo langu kwenye Mfuko huu wa *TASAF*?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nampongeza Mheshimiwa Omar Ali kwa namna ambavyo amekuwa akifuatilia masuala haya yanayohusu *TASAF*.

Mheshimiwa Spika, kuhusu wananchi wake kuondolewa kimyakimya, utaratibu uliopo ambao umewekwa na *TASAF* ni kwamba, wale wanaohitimu na kuimarika kiuchumi, kabla hawajaondolewa, kwanza wanapewa mafunzo na kuwaandaa na baadaye kupewa taarifa rasmi kwamba sasa mmefikia kwenye ukomo. Kama jambo hilo limetokea jimboni kwake, naomba kuchukua fursa hii kumwelekeza Mtendaji Mkuu wa *TASAF* afuatilie jambo hili na kama hawa hawakutaarifiwa, waweze kupata taarifa kufuatana na taratibu tulizoweka.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kufuatana naye kwenda jimboni, hili halina shaka, tukimaliza Shughuli za Bunge hapa tutaenda huko Pemba ili tukaone namna ya kuzungumza na kutatua changamoto hizi kwa pamoja. Ninakushukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Shally Josepha Raymond, swali la nyongeza.

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa *TASAF* haiwezi kugusa maskini wote wa Tanzania na kwa kuwa maskini waliopo ni wengi sana sana wakiwemo vijana waliomaliza vyuo ambao hawana kazi bado wanategemea wazazi; wakiwemo wanawake ambao wanangoja kuguswa tu ili waweze kufanya miradi, wakiwemo pia hata akinababa ambao hawawezi kumudu chakula kwenye nyumba zao. Je, Serikali haioni sasa ni wakati wa kutoa miradi midogomidogo kwa makundi hayo niliyotaja badala ya kusema wote wakaguswe na *TASAF*? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana. Kama Programu ya *TASAF* ilivyo, ina programu ambayo tulianza 2012 – 2019 na tuko awamu ya pili katika kunusuru kaya maskini ambayo itaenda 2019 mpaka 25 Septemba, mwakani. Serikali ina utaratibu mzuri, kuna namna ambavyo inawezesha haya makundi kwa mfano kupitia halmashauri kuna mikopo ya *4:4:2* na yote hii ni namna ambayo Serikali imejipanga namna ya kuwakwamua wananchi katika umaskini.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo na pamoja kwamba kuna Programu ya *TASAF*, bado pia Ofisi ya Waziri Mkuu ina programu ya mikopo kwa vijana ambayo inafanya ushirikiano pia pamoja na *TASAF* ambao wale vijana wanaotoka kaya maskini, wanaoshindwa, wanamaliza darasa la saba na kutokufanikiwa kwenda kidato cha kwanza, wameunganishwa na programu ya kwenda Ofisi ya Waziri Mkuu kupata mikopo ya kusomeshwa *VETA* bure. Ninashukuru. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Mhandisi Samwel Hhayuma, swali la nyongeza. Au ni nani? Aah! samahani, Mheshimiwa Charles Kajege, swali la nyongeza.

**MHE. CHARLES M. KAJEGE:** Mheshimiwa Spika, *TASAF* kwa kweli bado ni tatizo kubwa katika jimbo langu. Wengi waliomo mle hawastahili na walioachwa ndiyo wanastahili. Ninaomba kama akipata nafasi tuweze kuongozana naye kwenda Mwibara ili kuondoa hili tatizo ambalo limejitokeza, je, yuko tayari? Ninakushukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Spika, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Kajege kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, kama nilivyosema kwenye jibu langu la msingi, utaratibu wa kuwapata wanufaika wa kaya

maskini ulifanyika kupitia mikutano ya vijiji. Kwa hiyo vijiji na wananchi ndiyo waliamua nani anufaike na nani asiingie kwenye kunufaika.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo *TASAF* kwa maana ya *TASAF* waliletewa watu ambao tayari wamepitia katika michakato ya kijiji. Kama kuna tatizo kwenye jimbo lako Mheshimiwa Kajege, kupitia Bunge hili ninaomba kumuahidi tutafika huko ili tuone namna ya kutatua changamoto hii.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ninadhani kwa sababu watu katika umaskini ni kama katika utajiri, kuna wanaoingia na kutoka na kuna wanaoingia na kutoka. Kwa hiyo ninafikiri ni zoezi ambalo linapaswa kuwa endelevu kuwatambua wale ambao waliingia wanapaswa kutoka na wale ambao hawakuingia wanapaswa kuingia au ambao walitolewa wanaopaswa kurejea kwa sababu ya hali waliyonayo, kwa sababu hapa kila Mheshimiwa Mbunge atasimama aanze kueleza kwake wako wangapi. *(Makofi)*

Sasa hilo ninafikiri kama ulivyotoa maelekezo kwa *TASAF*, unaweza kuyatoa hayo ili ufuatiliaji uwe wa karibu zaidi kwa wale watu waliomo kama bado wanaendelea kuwemo na wengine ambao wanajitokeza ili waweze kupata hiyo huduma.

Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana…

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Spika, ahsante.

**SPIKA:** …kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Mheshimiwa Maryam Azan Mwinyi, Mbunge wa Viti Maalum, swali lake litaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Soud Mohammed Jumah.

Na. 53

**Serikali Kudhibiti Athari katika Bonde la Tibirinzi Chakechake Pemba**

**MHE. SOUD MOHAMMED JUMAH K.n.y. MHE. MARYAM AZAN MWINYI** aliuliza: -

Je, Serikali ina mkakati gani kunusuru vipando visivyohimili maji ya bahari katika Bonde la Tibirinzi Chakechake Pemba?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Mheshimiwa Hamza, majibu tafadhali.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kushirikiana na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inaendelea kuchukua hatua mbalimbali za kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi. Hatua hizo ni pamoja na ujenzi wa matuta ya kuzuia maji bahari yasiingie katika mabonde ya kilimo ikiwemo Kisiwa Panza, Kilimani, Msuka, Sipwese, Micheweni na Tovuni; na upandaji wa miti ya aina mbalimbali ikiwemo mikoko/mikandaa katika maeneo ya ufukwe ili kupunguza kasi ya uingiaji wa maji ya bahari katika maeneo ya kilimo.

Mheshimiwa Spika, aidha, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kushirikiana na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inaendelea kutafuta fedha kutoka katika vyanzo mbalimbali kwa ajili ya kuendelea kuweka miundombinu wezeshi inayozuia maji ya bahari kuingia katika makazi na maeneo ya kilimo ikiwemo Bonde la Tibirinzi. Lengo kuu ni kuhakikisha wananchi wanaendelea kutumia maeneo hayo kwa shughuli za kilimo na uchumi.

Mheshimiwa Spika, vilevile, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kushirikiana na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeandaa Mpango wa Kuirithisha Zanzibar ya Kijani ambao unalenga kuelimisha umma kuhusu umuhimu wa uhifadhi na

utunzaji wa misitu, na miti iliyopo na upandaji na utunzaji wa miti hususani kwenye maeneo ya fukwe ili kukabiliana na changamoto ya mabadiliko ya tabianchi.

Mheshimiwa Spika, ninakushukuru.

**SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Soud Mohammed Jumah, swali la nyongeza.

**MHE. SOUD MOHAMMED JUMAH:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, nina maswali mawili ya nyongeza kwa niaba ya Mheshimiwa Maryam Mwinyi. Swali la kwanza; kwa kuwa uharibifu wa misitu ya mikoko umepelekea maji ya bahari kupanda juu na kuingia katika mashamba ya kilimo ya wananchi Kisiwani Pemba na kupelekea uzalishaji wa mazao kuwa hafifu. Je, Serikali ina mpango gani wa kumaliza ujenzi wa Tuta la Sipwese ili kupunguza maji ya bahari yasiingie katika mashamba ya wananchi?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; je, Mheshimiwa Naibu Waziri, upo tayari kufanya ziara kuona uharibifu wa mikoko na athari zake ili kuharakisha upatikanaji wa fedha kwa ajili ya kuhami na kurejesha misitu ya mikoko Kisiwani Pemba? Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Spika, kwanza ninataka kumwambia Mheshimiwa Mbunge kwamba Sipwese pale tuna miradi miwili. Tuna miradi miwili, lakini yote ni ya ujenzi wa hayo matuta. Mmoja tayari umeshakamilika kwa asilimia zote na umeanza kuleta manufaa kwa wananchi, lakini mwingine hivi sasa upo kwenye 80% ambayo jumla ya shilingi bilioni 1.1 zilitumika kwa ajili ya ujenzi wa mradi huo.

Mheshimiwa Spika, nimwambie tu Mheshimiwa kwamba tarehe 24 Septemba, 2024, mimi na Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais Mheshimiwa Dkt. Kijaji, tulifanya ziara katika eneo hilo la Sipwese na tulitoa maelekezo kwa mkandarasi ili ukuta ule uweze kumalizika kwa haraka. Tulikubaliana baada ya

miezi miwili kwa maana kwamba mwezi Desemba ukuta ule utakuwa umeshakamilika. Nimwambie tu Mheshimiwa, awe na subira, tayari mkandarasi yupo *site* na ujenzi unaendelea.

Mheshimiwa Spika, linguine, nimwambie tupo tayari kwenda Pemba kuona hali ilivyo na kuona namna ambavyo tunaweza kuziomba fedha kwa haraka ziweze kutatua changamoto hiyo kwa sababu tumepanga sasa Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, kila mwezi tutakuwa tuna siku tatu za kwenda kufanya ziara Zanzibar ikiwemo Unguja na Pemba kwa ajili ya kuona miradi lakini kuona changamoto kubwa ya athari ya mabadiliko ya tabianchi. Kwa hiyo tuko tayari kwenda Pemba.

**SPIKA:** Mheshimiwa Simai Hassan Sadiki, swali la nyongeza.

**MHE. SIMAI HASSAN SADIKI:** Mheshimiwa Spika, je, ile dhamira ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kushirikiana na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar juu ya ujenzi wa ukuta maeneo ya fukwe za bahari kule Nungwi imefikia wapi? Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Spika, dhamira ya Serikali zote mbili Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ni kuendelea kutatua changamoto ikiwemo changamoto inayotatiza katika eneo la Kijiji cha Nungwi kama ambavyo Mheshimiwa Simai ameiona. Ninamwambia Mheshimiwa aendelee kuwa na subira, tunatafuta fedha, zitakapopatikana, basi Nungwi tunakwenda kufanya jambo kubwa la ujenzi wa ukuta kwa ajili ya kuzuia maji ya bahari yasiingie kwenye mitaa. Ninakushukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Hamida Abdallah, swali la nyongeza.

**MHE. HAMIDA M. ABDALLAH:** Mheshimiwa Spika, ninaomba kuuliza swali, Mheshimiwa Naibu Waziri nilishamwomba kuja Lindi kuangalia bahari namna ilivyokula nchi kavu. Sasa, ni lini atakuja

Lindi kuangalia ili kutafuta suluhu na kuokoa nchi kavu kwa namna ambavyo inaliwa? Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Spika, niko tayari kwenda Lindi na ninamwahidi sasa tena kwa mara ya mwisho Mheshimiwa Hamida kwamba baada ya Bunge hili, tutakwenda Lindi kwenda kuona changamoto na kuona namna ambavyo tunakwenda kushughulikia changamoto ya maji ya bahari pale Lindi. Kwa hiyo baada ya Bunge hili tutakwenda Lindi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ukiwa unamaanisha Jumamosi ijayo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Spika, haina maana hiyo, lakini tukimaliza Bunge hili basi tutapanga siku twende Lindi.

**SPIKA:** Maana umesema mara ya mwisho. Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Mheshimiwa Hawa Subira Mwaifunga, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 54

**Kiswahili Kutumika katika Bunge la *SADC***

**MHE. HAWA S. MWAIFUNGA** aliuliza:-

Je, kwa nini Lugha ya Kiswahili haitumiki kwenye Bunge la *SADC* kama ilivyo kwenye Bunge la *PAP* ambapo ni lugha rasmi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Mheshimiwa Cosato David Chumi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE (MHE. COSATO D. CHUMI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa ni mara yangu ya kwanza kujibu swali kwenye Bunge lako Tukufu, ninaomba uridhie kwa sekunde chache, kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu, pili nimshukuru Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuniamini na kuniteua kuwa Naibu Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Spika, kadhalika, ninakushukuru wewe binafsi kwa uongozi wako na malezi na pia ninawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania hususan Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama ambayo nilihudumu kwa miaka tisa, pamoja na wananchi wa Jimbo la Mafinga Mjini kwa ushirikiano wanaonipa katika kulitumikia Taifa letu. Ninaahidi kuendelea kutekeleza majukumu yangu ipasavyo kwa utii, bidii na moyo wa kujituma ikiwemo kusimamia utekelezaji wa Sera ya Mambo ya Nje na Ilani yetu ya Chama Cha Mapinduzi ya mwaka 2025. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, ninaomba sasa kujibu swali namba 54 la Mheshimiwa Hawa Subira Mwaifunga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, itakumbukwa kuwa, Mkutano wa 39 wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa *SADC* uliofanyika Mwezi Agosti, 2019 uliridhia pendekezo la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuhusu Lugha ya Kiswahili kuwa lugha ya kazi katika Mikutano ya Wakuu wa Nchi na Serikali wa *SADC*. Mheshimiwa Rais pia alitumia Lugha ya Kiswahili katika Mkutano wa 44 wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa *SADC* uliofanyika Zimbabwe tarehe 17 Agosti, 2024.

Mheshimiwa Spika, kufuatia hatua hiyo, Lugha ya Kiswahili ilianza na imeendelea kutumika katika Mikutano ya Wakuu wa Nchi na Serikali ya *SADC* na Mikutano ya Baraza la Mawaziri la *SADC*. Aidha, Tanzania inaendelea na ushawishi ili kukiwezesha Kiswahili kutumika katika Mikutano ya Makatibu Wakuu pamoja

na Vyombo na Taasisi nyingine ikiwemo Jukwaa la Wabunge la *SADC*. Kadhalika, Tanzania inaendelea na ushawishi wa kukifanya Kiswahili kuwa lugha rasmi ya nne ya Jumuiya ya *SADC* kupitia mapendekezo ya maboresho ya Mkataba wa Uanzishwaji wa *SADC* wa mwaka 1992.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kuwasilisha.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Hawa Subira Mwaifunga, swali la nyongeza.

**MHE. HAWA S. MWAIFUNGA:** Mheshimiwa Spika, swali la kwanza; Kiswahili kinatambulika kama lugha ya nne kwa nchi za Afrika, lakini Bunge la Afrika linatumia Lugha ya Kiswahili katika vikao vyake. Nini kigugumizi cha kuzungumza Kiswahili katika Jukwaa la *SADC*?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; changamoto kubwa ya Kiswahili katika Jukwaa la *SADC* inaonekana ni ufinyu wa bajeti kwa ajili ya wakalimani. Je, Serikali haioni sasa ni wakati mzuri wa kutumia jukwaa hilo ili kuweka wakalimani ili kuweza kuzungumza Kiswahili ambacho tutaweze kukitangaza katika Nchi za *SADC* kwa ukubwa wake? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE (MHE. COSATO D. CHUMI):** Mheshimiwa Spika, ninaomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Hawa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza ninapenda kumhakikishia na kulihakikishia Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na wananchi kwa ujumla kwamba hapakuwa na kigugumizi na ndiyo maana kumekuwepo na jitihada mpaka sasa. Pamoja na kuwa Kiswahili siyo lugha rasmi kati ya zile lugha rasmi za *SADC*, lakini kinatumika katika Mikutano ya Wakuu wa Nchi na Wakuu wa Serikali na ngazi ya Mawaziri.

Mheshimiwa Spika, jitihada zinafanyika na kwa sasa, ili lugha iwe rasmi, lazima mabadiliko ya kanuni na miongozo ndani ya

*SADC* yaweze kufanyiwa kazi ambayo Tanzania imekuwa mstari wa mbele kuhakikisha kwamba kipengele kile kinafanyiwa marekebisho ili kuifanya Lugha ya Kiswahili kuwa lugha ya nne rasmi katika shughuli zote za *SADC*.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na wakalimani, ni kweli kuna gharama kubwa sana za kugharamia masuala mazima ya kufanya ukalimani. Hata hivyo, kwa ushawishi, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeshawishi na kujenga hoja ili kusudi mzigo ule uweze kubebwa kwa ushirikiano kati ya Tanzania na *SADC*. Kwa sasa *SADC* katika mikutano inayoendelea, wamekubali kugharamia wakalimani katika shughuli zote zinazoendelea. Ninakushukuru. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Anatropia Lwehikila Theonest, swali la nyongeza.

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru, pamoja na majibu ya Mheshimiwa Waziri, bado tunakabiliwa na changamoto ya upatikanaji wa wakalimani. Kwa uzoefu nimeona, inafikia wakati wanaletwa Wakalimani wa Kenya katika Bunge la Afrika ambao wakati mwingine hata lafudhi yao siyo nzuri. Ni nini mkakati wa Serikali kuhakikisha wanaweza kusomesha wakalimani wa kutosha siyo tu kwa ajili ya kupelekwa kufanya ukalimani, lakini pia kuwapeleka dunia nzima ili waweze kufanya kazi ya kutangaza na kufundisha Kiswahili? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE (MHE. COSATO D. CHUMI):** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Anatropia, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ndani ya Serikali kumekuwa na jitihada za kuhakikisha kwamba, Kiswahili pamoja na kuwa ni lugha yetu ya Taifa, lakini tunaifanya kama bidhaa, kwamba, tuwe na wakalimani wa kutosha katika maeneo mbalimbali kwa sababu, kwa kufanya hivyo wao pia, watatuingizia mapato kupitia fedha za kigeni. Mojawapo ya jitihada ni kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu, kushirikiana na wenzetu wa BAKITA, kushirikiana na vyuo

kwa sababu, ukalimani nao ni taaluma. Watu wengi hudhani kwamba, kwa kujua tu Kiswahili na Kingereza au Kiswahili na Kifaransa, basi *automatically* utakuwa mkalimani.

Mheshimiwa Spika, ukalimani ni taaluma. Kwa hiyo, tunatoa wito kwa vyuo vyetu chini ya usimamizi wa Wizara ya Elimu ya Juu kuhakikisha kwamba, wanatoa mafunzo ya ukalimani kama taaluma, ili na sisi tunapotembea katika mikutano mbalimbali duniani tukutane na wakalimani ambao ni Watanzania.

**SPIKA:** Mheshimiwa Husna Sekiboko, swali la nyongeza.

**MHE. HUSNA J. SEKIBOKO:** Mheshimiwa Spika, katika hatua za kueneza Kiswahili duniani, Bunge liliwahi kuazimia na kuishauri Serikali kuweka madawati ya Kiswahili kwenye Balozi zetu. Je, Serikali imefikia hatua gani katika utekelezaji wa azimio hili? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa silikumbuki hilo azimio, lakini Mheshimiwa Waziri kama unayo majibu, tafadhali mjibu Mbunge.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE (MHE. COSATO D. CHUMI):** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi. Ninachoweza kumjibu Mheshimiwa Mbunge ni kwamba, jitihada zinafanyika siyo tu katika Balozi zetu kuwa na Madawati ya Kiswahili, lakini pia, hata kushawishi Balozi nyingine za nje zinazowakilishwa hapa nchini ziwe na taratibu mbalimbali za kuhakikisha kuwa, zinakuwa na kitu kama Madawati ya Kiswahili.

Mheshimiwa Spika, kumekuwepo pia na jitihada mbalimbali kwa mfano hivi karibuni kutakuwa na shughuli kubwa sana kule Havana, Cuba ambayo ni mojawapo ya jitihada za kukuza Kiswahili siyo tu katika ukanda wa Afrika Mashariki na katika Bara letu la Afrika, bali duniani kwa ujumla. Kwa hiyo, jitihada hizo zinafanyika kwa ushirikiano ndani ya Wizara ya Mambo ya Nje pamoja na wizara nyingine za kisekta, ikiwemo kama nilivyosema, Wizara ya Elimu pamoja na wenzetu wanaosimamia utamaduni kupitia Baraza la Kiswahili la Taifa pamoja na Baraza la Kiswahili la Zanzibar.

**SPIKA:** Mheshimiwa Vedastus Mathayo Manyinyi, swali la nyongeza.

**MHE. VEDASTUS M. MATHAYO:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa, Tanzania ndiyo waasisi wa Lugha ya Kiswahili na kwenye suala la Kiswahili huko duniani watu wengi wangependa kujua kusoma na kuandika. Ni kwa nini tusiwe na mikakati ya kuhakikisha kwamba, tunatoa walimu wengi kuwapeleka duniani, ili waweze kufundisha hiyo Lugha ya Kiswahili iweze kusambaa kwa haraka? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE (MHE. COSATO D. CHUMI):** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi na nashukuru kwa swali. Kama nilivyosema katika majibu yangu ya msingi na majibu mengine ya nyongeza, jitihada zinaendelea kufanyika kwa ushirikiano kati ya Wizara pamoja na Wizara za Kisekta, ili kuhakikisha kwamba, kama nilivyosema vyuo vyetu pia, vifundishe ukalimani kama taaluma. Kwa sababu, kujua tu Kiswahili kama lugha na kujua Kiingereza kama lugha haitoshi sisi kuwafanya wakalimani.

Mheshimiwa Spika, mimi mwenyewe nakumbuka wakati nafanya masomo yangu Amsterdam niliwahi kuombwa kuwa mkalimani, lakini ile nilikuwa nafanya kama ukalimani kwa sababu, najua Kiingereza na Kiswahili, lakini, ili tuwe na wanataaluma kabisa wa ukalimani ni lazima kama Serikali na kama nchi, tuwekeze katika kuhakikisha kwamba, tunakuwa na wanataaluma hao na kwa kweli, jitihada zinafanyika na ndiyo maana makongamano maeneo mbalimbali yanafanyika. Pia kilishakuwa katika mikutano mingi ya Kimataifa, hasa inayofanyikia hapa nchini, lugha inayotumika inakuwa Kiswahili na kuwa na vitendea kazi ambavyo vinatumika kama vile kufanya ukalimani kwa wale ambao hawajui Lugha ya Kiswahili.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE (MHE. COSATO D. CHUMI):** Mheshimiwa Spika, nakushukuru.

**SPIKA:** Wizara ya Afya, Mheshimiwa Nancy Hassan Nyalusi, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake. *(Makofi)*

Na. 55

**Serikali Kupeleka Mtaji *MSD***

**MHE. NANCY H. NYALUSI** aliuliza:-

Je, lini Serikali itapeleka mtaji *MSD?*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, Mheshimiwa Dkt. Godwin Mollel, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia mwezi Oktoba, 2024 Serikali imekwishatoa fedha kiasi cha shilingi bilioni 100 kama mtaji kwa Bohari ya Dawa *(MSD)* kati ya shilingi bilioni 561.5 iliyopangwa kutolewa. Serikali itaendelea kutoa fedha hizi kwa awamu kulingana na upatikanaji wake. Naomba kuwasilisha.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Nancy Nyalusi, swali la nyongeza.

**MHE. NANCY H. NYALUSI:** Mheshimiwa Spika, swali la kwanza; Mheshimiwa Naibu Waziri, hii shilingi bilioni 100 ni mtaji au amelipa deni kwa sababu, kwenye vitabu vya *MSD* inasomeka kama ni deni?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; kumekuwa na changamoto katika usambazaji wa vifaa tiba na dawa. Je, nini kauli ya Serikali? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, huu ni mtaji na Mheshimiwa Mbunge asisahau kwamba, kila mwezi *MSD* wanapewa shilingi bilioni 16.7 kwa ajili ya manunuzi ya dawa. Maana yake ni kila mwezi wanapata shilingi bilioni 16.7 na wamepewa hizi shilingi bilioni 100, ambazo wao wameamua kuelekeza kwenye kumalizia ujenzi wa viwanda.

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili amezungumzia suala la kwamba, kuna changamoto kwenye usambazaji wa vifaa tiba. Labda hiyo ni habari mpya, lakini hakuna changamoto kwenye usambazaji na ndiyo maana unasikia sasa hivi tumetumia zaida ya shilingi trilioni 6.7 kununua vifaa tiba na umeona vimesambazwa kwenye wilaya mbalimbali na wakati wote dawa zinafika kwenye wilaya mbalimbali. Kama kuna eneo ambalo umeliona lina changamoto, naomba uje kwenye kiti changu tujadili tuone kwa pamoja jinsi ya kulitatua.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, nakushukuru sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge…

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika…

**SPIKA:** …ama kuna swali lingine?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Ndiyo.

**SPIKA:** Ahaa! Sawa.

Mheshimiwa Subira Khamis Mgalu, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 56

**Mpango wa Serikali Kuanzisha M-Mama Pwani**

**MHE. SUBIRA K. MGALU** aliuliza:-

Je, Serikali imejipangaje kuanzisha mpango wa M-Mama katika maeneo ya Kibiti, Mafia na Mkuranga, ili kuzuia vifo vya akinamama wajawazito?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Mkoa wa Pwani ulianza kutumia mfumo wa M-Mama tarehe 15 Septemba, 2023. Mkoa huu umeingia mkataba na madereva ngazi ya jamii 112 ikihusisha madereva 14 toka Halmashauri ya Kibiti na Mafia wanaotumia boti. Hadi sasa jumla ya dharura 2,816 kutoka katika Halmashauri zote za Mkoa wa pwani zimesafirishwa kwa kutumia mfumo wa M-Mama.

Mheshimiwa Spika, naomba kusema kuwa mfumo huu unafanya kazi katika maeneo yote nchini. Hivyo, nawaomba Waheshimiwa Wabunge wote kwanza kuhamasisha wananchi juu ya matumizi ya namba 115 wawapo na dharura itokanayo na uzazi wakati wa ujauzito. Naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Subira Mgalu, swali la nyongeza.

**MHE. SUBIRA K. MGALU:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Kwanza nianze kumshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri kwa sababu, nimefuatilia, hasa maeneo ya visiwani, kama mpango huu kweli unaendelea. Maswali yangu mawili ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza; licha ya mpango huu wa M-Mama kufanya vizuri. Je, kuna sababu gani nyingine ambazo zimechangia kupunguza vifo vya akinamama wajawazito kutoka 556 kwa vizazi hai 100,000 hadi 104 kwa vizazi hai 100,000 kulinganisha na baadhi ya nchi ambazo zimeripoti vifo vya akinamama zaidi ya 386? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili; kwa kuwa, mpango huu wa M-Mama pia, una malengo ya kushughulikia changamoto za watoto wachanga wakiwemo watoto wanaozaliwa kabla ya muda, watoto njiti. Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga vituo, kwa ajili ya watoto njiti kwa kuwa, vifo vya

watoto njiti vinachangia 48% vya vifo vya watoto wote chini ya umri wa miaka mitano? Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, *yes.* Kwanza nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Mbunge, lakini niseme tu kwamba, kama mnakumbuka Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan alipohutubia kwa mara ya kwanza Bunge hili, akiwa amesimama hapo ulipo Mheshimiwa Spika, alipofika eneo la mama na mtoto alilisisitiza sana na kurudia mara mbili.

Mheshimiwa Spika, lakini hakuishia kwenye kusisitiza, ameleta shilingi trilioni 6.7 ambazo zimeenda kwenye maeneo ya miundombinu, teknolojia na pia, kufunza wataalamu na hizo fedha zote zimekwenda zikabadilisha, zikatutoa kwenye vifo 556 mpaka sasa tumefika vifo 104 na ni mfano wa kuigwa duniani. Kwa sababu tulikuwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu kwenye Mkutano wa Umoja wa Mataifa ni Marais wawili tu walikuwa wanapewa, kwenye eneo la afya nishani, kwa ajili ya kufanya vizuri. Rais wetu Dkt. Samia Suluhu alikuwa anapewa nishani kwenye eneo hili na walipoona Rais wetu hakuwepo akasema wenyewe watakuja Tanzania, kwa ajili ya kumshukuru. Wanataka waonane naye *physically* na kumpongeza na kumpa hiyo nishani yeye mwenyewe kwa hiyo, ni kazi kubwa imefanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pili, Mbunge amezungumzia eneo la watoto njiti. Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan ameshatutafutia shilingi bilioni 190. Siyo muda mrefu Waziri wetu tunaendelea na mchakato ndani ya Wizara ya Afya namna ya kujenga hivyo vituo vya watoto njiti na siyo muda mrefu Waziri wa Afya, Mheshimiwa Jenista Mhagama atakuja kutoa maelezo ni namna gani tunaweza kwenda mbele kwa kutumia hizo shilingi bilioni 190. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Wizara ya Maliasili na Utalii. Mheshimiwa Mhandisi Ezra John Chiwelesa, Mbunge wa Biharamulo Magharibi, sasa aulize swali lake.

Na. 57

**Ajira Kwa Wahitimu wa Vyuo vya Taaluma ya Wanyamapori, Pasiansi Mwanza na Mweka, Kilimanjaro**

**MHE. ENG. EZRA J. CHIWELESA** aliuliza:-

Je, nini mpango wa Serikali kuhakikisha Wahitimu wa Mafunzo ya Jeshi USU wanapata haki ya ajira sawa na Watanzania wengine?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Danstan Kitandula, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, taasisi zinazounda Jeshi la Uhifadhi Wanyamapori na Misitu hufuata utaratibu wa ajira kwa kuzingatia miongozo iliyopo katika Utumishi wa Umma, ambapo taasisi huomba kibali cha ajira kutoka Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Baada ya kupata kibali, hutolewa tangazo la ajira kupitia Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma pamoja na kuainisha vigezo vya mwombaji kwa kuzingatia Miongozo ya Utumishi wa Umma, Kanuni na Amri za Jumla za Jeshi la Uhifadhi.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia utaratibu huo wa ajira, kila Mtanzania mwenye sifa ana haki sawa ya kuomba na kupata nafasi ya kazi katika Taasisi za Jeshi la Uhifadhi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mhandisi Ezra John Chiwelesa, swali la nyongeza.

**MHE. ENG. EZRA J. CHIWELESA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali, lakini labda nitoe maelezo kidogo kabla ya kuuliza maswali. Majibu yanasema kila Mtanzania

mwenye sifa anayo haki ya kuomba, lakini ninachojua kwenye hili, Jeshi la Uhifadhi si kila Mtanzania mwenye sifa, ila ni aliyeandaliwa na familia yake mwenyewe kwa sababu, *they don't train them*, wazazi wanawaandaa halafu baada ya hapo wanabaki ku-*compete* kwa ajira. Kwa hiyo, si kila Mtanzania ni baadhi ya watu ambao wameandaliwa na wazazi wao.

Mheshimiwa Spika, sasa maswali yangu ni mawili. Swali la kwanza; ndani ya Bunge hili tuliondoa kigezo cha JKT, kwa ajili ya ajira hizi za majeshi na maeneo mengine ambayo yalikuwa yana *demand* kigezo cha JKT, lakini kwenye hili Jeshi la Uhifadhi kumekuwa na kigezo cha miaka 25. Sasa kigezo hiki una-*train* mtu kwa pesa ya mzazi mwenyewe halafu huna uwezo wa kumwajiri, huwezi kuajiri wote uliowa-*train* na hawana sehemu ya kuajiriwa kwa sababu, wao kazi yao wamejifunza kulinda wanyama na nini? Sasa inafikia *stage* hujawaajiri wote, leo unamwambia aliyevuka miaka 25 huwezi kumwajiri, ilhali tayari ameishakuwa *trained*, ni mwanajeshi yule. Kwa sababu, ame-*train*-niwa kutumia silaha na vitu vingine. Sasa je, hamuoni iko haja ya kusimamisha mafunzo yao haya kwanza, waajiri wote walio mtaani ambao wazazi wametoa pesa, wameuza viwanja wakawasomesha, ili waweze kuajiriwa wote waishe kwa sababu, waliwa-*train* wao na hamna sehemu ya kuwapeleka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili; kwa sababu, wanajiita jeshi na *experince* ya majeshi mengine kama Magereza, Polisi, Jeshi la Wananchi, Uhamiaji na mengine yamekuwa hayawa-*demand* wazazi ku-*train* watoto, ili nyie muweze kuwaajiri, yamekuwa yanachukua watoto *fresh from school*, wanawa-*train* wenyewe, wakishamaliza ku-*train* wanawaajiri wao wenyewe moja kwa moja. Je, hawaoni na wao iko haja ya kufuata mfumo ule, kuliko kutesa wazazi ku-*train* watoto ambao wanakuja kuajiriwa kwenye majeshi? Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Naomba kujibu maswali ya Mheshimiwa Chiwelesa kwa pamoja:-

Mheshimiwa Spika, kwanza nikushukuru sana wewe binafsi, tarehe 2 Septemba, uliruhusu hoja binafsi ya Mheshimiwa Ng'wasi Kamani ijadaliwe ndani ya Bunge hili. Kupitia mjadala ule, Serikali tulivuna mawazo, hekima na busara kubwa sana kutoka kwenye Bunge lako. Mawazo ambayo ndani ya Serikali kwa sasa tunayafanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niwaombe Waheshimiwa Wabunge, waiamini Serikali yao. Tuliyapokea maoni yale, tunayafanyia kazi, lakini vilevile vyuo hivi ndani ya Taasisi za Uhifadhi chini ya Wizara yetu vinahudumia Sekta pana ya Maliasili na Utalii, ambaye ni Mwajiri Mkuu kwenye Sekta hii; anaweza kuonekana kwamba, ni Serikali, lakini kwa kiasi kikubwa Sekta Binafsi inaajiri kwa kiwango kikubwa vijana wetu. Halmashauri zetu zote nchini Maafisa Wanyamapori wanatokana na vyuo hivi, kwa hiyo, kusema kwamba, ajira zinazotokana na vyuo vyetu hazipo, nadhani siyo sawa sana.

Mheshimiwa Spika, vyuo vyetu vimetoa wahitimu ambao wanaajiriwa kwenye Sekta Binafsi, Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, Taasisi za Kimataifa na ambao wamekwenda kwenye Taasisi za Kimataifa wamefanya kazi nzuri sana inayoliletea sifa Taifa letu. Nirejee kusema tunaliomba Bunge lako Tukufu na Waheshimiwa Wabunge watuamini jambo hili tunalifanyia kazi ndani ya Serikali. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Katiba na Sheria. Mheshimiwa Agnesta Lambert Kaiza, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 58

**Sheria za Kupambana na Matukio ya Ubakaji**

**MHE. AGNESTA L. KAIZA** aliuliza:-

Je, kwa kiwango gani Sheria zilizopo za kupambana na matukio ya ubakaji zinajitosheleza?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Katiba na Sheria, Mheshimiwa Pinda, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI K.n.y. WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwanza niweke sawa. Ni Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, najibu kwa niaba ya Waziri wa Katiba.

Mheshimiwa Spika, Mwaka 19...

**SPIKA:** Sasa hebu ngoja kwanza. Haya endelea Mheshimiwa.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI K.n.y. WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Mwaka 1998 Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania lilitunga sheria mahususi inayosimamia makosa ya kujamiiana na makosa yanayoendana nayo, yaani "*The Sexual Offence Special Provision Act, No. 4 of 1998*". Sheria hii ilifanya marekebisho ya Sheria ya Kanuni ya Adhabu, Sura ya 16; Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai, Sura ya 20; Sheria ya Ushahidi, Sura ya 6; Sheria ya Ukomo wa Adhabu, Sura ya 90 na Iliyokuwa Sheria ya Mtoto na Mtu mwenye Umri Mdogo, Sura ya 13.

Mheshimiwa Spika, lengo la kutungwa kwa sheria hiyo lilikuwa ni kumlinda mwanamke na mtoto dhidi ya makosa ya kujamiiana na makosa yote yanayoshabihiana. Sheria hii iliongeza adhabu ya makosa hayo kuwa ni kifungo cha maisha au kifungo kisichopungua miaka 30. Hivyo, kwa kiasi kikubwa, sheria zilizopo zinajitosheleza kupambana na matukio ya ubakaji.

**SPIKA:** Mheshimiwa Agnesta Lambert Kaiza, swali la nyongeza.

**MHE. AGNESTA L. KAIZA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na uwepo wa sheria mbalimbali ambazo amezitaja Mheshimiwa Waziri, bado vitendo vya ubakaji vimeshika kasi sana hapa nchini.

Kwa kuwa, zipo nchi ambazo zimefanikiwa katika suala zima la kupambana na vitendo hivyo ya ubakaji, mfano Nigeria wao wameenda mbali sana wamepitisha sheria ya kuwahasi wale wote ambao wanapatikana na hatia ya ubakaji. Swali la kwanza kwa Serikali; je, Serikali ipo tayari sasa kujifunza kwa nchi hizi ambazo zimefanikiwa kwa kufuata mfano wao ili mwisho wa siku tuweze kukomesha vitendo hivi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili; Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inamtambua kijana wa miaka 18 kama mtu mzima na ndiyo maana anaruhusiwa kupiga kura na kupigiwa kura, kuwa kiongozi, pia ana haki hata ya kuwa Mbunge wa Jamhuri la Muungano wa Tanzania. Ukiangalia sheria ya kupambana na masuala ya ubakaji, kijana wa miaka 18 anatambulika kama mtoto mdogo na hivyo akienda kubaka yeye adhabu yake ni kupigwa viboko. Je, Serikali haioni kwamba sheria hii imepitwa na wakati na hivyo inaleta *contradiction* kubwa sana ya Katiba Mama?

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge umeshauliza maswali mawili sasa.

**MHE. AGNESTA L. KAIZA:** …mpo tayari kupitia upya sheria hii ili mwisho wa siku tuweze kwenda sawasawa na kijana huyu wa miaka 18 sasa, ijulikane wazi kwamba ni mtoto. Kama ni mtoto sasa basi anakuwa hana hata hizi sifa nyingine ambazo nimezitaja, lakini kama atakuwa na hizo sifa, basi sheria hii ifanyiwe marekebisho ili mwisho wa siku tuweze kuwa na ustawi wa jamii ambao umekamilika? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, kwa niaba ya Waziri wa Katiba na Sheria, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI K.n.y. WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kupata nafasi ya kujibu swali hili, niende kwenye maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Spika, katika uhalisia Serikali inapotunga sheria na watungaji wa sheria wenyewe ndiyo sisi tuliopo hapa kwenye chombo hiki, kimsingi kila sheria unapoiona inakuja, inakuja kwa wakati wake na kwa uhitaji wake. Sheria katika mwenendo wake zinachakaa au zinaharibika kabisa kutokana na mfumo wa mambo mbalimbali yanayojitokeza kwenye jamii husika, hapo ndipo tunapopata nafasi ya kuzikarabati kwa maana ya kuziimarisha zikae sawa na wakati tulionao au kuanzisha sheria mpya kabisa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hii ya kuhasi ambapo nchi nyingine inatumia kwanza sipendekezi sana kuiga, ninadhani ni mfumo mzuri kutengeneza kitu ambacho kitakuwa cha kwetu badala ya kuiga kwa sababu wakati wanatunga labda walikuwa na vitu vilivyowasukuma wafanye vile.  Kwa ujumla wake tupokee ushauri wako kwamba, tupitie upya hizi sheria ambazo zimepitwa na wakati au zina mwingiliano ambao hauna tafsiri sahihi ya sheria na matukio ambayo yanaendelea kwa sasa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali la pili la umri wa miaka 18, ni kweli kwa sababu watunzi wa sheria wote tunaletewa *draft* hapa na baadaye tunaipitisha, lakini uanzishwaji wa utungaji wa sheria unategemea taasisi iliyowasilisha hoja yake hapa Bungeni. Hii vilevile, imekuwa na kasoro ndogondogo za mwingiliano bila kujali kwamba, kuna sheria nyingine ambayo imesimama upande huu ikieleza jambo ambalo linamhusu kwa mfano kijana wa miaka 18.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kipengele cha 13 utakiona kinaeleza umri wa miaka 18 kama umri sahihi wa mtu kutambuliwa kuwa mtu mzima, lakini kwenye sheria ya udhibiti wa mama na mtoto, mtoto wa miaka 18 bado anaonekana kwamba hajaingia kwenye kipindi chanya cha umri wa miaka 18 kuwa mtu mzima. Haya yote haya wakati tunapokwenda kwenye utekelezaji tunakutana na hizi changamoto ndiyo maana tunarudi tena kukaa na kuangalia namna ambavyo tunaweza tukazi-*level* zikafanana.

Mheshimiwa Spika, nimtoe wasiwasi Mheshimiwa Mbunge na Wabunge kwamba, kwa sababu ni sisi wenyewe tumebaini, basi

ipo haja na tupokee ushauri wako kwenda kuangalia pale ambapo panaleta *conflict* ya kisheria ili tuweze kunyoosha mapito ya sheria hii. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ni sheria gani hapo umeitaja ya udhibiti wa mama na mtoto?

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, kwenye kumbukumbu nimetaja tu kipengele cha Katiba Namba 13.

**SPIKA:** Aaah! Nilifikiri kuna sheria nyingine pengine inaitwa hili jina, lakini hii ya miaka 18 kwamba ni mtoto hawezi, hii tumeiweka kwenye sheria gani? Ama tusiseme mtoto, kijana wa miaka 18 anahesabika ni mtoto akibaka? Kuna uhalisia hapo? Hebu naona Mwanasheria mwingine anataka kutusaidia hapo.

Mheshimiwa Patrobass Katambi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCAL P. KATAMBI):** Mheshimiwa Spika, kwa muktadha huo ninadhani kuna mkanganyiko ambao ameufanya. Kilichofanyika, mwenye umri wa miaka 18 anatambulika ni mtu mzima kwa sheria tulizonazo, hata zile tulizobadilisha huwa tuna *Young Persons Act* pia kuna *Age of the Majority,* lakini katika msingi huo wa miaka 18 aliousema, kama angefafanua vizuri ni kwamba mwaka 1998 ilitungwa ile *Sexual Offenses Special Provisions Act,* ambayo iliingiza hata mtoto wa shule ya msingi au sekondari mwenye umri wa miaka 18 ili mradi kwamba ni mwanafunzi *with or without consent* akiwa kwenye mahusiano, kosa litatambulika kwamba ni ubakaji. Kwa hiyo, ile ndio muktadha ule wa miaka 18, lakini mpaka sasa sheria inatambua miaka 18 ni mtu mzima. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Sawa, ile siyo hii sheria uliyoitaja ni sheria inayohusu elimu ndiyo tuliibadilishia huko. Sasa, hata kule yaani kosa analokuwa amefanya ni kosa la huku kwingine, sasa mtu ana miaka 23 yupo kule unasema kwa kuwa ni mwanafunzi hawezi kubaka. Kule hatukusema mambo ya kubaka. Ninakumbuka wakati wa kutunga ile sheria, hatukuzungumzia mambo ya

amefanya kosa la jinai, ameua, amefanya nini hata kama ni mwanafunzi, lakini ana umri huo anahukumiwa kwa kosa la huku. Kosa tu linaloingia kule ni lile la kwamba, yeye kwenye ndoa na nini, yaani vitu kama hivyo, lakini haya mengine haya sikumbuki tumeweka wapi hapo mahali ambapo tunamwona mtu wa miaka 18 kwamba ni mtoto, akibaka anachapwa viboko.

Ninadhani hilo tulitazame kwa pamoja, kama hatuna hicho kifungu tukatazame vizuri kama kuna mahali kuna changamoto tuirekebishe, kwa sababu itakuwa siyo sawa.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCAL P. KATAMBI):** Mheshimiwa Spika, haipo katika sheria zetu. Juzuu zote 441 haipo.

**SPIKA:** Sawa. Kwa sababu bado tupo kwenye kipindi chetu cha maswali na majibu na hapa Mbunge anasisitiza ipo, ngoja ajaribu kutazama atakaponiletea hapa tutatoa ufafanuzi vizuri ili wote tuwe tumeelewana vizuri. Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali na wewe utazame na Mheshimiwa Naibu Waziri na wewe ukatazame, Mbunge na yeye anatazama. Nitaletewa hapa mbele tutaoa ufafanuzi vizuri.

Mheshimiwa Naibu Waziri tunakushukuru sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

**SPIKA:** Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. Wewe kwa sababu ni Mwanasheria, ukikaa huko angalia hicho Kifungu ni wapi, tueleze vizuri ili wananchi wapate huo uelewa.

Waheshimiwa Wabunge tunaenda Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. Mheshimiwa Khamis Yussuf Mussa, Mbunge wa Kwahani sasa aulize swali lake.

Na. 59

**Ukarabati Kituo cha Polisi Ng'ambo – Kwahani**

**MHE. KHAMIS YUSSUF MUSSA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itakarabati Kituo cha Polisi Ng'ambo, Kwahani kwa kuwa ni chakavu na cha muda mrefu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Daniel Baran Sillo, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Kituo cha Polisi Ng'ambo – Kwahani ni kituo cha Daraja B na jengo lake ni la siku nyingi na ni chakavu. Tathmini kwa ajili ya kufanya ukarabati imefanyika na kiasi cha fedha shilingi 109,582,820 kinahitajika. Fedha hizo zinatarajia kutengwa toka kwenye Mfuko wa Tuzo na Tozo kwa mwaka wa fedha 2025/2026, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Khamis Yussuf Mussa, swali la nyongeza.

**MHE. KHAMIS YUSSUF MUSSA:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru Serikali kwa majibu yake mazuri na yanatuletea faraja kidogo lakini kuna swali moja tu la nyongeza. Je, ni lini mchakato wa ukarabati huo utaanza? Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Ninaomba kujibu swali moja la nyongeza la Mheshimiwa Khamis Yussuf Mussa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema katika jibu la msingi kwamba katika mwaka wa fedha 2025/2026, tumetenga fedha hizo kwa ajili ya kuanza ukarabati wa hilo Jengo la Polisi Kwahani. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Asia Halamga, swali la nyongeza. Mheshimiwa ulishauliza swali la nyongeza tayari, kwa hiyo hutapewa ligine ili nisikufanye usimame kila wakati.

Mheshimiwa Asia Halamga, swali la nyongeza.

**MHE. ASIA A. HALAMGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Je, ni lini Serikali itakamilisha ujenzi wa Kituo cha Polisi katika Mkoa wa Manyara?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Asia Halamga, Mbunge wa Vijana, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli jengo la Mkoa wa Manyara la Kamanda linaendelea, lakini kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, tumetenga shilingi 800,000,000 kwa ajili ya kukamilisha jengo hilo la Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Manyara. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Zuberi Kuchauka, swali la nyongeza.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Je, Serikali wapo tayari kunirudishia fedha zangu za Mfuko wa Jimbo, ambazo nilizitoa kwa ajili ya kujenga Kituo cha Polisi Wilaya ya Liwale na hawataki kukijenga mpaka leo ni miaka mitatu? *(Makofi/Kicheko)*

**SPIKA:** Sawa. Sasa ili nijue swali lako nilielekeze kwa nani fedha za Mfuko wa Jimbo alikabidhiwa nani? Walikabidhiwa Polisi ama bado zipo kwa Mkurugenzi, lakini wewe kwenye vikao vyako uliekeza kijengwe kituo, ili nijue nani ajibu swali lako?

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Spika, fedha hizi zilitengwa kwenye bajeti ya 2020/2021, tayari zipo Polisi lakini hawaoneshi nia ya kujenga hicho kituo mpaka leo? *(Makofi)*

**SPIKA:** Hapana, zilishatoka fedha kwa Mkurugenzi zikaenda Polisi?

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Spika, zipo Polisi.

**SPIKA:** Aaah! zipo Polisi.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Spika, Polisi wamekubali kupokea na hati ninayo hapa waliyopokelea, lakini hawana nia ya kujenga hicho kituo ni mwaka wa tatu leo. Hizo fedha zirudi kwenye Mfuko wa Jimbo! *(Makofi/Kicheko)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, hela zake anataka zirejee ili akatumie kwenye maendeleo mengine, maana kituo sasa hakijengwi. *(Makofi/Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, nimpongeze Mheshimiwa Mbunge kwa kuanzisha kujenga Kituo cha Polisi japo hajamaliza, basi sisi kama Jeshi la Polisi tunamalizia kituo hicho, lakini pia nitaonana naye baadaye tuzungumze jinsi alivyotuma fedha hizo. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Conchesta Rwamlaza, swali la nyongeza.

**MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA:** Mheshimiwa Spika, wananchi wa Kijiji cha Kasharunga, Kata ya Kasharunga katika Wilaya ya Muleba walijenga Kituo chao cha Polisi kwa nguvu za wananchi. Ni kwa nini Serikali haitaki kufungua kituo hiki? Watoe sababu wananchi waelewe. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Conchesta kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ninawapongeza sana wananchi wa Kijiji cha Kasharunga kwa kujenga Kituo cha Polisi. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, baada ya Bunge hili tutaenda kufungua kituo hicho kilichojengwa ili kuhudumia wananchi wa maeneo haya. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Kassim, aha! Haya. Mheshimiwa Omar Kombo, swali la nyongeza.

**MHE. OMAR ISSA KOMBO:** Mheshimiwa Spika, je, ni lini Serikali itafanyia ukarabati Kituo cha Polisi Wilaya ya Micheweni wakati ni mara nyingi wametuahidi, lakini bado mpaka leo? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Omar Kombo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nia ya Serikali ni kukarabati vituo vyote vya Polisi ambavyo ni chakavu na kujenga vipya. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, kituo chake hicho alichokitaja kipo kwenye mpango na tayari tumefanya ukarabati ili wananchi wetu waweze kuhudumiwa kwa maana ya usalama wa raia na mali zao katika eneo lake. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Ritta Enespher Kabati, Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake.

Na. 60

**Mchango wa Serikali Kujenga Kituo cha Polisi Mdabulo – Mufindi**

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI** aliuliza:-

Je, kuna mpango gani wa kuunga mkono juhudi za wananchi wa Kata ya Mdabulo Mufindi wanaojenga Kituo cha Polisi kwa nguvu zao wenyewe?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Jeshi la Polisi imeshafanya tathmini kwa ajili ya kumalizia ujenzi wa jengo la Kituo cha Polisi

Mdabulo ili kuunga mkono nguvu za wananchi ambao umefikia kwenye hatua ya lenta na kiasi cha fedha shilingi 56,000,000 kinahitajika. Fedha hizo zinatarajiwa kutengwa toka kwenye Mfuko wa Tuzo na Tozo kwa mwaka wa fedha 2025/2026.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ritta Kabati, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Spika, nimshukuru Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake mazuri, lakini ninaomba niulize maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; ninaomba Kata ya Mapanda katika Jimbo la Mufindi Kaskazini ina changamoto kubwa sana ya Kituo cha Polisi. Je, Serikali ipo tayari sasa kutenga fedha ili wananchi wa Mapanda waweze kupata Kituo cha Polisi kizuri? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili; ninapongeza sana Serikali kwa ujenzi wa Jengo la Polisi la Makao Makuu Wilaya ya Kilolo. Je, nini sasa mpango wa kuwajengea makazi Askari Polisi wa Wilaya ya Kilolo kwa sababu wanaishi mtaani na hawana Kambi ya Polisi wanaishi maisha magumu sana. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, ninaomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Dkt. Ritta Kabati, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, moja; mkakati wa Serikali ni kuhakikisha kwamba tunajenga vituo vya polisi vya kata nchi nzima pamoja na shehia kwa upande wa Zanzibar, vituo hivi vinajengwa awamu kwa awamu. Kwa kuwa, Kata aliyoitaja ya Mapanda inahitaji Kituo cha Polisi, tutaiweka kwenye mpango ili na chenyewe kitengewe fedha kwa ajili ya kujengwa.

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili kuhusu mkakati wa makazi ya Askari Polisi. Ni kweli maeneo mengi bado kuna changamoto ya makazi ya Askari Polisi, lakini Serikali inaenda kujipanga kwenye mipango yetu ili kuhakikisha kwamba askari wetu wanakaa katika makazi bora kwa ajili ya kuendelea kulinda

raia pamoja na mali zao. Kwa hiyo, Wilaya ya Kilolo pia itakuwa ni mojawapo ya Wilaya ambayo tutaweka kwenye mpango kwa ajili ya kujengewa nyumba za makazi ya Askari Polisi. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Sophia Mwakagenda, swali la nyongeza.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Mbunge wa Jimbo la Busokelo na Mkuu wa Wilaya wamejitahidi sana kutafuta fedha za kujenga Kituo cha Polisi Busokelo; je, Serikali wataongeza nguvu lini ili waweze kumalizia kituo hicho?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, ninaomba kujibu swali moja la nyongeza la Mheshimiwa Mwakagenda, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza, nimpongeze Mheshimiwa Mkuu wa Wilaya pamoja na wananchi hawa waliojitahidi kujenga kituo hicho na tutafanya tathmini kwa fedha zilizobaki ili Serikali pia iweze kuwaunga mkono kwa kazi hiyo nzuri iliyofanywa na wananchi wa Busokelo. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Salma Rashid Kikwete, swali la nyongeza.

**MHE. SALMA R. KIKWETE:** Mheshimiwa Spika, nina swali dogo tu la nyongeza; ninaomba kujua lini Kituo cha Polisi katika Tarafa yetu ya Mchinga kitajengwa na hii ni kwa sababu hata Mheshimiwa Jumanne Sagini akiwa Naibu Waziri, alikuja akaangalia na akaona kadhia inayopatikana na hasa kwa askari wetu kuishi katika mazingira ambayo siyo rafiki. Swali langu, ni lini watatuletea fedha tujenge Kituo cha Polisi? Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, ninaomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Salma Kikwete, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli Tarafa ya Mchinga inahitaji Kituo cha Polisi na tayari Serikali imeshaahidi. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, tutatenga fedha kwa ajili ya kujenga Kituo hiki cha Polisi haraka iwezekanavyo kwa sababu wananchi hawa wa Mchinga wamesubiri kwa muda mrefu sana. Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaenda Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mheshimiwa Zacharia Paulo Issaay, Mbunge wa Mbulu Mjini, sasa aulize swali lake.

Na. 61

**Ujenzi wa Minara ya Simu Kata za Mbulu**

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY** aliuliza:-

Je, lini Serikali itaanza Ujenzi wa Minara ya Simu katika Kata za Nahasey, Gunyoda, Silaloda na Marang - Mbulu Mjini?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji kwa niaba ya Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mheshimiwa Mhandisi Kundo, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI K.n.y WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia mwezi Machi, 2024, Serikali kupitia *UCSAF,* imetekeleza miradi katika Kata Tano za Wilaya ya Mbulu Mjini, ya ujenzi wa minara ya simu, ambapo miradi ya ujenzi katika Kata hizo imekamilika na wananchi wananufaika na huduma za mawasiliano. Aidha, katika Kata ya Nahasey, Kampuni ya *Airtel* ilikamilisha ujenzi wa mnara katika Kijiji cha Banee mwezi Machi, 2024.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa Serikali kupitia Mradi wa Tanzania ya Kidijitali *(Digital Tanzania Project)* inaendelea na ujenzi wa minara katika Kata mbili za Gunyoda na Marang. Minara katika kata hizi inatarajiwa kukamilika kabla ya mwezi Mei, 2025 ambapo kukamilika kwa Kata hizi mbili kutaboresha huduma za mawasiliano ya simu katika Vijiji vya Banee, Hassama, Haysali, Nahasey, Gedamar, Gunyoda, Silaloda, Aicho na Gwandumehi na hivyo kuifanya Kata ya Silaloda kuwa na mawasiliano.

**SPIKA:** Mheshimiwa Zacharia Paulo Issaay, swali la nyongeza.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali na kwamba tayari imeshafanya kazi kubwa sana ya kuweka minara katika Jimbo la Mbulu Mjini, Kata ya Gunyoda na Silaloda zina jiografia ya milima. Minara hii itakayojengwa katika Kata ya Gunyoda na Kata ya Marang haitaweza kuhudumia Kata ya Gunyoda. Swali la kwanza; je, Serikali haioni kuwa kuna umuhimu mkubwa wa kujenga mnara katika Kata ya Silaloda kwa ajili ya jiografia ya milima? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili; kwa kuwa tumekuwa na minara mingi sana katika maeneo yetu. Je, Serikali haioni utashi wa kukaa meza moja na Makampuni ya Simu ili kuunganisha minara na kuweza kutoa huduma kwa pamoja ili kuleta ufanisi zaidi katika mawasiliano? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI K.n.y WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, ninapenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Zacharia kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa kwamba kata hii na kwa jiografia yake, ina milima sana kiasi kwamba *line of sight* inajikuta kwamba haiwezi kuhudumia katika maeneo ambayo yako mabondeni na hivyo changamoto bado inaendelea kuwepo.

Mheshimiwa Spika, Serikali itatuma wataalam wake kwenda kufanya kazi ya kiufundi na kufanya tathmini. Tuchukue hatua ipi

ambayo itaendana na aina ya tatizo ambalo litakuwa limeonekana pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo la pili ni kuangalia namna ambavyo mitandao inaweza ikaunganishwa. Kwanza kabisa Serikali kupitia Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari tulikwishatengeneza kanuni. Kwanza ni Kanuni ya *Roaming*. Maana yake ni kwamba, mtoa huduma mmoja anaweza akatumia huduma ya mtoa huduma mwingine. Pili, ni *infrastructure sharing*, hii ni pamoja na hayo mambo ya *co-location*; maana yake ni kwamba *Vodacom, Airtel*, *Tigo*, wanaweza wakapatikana kwenye mnara mmoja ili kuhakikisha kwamba tunapunguza gharama za uwekezaji, lakini huduma iendelee kupatikana.

Mheshimiwa Spika, tumekwenda zaidi ya hapo, tumekwenda kwenye eneo la *spectrum* (masafa). Napo tumetengeneza kanuni ya kuruhusu sasa, kwamba tunaweza tukawa na *spectrum sharing* ili kuhakikisha kwamba tunaendelea kupunguza gharama za uwekezaji na za uendeshaji, wakati huo huo huduma iendelee kuboreshwa na wananchi waendelee kupata huduma ya mawasiliano. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Deo Mwanyika, swali la nyongeza.

**MHE. DEODATUS P. MWANYIKA:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru sana. Katika Kijiji cha Uliwa Kata ya Uliwa kumekuwa na ahadi ya muda mrefu sana kuhusu huo mnara na hata na yeye alipokuwa Naibu Waziri aliahidi. Je, ni lini sasa mnara huo ambao umeahidiwa utajengwa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI K.n.y WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, ninapenda kujibu swali, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mradi wetu wa Tanzania ya Kidijitali wenye minara 758, minara takribani 295 ambayo ni sawasawa na

40% imekwishakamilika, lakini kuna minara mingine ambayo inaendelea katika hatua mbalimbali za utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, katika utekelezaji huo tumekutana na changamoto mbalimbali kiasi kwamba tumejikuta tunahama katika eneo moja kwenda kutafuta eneo lingine. Vilevile tumekutana na migogoro katika maeneo ambayo minara inataka kujengwa. Hii yote imesababisha ucheleweshaji wa maeneo mbalimbali kupata huduma.

Mheshimiwa Spika, kingine ambacho Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari inakifanya, Mheshimiwa Waziri Jerry Silaa ameandaa kitabu chenye taarifa ya utekelezaji wa minara 758, ambapo kila mnara unakojengwa namba ya mtoa huduma ambaye atakuwa anatoa taarifa ya *progress* ya utekelezaji kila eneo. Katika taarifa hizo kuna namba za Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote *(UCSAF)* ambao watakuwa wanaweza kutoa *update* ya hatua ambazo zinaendelea katika eneo husika. Kwa hiyo, ninaamini kabisa kwamba eneo la Mheshimiwa Mwanyika liko katika ile miradi ambayo iko katika hatua mbalimbali. Ninaamini kabisa kwamba, mpaka Mei, 2025 yote itakuwa imekamilika kama ambavyo Serikali imeelekeza. Ahsante sana.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, pamoja na maelezo hayo, ninaona bado mmesimama kuhusu minara. Sasa, ninataka kujua; nyie mmeshasoma kile kitabu na bado mmeona kuna changamoto ama? Ama kati yenu kuna ambaye hajasoma kile kitabu ambacho kimetolewa na taarifa zinazohusu minara?

Wote mmesoma na bado mmeona mna maswali baada ya kuona hicho? Sasa jamani, huyu Mheshimiwa Naibu Waziri pamoja na kwamba anayajua mambo ya minara, lakini amejibu swali kwa niaba. Yeye sasa hivi ni Naibu Waziri wa Maji. Sasa, mkisimama wengi kidogo inakuwa mtihani. *(Makofi)*

Ninampa nafasi Mheshimiwa Edwin Enosy Swalle, atapata pia Mheshimiwa Sylivia Sigula. Wengine mmeshawahi kupata nafasi ya kuuliza, kwa hiyo mketi.

**MHE. EDWARD O. KISAU:** Mheshimiwa Spika, mimi sijapata.

**SPIKA:** Wewe hujapata eeh?

**MHE. EDWARD O. KISAU:** Ndiyo.

**SPIKA:** Haya basi na wewe utapata nafasi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Edwin Enosy Swalle, swali la nyongeza kwa kifupi.

**MHE. EDWIN E. SWALLE:** Mheshimiwa Spika, Kata ya Ikondo Jimbo la Lupembe ina changamoto kubwa ya mawasiliano, hasa maeneo ya Nyave, Idyadya, Itova na kadhalika. Je, ni lini mnara wa simu utajengwa Ikondo kwa ajili ya wananchi wangu? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI K.n.y WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa *Advocate* Edwin Swalle, Mbunge wa Lupembe kwa kazi kubwa na kwa namna ambavyo amepambania kuhusu hii Kata ya Ikondo. Ninaikumbuka vizuri sana. Kwa bahati nzuri na salamu njema kwake, leo nimepatiwa taarifa na Mheshimiwa Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari; katika maeneo ambayo nilikuwa ninajua kabisa kwamba yalikuwa na changamoto ya muda mrefu, Kata ya Ikondo, wakandarasi wameshafika *site* na wako tayari kwa kuanza kujenga mnara wa mawasiliano katika eneo hilo. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Sylivia Sigula, swali la nyongeza kwa kifupi.

**MHE. SYLVIA F. SIGULA:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru. Ukiwa Sitalike kama unaelekea Namanyere, unapita Hifadhi ya Taifa ya Katavi, umbali wa zaidi ya kilometa 70 hakuna mawasiliano kabisa. Je, Serikali ina mpango gani, ukizingatia pale kuna wanyama wakali?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI K.n.y WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, moja ya changamoto ambazo nimeongelea wakati wa kucheleweshwa kwa baadhi ya maeneo ya kujengwa minara nimeongelea migogoro; lakini kuna maeneo mengine tunapata changamoto ya kupata vibali. Kwa eneo lile tumepata changamoto ya kupata vibali kwa wakati kutoka *TSF*.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tunaamini kabisa kwamba tunaendelea kuwa-*engage* wenzetu na watakapoweza kutoa kibali hicho tuna uhakika kabisa kwamba tutakwenda kujenga minara katika maeneo hayo, ili kuhakikisha kwamba tunaondoa hatari ambayo inaweza ikatokana na wanyama wakali ambao Mheshimiwa Mbunge ametaja. Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimwia Edward Olelekaita, swali la nyongeza.

**MHE. EDWARD O. KISAU:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa nafasi. Kiteto tangu tupate uhuru hatusikilizi *Redio Tanzania*, na kauli ya mwisho walisema kwamba wangejenga mnara mwezi wa pili mwaka huu. Sasa, nini kauli ya mwisho kabisa kwa wananchi wa Kiteto?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI K.n.y WAZIRI WA HABARI, MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Spika, ninapenda kujibu kama ambavyo Mheshimiwa *Advocate* Olelekaita, Mbunge wa Kiteto alivyouliza.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa nimekwishafika Kiteto, na Mheshimiwa Mbunge tulizunguka katika jimbo lake takriban siku nzima ili nilijione changamoto. Tulifanya mkutano wa hadhara, wananchi waliongelea kuhusu changamoto hii. Ninamhakikishia kwamba, jambo hili ambalo ni ahadi ya Serikali kwa Watanzania, hasa wananchi wa jimbo lake, ahadi ya Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan itatekelezwa na itatimia. Nimwombe, atupatie muda kidogo ili tuendelee kufanyia kazi baadhi ya

changamoto ambazo zinaendelea kutokana na mambo ya kiufundi. Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, tunakushukuru sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Pamoja na shukrani hizo kuna ujumbe nimeletewa hapa. Kuna maeneo ambayo minara imejengwa na bado mitandao haipatikani. Kwa hiyo, hata kule ambako imejengwa kuna maeneo ambayo bado kuna changamoto ya mawasiliano. Kwa hivyo, ni muhimu kuendelea kufuatilia. Utamfikishia Mheshimiwa Waziri salamu hizo. Ahsante sana.

Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo, Mheshimiwa Tauhida Cassian Gallos, Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake.

Na. 62

**Wasanii Kufanya Kazi Pasipo Kuvunja Sheria na Maadili**

**MHE. TAUHIDA CASSIAN GALLOS** aliuliza:-

Je, kuna mpango gani kuhakikisha wasanii wanafanya kazi zao kwa uhuru pasipo kuvunja sheria, kanuni na maadili ya Kitanzania?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Mheshimiwa Hamis Mwinjuma, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Wizara yetu kupitia Baraza la Sanaa la Taifa iliandaa Mwongozo wa Uzingatiaji wa Maadili katika Uzalishaji wa Kazi za Sanaa, ambao ulizinduliwa rasmi tarehe 3 Novemba, 2023. Kwa sasa tunaendelea na maboresho ya Kanuni za BASATA za Mwaka 2018 na pia mwongozo wa uendeshaji matukio ya sanaa ili kuweka misingi thabiti ya usimamizi wa matukio hayo.

Mheshimiwa Spika, lengo kuu la maboresho haya ni kulinda maadili katika uzalishaji wa kazi za sanaa na kuwafanya wasanii wajitathmini wenyewe kabla hawajazalisha na kuzitoa kazi hizo kwa walaji. Aidha, BASATA inaendelea kutoa elimu kwa waandaaji wa kazi za sanaa kuzingatia miongozo iliyotolewa kabla ya kuzalisha kazi yoyote iwe ya sauti (muziki) ama ya kutengeneza maudhui mtandaoni.

Mheshimiwa Spika, ninapenda kuliahidi Bunge lako Tukufu kuwa, BASATA inaendelea kuwaelimisha wasanii ili kuwajengea uelewa wa kulinda maadili ya Mtanzania katika uzalishaji wa kazi zao.

**SPIKA:** Mheshiimiwa Tauhida Cassian Gallos, swali la nyongeza.

**MHE. TAUHIDA CASSIAN GALLOS:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali moja la nyongeza. Ninamshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri ambayo yanaendelea kutia matumaini ndani ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, pamekuwepo na baadhi ya wasanii ambao wanawakilisha ndani ya mataifa mengine ya nje, lakini wasanii hao ni wazuri, hawana *scandal* ya aina yoyote. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri anaonaje kwa wakati huu achukue fursa ya kuwezesha wasanii hawa kupatiwa hata *Passport* za kihuduma ambazo zitawafanya wao waendelee kuitunza sana aa kuiwakilisha vizuri Tanzania?

**SPIKA:** Mheshimliwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Serikali inatambua umuhimu wa wasanii katika kuitangaza nchi yetu, lakini pia katika kuchangia uchumi wetu. Ninakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba, upo umuhimu wa kuendelea kuwarahisisishia wakati wanavyofanya safari za kwenda kufanya kazi zao nje ya mipaka ya Tanzania ambako wanakwenda kuitangaza nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, nchini mamlaka ambayo ina jukumu la kutoa *Passport* na hati nyingine za kusafiria ni Idara ya Uhamiaji ambayo iko chini ya Wizara ya Mambo ya Nchi. Kwa mujibu wa Sheria ya *Passport* na Hati Nyingine za Kusafiria ya Mwaka 2002, wasanii si miongoni mwa wanufaika wa Hati za Kidiplomasia ama Hati za Kihuduma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninamhaidi Mheshimiwa Mbunge, swali lake hili ambalo limekuja kama maoni na ushauri, tutakaa na wenzetu wa Wizara ya Mambo ya Ndani kuona namna ambavyo tunaweza kuendelea kuwarahisishia wasanii wetu wanaofanya kazi kubwa ya kuitangaza nchi yetu nje ya mipaka yetu namna ya kusafiri ili waendelee kuifanya kazi hiyo kwa moyo mmoja. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Maendeleo ya Jamii Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Mheshimiwa Abeid Ighondo Ramadhani, Mbunge wa Singida Kaskazini sasa aulize swali lake. *(Makofi)*

Na. 63

**Hatua kwa Watu Wanaojihusisha na Mapenzi ya Jinsia Moja**

**MHE. ABEID R. IGHONDO** aliuliza:-

Je, kuna mpango gani wa kuwakamata na kuwachukulia hatua watu wanaojihusisha na mapenzi ya jinsia moja?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Mheshimiwa Mwanaidi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM** aljibu:-

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 154 cha Sheria ya Kanuni ya Adhabu, Sura Na. 16 ya Sheria za Tanzania kinatamka bayana

kuwa, vitendo vya mapenzi ya jinsia moja au mahusiano kinyume na maumbile, iwe faragha au kwa makubaliano ni kosa la jinai. Aidha, Kifungu cha 155 cha sheria hiyo, kinaweka adhabu kwa kosa la kujaribu kufanya vitendo vinavyokatazwa chini ya Kifungu cha 154. Hivyo, tutaendelea kushirikiana na Jeshi la Polisi na Mahakama katika kusimamia utekelezaji wa Kifungu cha 154 na 55 cha Sheria ya Kanuni za Adhabu Sura ya 16. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Abeid Ighondo Ramadhani, swali la nyongeza.

**MHE. ABEID R. IGHONDO:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru. Pamoja na majibu hayo nina maswali mawili madogo ya nyongeza. Swali la kwanza; ninapenda kujua kwa kipindi hiki cha miaka miwili, mwaka 2023 na huu mwaka 2024, ni watu wangapi ambao wametiwa hatiani kwa makosa hayo?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; ninapenda kujua mikakati madhubuti ya Serikali katika kuhakikisha tunakomesha au inakomesha matendo hayo kwenye jamii, kwa sababu bado tunaona pamoja na sheria zilizopo, lakini kule *field* bado matukio hayo ni mengi, sasa walete sheria, walete Muswada hapa Bungeni tutunge sheria kuiongezea meno sheria iliyopo kukomesha matendo hayo.

**SPIKA:** Haya, ahsante sana. Mheshimiwa, swali lako la kwanza linahusu takwimu, kwamba wangapi wametiwa hatiani. Mheshimiwa Naibu Waziri, kama unazo takwimu unaweza kumpa, lakini kama huna kanuni zinakuruhusu kumpatia baadaye Mheshimiwa Mbunge.

Swali la pili liko dhahiri, unaweza kuendelea kujibu. Aidha, yote mawili ama la pili; la kwanza utampa takwimu Mheshimiwa Mbunge kama huna. Kama unazo, endelea na majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Ninapenda kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, swali lake la kwanza linahusu takwimu. Kwa swali hili ninaomba tukutane ili nimtafutie takwimu, ili tuone ni matukio mangapi yametokea katika mahusiano ya jinsia moja ili tuweze kujua na kuukomesha ukatili huu wa kijinsia.

Mheshimiwa Spika, kwa swali lake la pili, sisi sote tunafahamu masuala haya ya mmomonyoko wa maadili kwamba yanakera sana kwa jamii. Tunapaswa kujua kuwa Serikali ya Awamu ya Sita ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan iko makini kwa usimamizi wa utekelezaji wa sheria, kanuni na miongozo iliyowekwa ili kuweka heshima na kuwa sehemu ya kuimarisha misingi ya utawala bora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tutaendelea kuimarisha kutoa elimu kwa jamii ili kukomesha vitendo hivi vya kikatili na mapenzi ya jinsia moja kwa kuhakikisha kwanza mila na desturi za Mtanzania zinaimarishwa. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Kilimo, Mheshimiwa Asha Abdullah Juma, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

**MHE. ASHA ABDULLAH JUMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante, ninaomba swali langu Na. 64 lipatiwe majibu ya ...

**SPIKA:** Washa kisemeo Mheshimiwa, washa kisemeo.

**MHE. ASHA ABDULLAH JUMA:** Mheshimiwa Spika, hujanisikia? Ahsante, ninaomba...

**SPIKA:** Mimi nimekusikia, lakini Taarifa Rasmi za Bunge hazijakusikia.

**MHE. ASHA ABDULLAH JUMA:** Mheshimiwa Spika, hewala, ahsante.

Na. 64

**Ujenzi wa Mabwawa Nchini**

**MHE. ASHA ABDULLAH JUMA** aliuliza:-

Je, Serikali imejenga mabwawa makubwa mangapi nchini?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Daivd Ernest Silinde, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Serikali inaendelea na ujenzi wa mabwawa makubwa 18 ya umwagiliaji yenye jumla ya mita za ujazo milioni 321.89 katika Mikoa ya Dodoma, Tabora, Singida, Mwanza, Simiyu, Shinyanga, Geita, Mtwara, Lindi, Arusha, Tanga, Kigoma, na Manyara.

Mheshimiwa Spika, kati ya mabwawa hayo, ujenzi wa Bwawa la Tlawi Mkoani Manyara lenye mita za ujazo milioni 1.1, na ukarabati wa Bwawa la Ulyanyama, Tabora lenye mita za ujazo milioni 2.07 umekamilika. Aidha, ujenzi wa mabwawa 16 upo katika hatua mbalimbali za utekelezaji.

**SPIKA:** Mheshimiwa Asha Abdullah Juma, swali la nyongeza.

**MHE. ASHA ABDULLAH JUMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Ninashukuru sana kwa majibu ya kina kutoka kwa Mheshimiwa Waziri, lakini nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza; tumeshuhudia mvua kubwa hivi karibuni na siku za nyuma na upotevu wa maji mengi ya mvua ambayo ni muhimu kwa kilimo. Je, Serikali ina mpango gani wa kuainisha maeneo yale ambayo maji yanaendelea kupotea na kujenga mabwawa ya wastani na madogo madogo kwa ajili ya kilimo ambacho ndiyo uti wa mgongo wa nchi yetu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili; mara kadhaa tumeshuhudia mafuriko katika maeneo ya Rufiji, ambayo yameharibu kilimo makazi, miundombinu hata maisha ya watu. Je, ni lini Serikali itafanya utafiti mahsusi wa kujua ni aina gani ya mabwawa yajengwe kwenye maeneo hayo ili kugema haya maji kwa maendeleo ya kilimo nchini?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Nimthibitishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali tuna mpango madhubuti; ambapo tulishapata maelekezo kutoka kwa Mheshimiwa Rais; wa kujenga mabwawa makubwa 100 nchi nzima. Mpango huo ambao tunao katika hatua ya sasa tumewakabidhi washauri waelekezi kwa ajili ya kuandaa usanifu wa maeneo hayo yote.

Mheshimiwa Spika, kazi hii itafanyika ndani ya kipindi cha miezi sita na baada ya hapo tutakuwa na taarifa kamili na tutaanza sasa kujua tunatafuta pesa wapi na kuanza kutangaza *tender* ili tupate wakandarasi. Kwa hiyo, hatua hiyo ipo kwa sasa hivi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu Bonde la Mto Rufiji ambako kumekuwa na mafuriko makubwa na yenyewe ni kwamba msanifu mkubwa kampuni ya SABA ipo kule *site* sasa hivi. Wakishamaliza maana yake tutatangaza *tender* haraka kwa sababu haya yalikuwa ni maelekezo ya Mheshimiwa Rais wakati ule mafuriko yametokea. Kwa hiyo *tender* hizi zitafanyika katika mwaka huu wa fedha, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa, aah! Kuna Mbunge hajauliza swali kabisa. Mheshimiwa Agnes Hokororo, swali la nyongeza.

**MHE. AGNES E. HOKORORO:** Mheshimiwa Spika, je, katika hayo mabwawa 100, upo uwezekano wa kujenga bwawa moja kubwa kutokana na Bonde la Mto Lukuledi ambalo pia limekuwa likisababisha madhara katika Mkoa wa Lindi na Mtwara? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, ni kwamba Bonde la Mto Lukuledi ni miongoni mwa maeneo ambayo yapo katika mpango. Hayo mabwawa 100 ni mabwawa yote nchini katika maeneo yote nchi nzima, yaani hakuna mkoa ambao tumeuacha katika maelekezo haya ambayo tunakwenda kuyatekeleza. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Maji, Mheshimiwa Jonas William Mbunda, Mbunge wa Mbinga Mjini, sasa aulize swali lake.

Na. 65

**Kukamilisha Miradi ya Maji Halmashauri ya Mji wa Mbinga**

**MHE. JONAS W. MBUNDA** aliuliza:-

Je, kuna mkakati gani wa kuhakikisha miradi ya maji inakamilika kwa wakati katika Halmashauri ya Mji wa Mbinga?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, Mhandisi Kundo, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea na utekelezaji wa Miradi ya Maji katika Halmashauri ya Mji wa Mbinga ambapo katika mwaka wa fedha 2023/2024 imekamilisha miradi saba kati ya miradi tisa iliyokuwa imepangwa kutekelezwa kwa kipindi hicho. Pia katika mwaka wa fedha 2024/2025, jumla ya miradi minne imepangwa na inaendelea kutekelezwa na ipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji. Mkakati mahususi wa Serikali ni kuhakikisha inapeleka fedha zinazohitajika kwa wakati sambamba na kusimamia kwa karibu utekelezaji wa Miradi ya Maji kote nchini ikiwemo Wilaya ya Mbinga ili miradi hiyo iweze

kukamilika kwa wakati na kuanza kutoa huduma iliyokusudiwa kwa Watanzania.

**SPIKA:** Mheshimiwa Jonas William Mbunda, swali la nyongeza.

**MHE. JONAS W. MBUNDA:** Mheshimiwa Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa majibu mazuri ya Serikali. Pia, nichukue nafasi hii kuipongeza sana Serikali kwa kutekeleza miradi hiyo ya maji katika Jimbo la Mbinga Mjini, lakini nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; Serikali imejenga miradi katika Kijiji cha Mbagamao, Kijiji cha Tanga na Kijiji cha Ruvuma chini ambayo ni miradi mikubwa. Nilikuwa nataka nijue sasa ni lini Serikali itapeleka fedha kwa ajili ya kusambaza maji kwenye vitongoji ambavyo vipo jirani na miradi hiyo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili; Kata ya Kikolo, Kijiji cha Kikolo pamoja na Kitongoji cha Kitete kuna changamoto kubwa sana ya upatikanaji wa maji. Je, ni lini Serikali itapeleka fedha kwa ajili ya kujenga mradi katika eneo hilo? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa katika maeneo haya Mbagamao, Mheshimiwa Mbunge amekuwa akituomba sana Serikali kwenda kuhakikisha kwamba tunaendelea kupanua na kusambaza mtandao wa maji katika vijiji alivyovitaja. Serikali inatafuta fedha na kuhakikisha kwamba tutaenda kufanya upanuzi huo katika vijiji na vitongoji ambavyo Mheshimiwa Mbunge ameviomba.

Mheshimiwa Spika, upande wa Kijiji cha Kikolo tayari tumekamilisha usanifu na tutaingiza katika bajeti yetu ya 2025/2026, kuhakikisha kwamba eneo hilo linaenda kupata huduma ya maji safi na salama. Kwa eneo la Kitete, bado Serikali kupitia Wizara ya Maji, tunaendelea kutafuta chanzo. Tutakapokipata chanzo, ndipo tutaanza usanifu wa mradi ili tujue

kwamba itahitaji gharama ya shilingi ngapi kwenda kuutekeleza mradi huo. Baada ya hapo, Serikali itachukua hatua stahiki kwa wakati sahihi. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge nimewaona, lakini muda wetu umekwenda sana. Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Wizara ya Ujenzi, Mheshimiwa Kavejuru Eliadory Felix, Mbunge wa Buhigwe, sasa aulize swali lake.

Na. 66

**Barabara ya Kuunganisha Wilaya ya Kigoma na Buhigwe**

**MHE. KAVEJURU E. FELIX** aliuliza:-

Je, lini barabara inayounganisha Wilaya ya Kigoma Vijijini na Buhigwe itajengwa kwa kiwango cha lami kuanzia Mahembe, Kinazi hadi Buhigwe?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Mhandisi Godfrey Kasekenya Msongwe, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa barabara ya kuunganisha Wilaya ya Kigoma na Buhigwe unatekelezwa kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha. Kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara hii kuanzia Kalela, Munzeze, Janda hadi Buhigwe imekamilika. Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara hiyo. Aidha, Serikali itaendelea kuifanyia matengenezo barabara hii ili iendelee kupitika majira yote ya mwaka, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kavejuru Eliadory Felix, swali la nyongeza.

**MHE. KAVEJURU E. FELIX:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali nina maswali mawili ya nyongeza. Serikali ina mikakati gani ya kujenga kwa kiwango cha lami Barabara ya

Buhigwe, Muyama, Kitanga hadi Kumsenga ambayo ni barabara ya ulinzi na itaunganisha wilaya tatu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili; lini ujenzi wa barabara ya kiwango cha lami kilometa 260 kuanzia Kabingo, Kibondo, Malagarasi, Kasulu hadi Manyovu utakamilika? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Barabara ya Buhigwe, Muyama, Kitanga hadi Kumsenga hadi Mabamba ambayo inaenda Gitega, kama alivyoisema tayari tumeshafanyia usanifu. Kupita Mto Malagarasi, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, kwamba sasa hivi tunajenga daraja, tunajenga zile nguzo na daraja lililokuwa linatumika pale Malagarasi chini kati ya Mvugwe na Kibondo ndio litahamia pale. Kwa hiyo mkandarasi yupo *site* kuunganisha hiyo barabara na tumeshaifanyia usanifu barabara hiyo ya ulinzi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu barabara ya kilometa 260, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, Wanabuhigwe na Wanakigoma na Watanzania wote kwamba Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, anaandika historia. Sasa tuna kilometa saba tu ambazo zimebaki kuanzia Manyovu, Kasulu, Kibondo, Kakonko hadi Mwanza bado kilometa saba ambazo ni za vumbi. Mwezi wa tatu hiyo barabara itakuwa imekamilika yote kwa kiwango cha lami.  Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge narejea tena, wote nimewaona, lakini bahati mbaya muda wetu umekwenda sana.

Wizara ya Uchukuzi, Mheshimiwa Mhandisi Stella Martin Manyanya, Mbunge wa Nyasa, sasa aulize swali lake.

Na. 67

**Ujenzi wa Bandari ya Mbambabay**

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA** aliuliza:-

Je, lini Bandari mpya ya Mbambabay itaanza kujengwa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi kwa niaba ya Wizara ya Uchukuzi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI K.n.y WAZIRI WA UCHUKUZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia *TPA* (Mamlaka ya Bandari ya Tanzania) imeanza utekelezaji wa ujenzi wa bandari mpya ya Mbamba Bay ambapo mkataba wa utekelezaji wa mradi huu ulisainiwa tarehe 4/12/2023 na mkandarasi alianza kazi mnamo tarehe 27 Januari, 2024 ambapo hadi kufikia sasa hivi mradi umefika asilimia nane ya utekelezaji na mradi uliwekwa jiwe la msingi tarehe 25 Septemba, 2024 na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, muda wa utekelezaji wa mradi huu ni miezi 24 na gharama ya mradi huu ni shilingi bilioni 75.853 ambapo kazi mbalimbali zinazotarajiwa kufanyika zikiwemo; ujenzi wa gati na jengo la abiria, ujenzi wa majengo ya kuhifadhia mizigo pamoja na ujenzi wa barabara ya kuingia eneo hilo la bandari zitafanyika. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mhandisi Stella Martin Manyanya, swali la nyongeza.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwanza kwa dhati ya moyo wangu na kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Nyasa, naomba nitoe shukrani nyingi sana kwa Mheshimiwa Rais pamoja na Wizara ya Uchukuzi kwa ujumla kwa kazi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nina maswali mawili madogo ya nyongeza. Moja; kwa kuwa katika mradi huu tuliomba pia

tujengewe mnara wa alama ya Mji wa Mbamba Bay ambao utakuwa unautambulisha mji wetu pamoja na wilaya kwa ujumla. Je, ni hatua gani imefikiwa katika kufanya kazi hiyo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la pili; kwa sasa tumeshuhudia kwamba vifaa vingi vimeshushwa kupelekwa Mbambabay kwa ajili ya kuanza ujenzi wa bandari hii. Swali langu ni kwamba, ni namna gani vijana pamoja na wananchi wa Mbambabay kwa ujumla watafanikisha katika kupata ajira zitakazotokana na kuendeleza mradi huu?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI K.n.y WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba nijibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli hili lilikuwa ni ombi la wananchi wa Nyasa kupitia Mbunge wao Mheshimiwa Stella Manyanya, kuhusu kujengewa Mnara ambao utatambulisha Mji wa Nyasa. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba maelekezo yalishatolewa kwa Mtendaji Mkuu wa Bandari, kwamba mkandarasi ambaye anajenga bandari ahakikishe kwamba anajenga mnara huo ikiwa ni sehemu ya *CSR* kwa wananchi wa Nyasa pamoja na *CSR* sehemu zingine ambazo atafanya.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ajira tumekuwa na utaratibu pale ambapo miradi inatekelezwa maeneo yoyote na kazi ambazo hazihitaji ujuzi maalum basi kipaumbele kiwe kwa wananchi ambao mradi huo unatekelezwa. Nichukue nafasi hii kumwelekeza Meneja wa Bandari ahakikishe kwamba wananchi wa Nyasa na hasa vijana wanapewa kipaumbele kwa ajira ambazo hazihitaji ujuzi maalum. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge kabla hatujahitimisha kipindi chetu cha maswali kutoka kwenu na majibu upande wa Serikali kulikuwa na hoja wakati wa swali la Mheshimiwa Agnesta Lambert

Kaiza na nilisema tutafute ufafanuzi ili kama hiyo changamoto ipo basi iweze kufanyiwa kazi. Sijajua ni yupi sasa ambaye ametazama.

Mwanasheria Mkuu wa Serikali, karibu.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa naomba nichukue nafasi hii kukupongeza kwa hotuba yako nzuri ambayo uliitoa katika Umoja wa Mabunge Duniani. Ni hotuba ambayo ilikuwa imejaa weledi, ukomavu na msimamo. Kwa hakika hotuba yako ile imetuheshimisha kama Taifa na imemheshimisha Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, sasa niende kwenye hoja kutoka kwa Mheshimiwa Kaiza. Kwanza kabisa nimshukuru kwa hoja yake nzuri na alichokisema ni kweli ukiangalia kanuni zetu za adhabu *(Penal Code)* kifungu cha 131 kimeweka adhabu kwa mtu ambaye anafanya makosa ya ubakaji, kifungo cha maisha au kisichopungua miaka 30. Pia, kikaendelea na kuweka adhabu zingine pamoja nazo kwa maana ya *corporal punishment*, faini pamoja na fidia.

Mheshimiwa Spika, pia, kikaweka 131(2) kama angalizo sasa kwamba kama makosa haya yametendwa na mvulana ambaye ana umri chini ya miaka 18 kwenda chini, basi kama ni mara yake ya kwanza atapata adhabu ya viboko na kama ni mara ya pili imeendelea pale na kadhalika. Sasa imekinzana na Sheria yetu ya Mtoto kupitia kifungu kile cha nne ambacho kimetafsiri vizuri kwamba mtoto ni yule ambaye yupo chini ya miaka 18.

Mheshimiwa Spika, kwa hivyo, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, inalichukua hili na kwenda kuliangalia, lakini tutatanguliza utafiti kidogo. Kwa sababu wakati mwingine inawezekana sio tu umri, inawezekana wakati ule tunaandika tulikuwa na taarifa tulizokuwa nazo. Kwa hiyo sasa hivi ndio mwendo tutakuwa tunakwenda nao kwamba kila Miswada ya Sheria itakayokuwa inaletwa lazima iwe imetanguliwa na utafiti wa kina kwa sababu utafiti ndio utakupelekea sasa uweze kuandika sheria ambayo ni nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo tutafanya utafiti kidogo kwa nini tulikuja na hii *exemption* kwa mtoto wa miaka 18 asifungwe kwa mfano kifungo cha maisha. Nilijaribu kuangalia kwenye *murder* haipo *exemption*. Kwa hiyo nadhani ni hoja nzuri na niseme kwamba tumeipokea. Tutafanya utafiti kidogo na baada ya hapo *probably* tunaweza kufanya *harmonization*. Kama tutakuwa hatufanyi *harmonization* utafiti utakuwa umetupa majibu yaliyo sahihi.

Mheshimiwa Spika, kwa heshima na taadhima naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nafikiri kwa maelezo aliyotoa Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, sote tumuachie hii kazi ili wakaifanyie utafiti kwa sababu wenzetu waliyoiandika kwa sura hii watakuwa walikuwa na sababu. Sasa zikajulikane hizo sababu kama sasa zimebadilika ama kuna sababu ya pengine kurekebisha hapa na pale basi tufanye hivyo.

Ninakumbuka hapa Bungeni ilishawahi kuja hoja kutokea Iringa ninafikiri, ililetwa na Mheshimiwa Rose Tweve. Kulitokea changamoto kidogo huko kwa ajili ya kifungu hiki, kwa sababu mtu alikuwa kama wiki mbili ama miezi miwili ndio amekuwa na miaka 18 halafu akabaka mtoto huko ikawa shughuli inabidi aadhibiwe kama mtu mzima ama kifungu hiki anakuwa nacho.

Sasa ukisema miaka 18 au pungufu unamaanisha 18 akiwa na miezi mingapi ndani ya miaka 18 au hata yule anayekaribia 19 yaani anakaribia 19 ndani ya siku mbili tatu akifanya leo; je, bado ana yupo chini ya hiki kifungu au hapana? Hata hivyo, Mwanasheria Mkuu wa Serikali, ametoa maelezo mazuri yanayojitosheleza. Tuwape fursa wakafanye utafiti ili tuendelee na ulinzi wetu wenyewe lakini pia ulinzi wa watoto wetu, ulinzi wa akinamama, ulinzi wa wakinadada kila mtu awe amelindwa na sheria hii kwa sababu ndio kusudio lake.

Waheshimiwa Wabunge, tunayo matangazo na tangazo la kwanza ni la wageni. Tutaanza na wageni waliokaa Jukwaa la Spika.

Kwanza wapo wageni wanne wa Mheshimiwa Profesa Kitila Alexander Mkumbo ambaye ni Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji. Hawa ni viongozi wa Tume ya Mipango kutoka Wizara ya Mipango na Uwekezaji, lakini pia wapo viongozi waandamizi wa kutoka ofisi hii; yupo Dkt. Tausi Mbaga Kida, ambaye ni Katibu Mkuu Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji; Dkt. Mursal Milanzi, Kaimu Katibu Mtendaji Tume ya Mipango; Dkt. Lorah Madete, Naibu Katibu Mtendaji Tume ya Mipango; na Bi. Angela Shayo, ambaye ni Kaimu Mkurugenzi Mipango Taifa, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni wenu Waheshimiwa Wabunge. Kwanza ni wageni watatu wa Mheshimiwa Zuberi Mohamedi Kuchauka, ambao ni viongozi wa *Agricultural Marketing Cooperative Society (AMCOS)* na Mtumishi wa Halmashauri ya Liwale Mkoa wa Lindi, karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni watano wa Mheshimiwa Ravia Idarus Faina, ambao ni viongozi wa Jumuiya ya Wazazi Wadi kutoka Makunduchi Mkoa wa Kusini Zanzibar, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni wawili wa Mheshimiwa Festo Richard Sanga, ambao ni wafanyabiashara kutoka Jijini Dar es Salaam, karibuni sana. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Jacqueline Andrea Kainja, ambaye ni ndugu yake kutoka Afrika Kusini, karibu sana. *(Makofi)*

Wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo. Wapo wageni 16 wa Mheshimiwa Dkt. Hamisi Andrea Kigwangalla, ambao ni wafanyakazi wa Shirika Lisilo la Kiserikali la *One Health Society* kutoka Jijini Dar es Salaam, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wajasiriamali 30 kutoka Wilaya ya Mvomero, Mkoa wa Morogoro, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wanafunzi 45 na Walimu wawili wa Chuo cha Biblia kutoka Jijini Dodoma, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wanafunzi wanafunzi 45 na Walimu watano kutoka Kituo cha *Chilemu Academy* kinachojihusisha na kutoa masomo ya ziada kwa wanafunzi wa Shule za Msingi na Sekondari Mkoa wa Morogoro, karibuni sana. *(Makofi)*

Wapo wanafunzi 100 na Walimu nane wa Shule ya Msingi Mtemi Mazengo kutoka Jijini Dodoma, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, nina tangazo kutoka kwa Katibu wa Bunge, anawatangazia Waheshimiwa Wabunge wote, kwamba leo kutakuwa na semina kuhusu rasimu ya awali ya Dira ya Taifa ya mwaka 2050 inayotolewa na Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji. Lengo la semina hiyo ilifafanuliwa sana jana lakini tufahamu tu Waheshimiwa Wabunge tunatarajiwa kutoa ushauri na maoni kwa ajili ya kuboresha rasimu hiyo.

Waheshimiwa Wabunge, semina hii itafanyika mara baada ya kusitisha Shughuli za Bunge na itafanyikia katika Ukumbi wetu wa Msekwa. Wote mnatakiwa kuhudhuria, baada ya matangazo hayo tunaendelea na ratiba yetu.

Katibu.

**NDG. BARAKA I. LEONARD – KATIBU WA BUNGE:**

## KAMATI YA MIPANGO

**MWENYEKITI:** Kamati ya Mipango. *(Makofi)*

Haya, ahsante sana Waheshimiwa Wabunge, japokuwa sijajua mnashangilia nini, lakini ahsanteni sana. *(Makofi/Kicheko)*

Katibu.

**NDG. BARAKA I. LEONARD – KATIBU WA BUNGE.**

## Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa Unaokusudiwa Kutekelezwa na Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026

**na**

**Mapendekezo ya Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tupo kwenye Kamati ya Mipango kwa kadiri ya Kanuni yetu ya 113 inavyotutaka. Sasa tunaanza na Mheshimiwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji ili aje awasilishe Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa, Mheshimiwa Prof. Kitila Alexander Mkumbo. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia Kanuni ya 113(1) na (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari ,2023, naomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako likae kama Kamati ya Mipango ili kupokea na kujadili Mapendekezo ya Mpango wa Taifa wa Maendeleo kwa mwaka 2025/2026. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti, wakiongozwa na Mwenyekiti wake Mheshimiwa Oran Manase Njeza, Mbunge wa Mbeya Vijijini na Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Twaha Ally Mpembenwe, Mbunge wa Kibiti, kwa maoni na ushauri wakati wa vikao vya Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kukuhakikishia kuwa maoni na ushauri wa Kamati umezingatiwa na utaendelea kuzingatiwa katika kuandaa Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka 2025/2026.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utakumbuka kwamba mwaka 2023, nikiwasilisha mapendekezo kama haya nilikuwa peke yangu katika Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji kwa maana ya Waziri. Nachukua nafasi hii kumshukuru sana Mheshimiwa Rais, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kuweza kumteua Mheshimiwa Stanslaus Haroon Nyongo, Mbunge kuwa Naibu Waziri wa Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tangu Mheshimiwa Nyongo, ajiunge na sisi amerahisisha kazi zetu, ni kiongozi mahiri sana, mtu

ambaye ana ushirikiano na utayari wa kuchapa kazi wakati wowote. Ninamshukuru sana Mheshimiwa Nyongo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo yamezingatia maudhui ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025, Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/2022 - 2025/2026, Ilani ya Chama Cha Mapinduzi kwa ajili ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020, *Agenda* ya Maendeleo ya Afrika 2063, Malengo ya Maendeleo Endelevu 2030 na mipango mingine ya kikanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, mapendekezo haya yamezingatia kikamilifu maono ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, hususan misingi iliyojengwa katika Falsafa ya *4R* yaani Maridhiano, Ustahimilivu, Mageuzi na Kujenga Upya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kitabu cha Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2025/2026 yanawasilishwa katika Sura Tano. Sura ya Kwanza ni Utangulizi; Sura ya Pili ni Tathmini ya Mwenendo wa Hali ya Uchumi; Sura ya Tatu ni Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2023/2024; Sura ya Nne ni Mapendekezo ya Vipaumbele na Malengo ya Kuzingatiwa katika Maandalizi ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2025/2026; na Sura ya Tano ni Ufuatiliaji, Tathmini na Vihatarishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pamoja na hotuba yangu hii, Kitabu ambacho tumewasilisha kiwe sehemu ya *Hansard*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Utangulizi ambao upo ukurasa wa pili mpaka wa tano wa Kitabu ambacho tumewasilisha, tumeainisha mawanda ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/2022 - 2025/2026 ambayo yanaweka msingi wa maudhui ya Mpango wa Mwaka ujao 2025/2026. Aidha, Utangulizi umeainisha mapendekezo ya malengo ya mpango wa mwaka 2025/2026.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2025/2026, Serikali inatarajia kutumia shilingi trilioni 16.459 kwa ajili ya kugharamia

programu na miradi ya maendeleo. Vyanzo vya fedha hizi ni pamoja na mapato ya ndani, misaada, mikopo ya ndani yenye masharti ya biashara na mikopo ya nje yenye masharti nafuu na masharti ya kibiashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Serikali itaendelea kuimarisha njia mbadala za ugharamiaji wa miradi ya maendeleo kwa kuendelea kuweka mazingira mazuri kwa ajili ya kuvutia uwekezaji, pia utekelezaji wa miradi kwa njia ya ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafsi *(PPP)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwenendo wa Hali ya Uchumi nimeeleza kwa kina katika sura ya pili, ukurasa wa saba mpaka 21 wa vitabu ambavyo tumewasilisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pato halisi la Taifa kwa bei za mwaka 2015 lilifikia shilingi trilioni148.4 kwa mwaka 2023 ikilinganishwa na shilingi trilioni 141.25 kwa mwaka 2022, sawa na ukuaji wa 5.1%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, malengo na shabaha za uchumi zipo katika ukurasa wa 21 ni kama ifuatavyo: -

(i) Pato halisi la Taifa linakadiriwa kukua kwa 5.4% mwaka 2024 na kuongezeka hadi 5.8% mwaka 2025 na 6.1% mwaka 2026;

(ii) Mfumko wa bei unatarajiwa kubaki kwenye wigo wa tarakimu moja na wastani wa asilimia kati ya tano mpaka tano kwa muda wa kati;

(iii) Mapato ya ndani kufikia 16.1% na mapato ya kodi 13.0% ya pato la Taifa kwa mwaka 2025/2026;

(iv) Kuwa na akiba ya fedha za kigeni kwa kiwango kinachokidhi mahitaji ya uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje kwa kipindi kisichopungua miezi minne.

Mheshimiwa Mwenyekiti, thamani ya mauzo ya bidhaa na huduma nje iliongezeka kwa 14.7% na kufikia dola za Marekani shilingi bilioni 14.7 ikichangiwa zaidi na mauzo ya dhahabu na

bidhaa asilia pamoja na mapato ya utalii. Thamani ya bidhaa na huduma zilizoagizwa kutoka nje zimepungua kwa 5.6% na kufikia dola za Marekani bilioni 16.03.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwenendo huu umetokana na kupungua kwa gharama ya uagizaji wa bidhaa, hususan mafuta ya petroli, mitambo, na vifaa vya viwandani na mbolea na kuongezeka kwa mauzo ya bidhaa na huduma nje. Kupungua kwa nakisi ya malipo ya nje ni ishara nzuri inayoonesha uwezo wa kudhibiti mahitaji ya fedha za kigeni na kujenga akiba ya fedha za kigeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka 2023/2024, kiwango cha akiba ya fedha za kigeni ilifikia dola za Marekani bilioni 5.345 ikilinganishwa na dola za Marekani bilioni 5.21 kipindi kama hicho mwaka 2022/2023, hivyo kuendelea kukidhi mahitaji ya uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiasi hicho kinatosheleza malipo ya uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje ya nchi kwa kipindi cha miezi 4.4, zaidi ya lengo la nchi la kuwa na akiba ya fedha za kigeni inayokidhi uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje kwa miezi isiyopungua minne.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ujumla, kama ambavyo taasisi mbalimbali za kimataifa zimekuwa zikieleza, uchumi wa Tanzania umeendelea kuhimili vyema changamoto za dunia zilizojitokeza katika miaka ya hivi karibuni. Kwa mujibu wa taasisi hizo, pamoja na changamoto zilizojitokeza, uchumi wetu umeendelea kuimarika kutokana na sababu kuu tatu:-

(i) Utekelezaji wa mageuzi makubwa yaliyolenga katika kuchochea na kuimarisha ushindani katika uchumi, sambamba na eneo la kwanza la kipaumbele cha Mpango wa Maendeleo ambalo ni kuchochea uchumi shindani na shirikishi;

(ii) Kuendelea kuboresha na kuimarisha mazingira ya biashara na uwekezaji nchini;

(iii) Kuendelea kuaminiwa na taasisi za fedha duniani, pamoja na wadau wetu wa maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuhakikisha kuwa ukuaji wa uchumi unakuwa na athari chanya katika kuinuia kiwango cha miasha ya watu wetu na kupunguza umaskini, Dira ya Taifa ya Maendeleo inayoandaliwa, na mipango itakayoambatana nayo, itajikita katika kuhakikisha kuwa ukuaji wa uchumi wetu unakuwa jumuishi, unapunguza umaskini, unazalisha ajira nyingi, na unachochea mauzo ya bidhaa zilizoongezwa thamani nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kufikia azma hii, mkazo mahususi utawekwa katika sekta za uzalishaji ambazo zinahusisha watu wengi. Mkazo wa kipekee utaendelea kuwekwa katika kuchochea maendeleo kijamii na kiuchumi vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa nieleze Mafanikio ya Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo 2023/2024 kama sehemu ya utekelezaji wa Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano. Pamoja na mambo mengine, Serikali imepanga kutekeleza miradi 17 ya kielelezo inayolenga kuleta matokeo makubwa katika maeneo hayo matano ya kipaumbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi hii imegawanyika makundi mawili, ambayo ni miradi ya miundombinu ya usafiri na usafirishaji; na miradi ya kuongeza uzalishaji viwandani. Taarifa ya kina kuhusu utekelezaji wa miradi hii ipo katika sura ya tatu ya kitabu ambacho tumewasilisha ukurasa wa 23 mpaka 56.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue nafasi hii kueleza kwa upana kidogo kuhusu mafanikio yaliyopatikana na yanayoendelea kupatikana kutokana na utekelezaji wa baadhi ya miradi ya kimkakati na nimechagua miradi mikubwa mitatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, ni uwekezaji katika Bandari ya Dar es Salaam. Tarehe 22 Oktoba, 2023 Serikali, kupitia Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari *(TPA)*, ilisaini mikataba mitatu

ya uwekezaji na Kampuni ya *DP World*. Mkataba huu unahusisha uendeshaji wa shughuli za bandari katika uhudumiaji wa Makasha, Mzigo Mchanganyiko, Mzigo wa Kichele na Shehena ya Magari. Ili kutoa huduma hizi, kwa kuzingatia sheria zetu, Kampuni ya *DP World* ilifungua Kampuni ya Tanzania inayoitwa *DP World* Dar es Salaam. Kampuni hii ilikabidhiwa rasmi shughuli za uendeshaji wa bandari tarehe 15 Aprili, 2024.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tangu Kampuni hii ianze uendeshaji wa shughuli za bandari mafanikio mbalimbali yamepatikana. Naomba nieleze hapa mafanikio kumi ambayo yamepatikana katika miezi mitano ya uwekezaji wa Kampuni ya *DP World* katika Bandari ya Dar es Salaam.

(i) Kwa mujibu wa mkataba, Kampuni hii inapaswa kuwekeza Dola za Kimarekani milioni 250 sawa na shilingi bilioni 675 katika kipindi cha miaka mitano. Katika kipindi cha miezi mitano tayari imeshawekeza shilingi bilioni 214.425 sawa na 31% ya lengo la kuwekeza shilingi bilioni 675 na fedha zimewekezwa katika manunuzi ya mitambo ya kisasa; Ukarabati wa mitambo iliyokuwa ya *TPA;* na usanifu na usimikaji wa mifumo ya *TEHAMA* ya kisasa kwa ajili ya uendeshaji wa shughuli za Bandari;

(ii) Wastani wa muda wa meli kusubiri kwenye nanga umepungua kutoka wastani wa siku 46 mwezi Mei, 2024 hadi kufikia wastani wa siku saba saba ikiwa ni siku sifuri kwa meli za makasha, siku 12 kwa meli za kichele, na siku 10 kwa meli za mzingo mchanganyiko;

(iii) Kampuni imefunga vitendea kazi vya kisasa vya *SSG* na *RTG* na kufuatia kufungwa kwa mitambo hii, katika kupakia na kushusha mizigo, muda wa kuhudumia meli za makasha kwenye gati umepungua kutoka wastani wa siku saba hadi wastani wa siku tatu, na hivyo kupunguza idadi ya meli zinazosubiri kwenye nanga kutoka wastani wa meli 35 mwezi Septemba, 2023 hadi wastani wa meli 15 mwezi Septemba, 2024;

(iv) Kuongezeka kwa shehena zinazohudumiwa kutoka shehena 141,889 mwezi Mei, 2024 hadi kufikia shehena 168,331

mwezi Septemba, 2024, ikiwa ni ongezeko la asilimia 18.6 katika kipindi cha miezi mitano;

(v) Kuongezeka kwa idadi ya makasha yanayohudumiwa *(Twenty-Feet Equivalent Units*) katika Bandari ya Dar es Salaam, *Terminal One* kutoka wastani wa makasha 12,000 kwa mwezi hadi kufikia makasha 27,000 kwa mwezi Septemba, 2024. Idadi hii ya makasha ilikuwa haijawahi kufikiwa katika historia ya Bandari ya Dar es Salaam. Kiwango cha juu kabisa kabla ya hii ilikuwa ni makasha 15,000;

(vi) Katika kipindi cha miezi mitano gharama za matumizi ya uendeshaji wa bandari zimepungua hadi kufikia 2.7% ya makusanyo wakati ambapo matumizi yalikuwa yanaongezeka kwa 15.1% kwa mwezi kabla ya kukabidhiwa uendeshaji wa bandari kwa kampuni hii.

(vii) Katika kipindi cha miezi mitano Aprili hadi Septemba, 2024 tangu *DP World* Dar es Salaam waanze kuendesha Gati 0 - 7 katika Bandari ya Dar es Salaam Serikali imeshakusanya jumla ya shilingi bilioni 325.3 ikiwa ni mapato yanayotokana na shughuli za mikataba iliyoingiwa kati ya *TPA* na *DP World,* ikijumuisha tozo ya pango *(land rent),* tozo ya mrahaba, na Ardhia *(wharfage)*.

(viii) Kutokana na kuongezeka kwa mapato na kupungua kwa gharama za uendeshaji, kufuatia maboresho yaliyofanyika, Serikali kupitia *TPA,* imeanza uwekezaji katika miradi yenye thamani ya shilingi trilioni 1.922 kwa kutumia makusanyo yanayopatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha hizi ingelazimika Serikali kukopa ili kuwekeza, lakini sasa hatukopi, tunatumia makusanyo ambayo yanapatikana kutokana na uwekezaji wa *DP World*. *(Makofi)*

(ix) Kuunganishwa kwa mifumo ya forodha *(Tanzania Customs Integrated System)* na ile ya bandari *(Tanzania Electronic Single Window System)*. Hii imewezesha kupunguzwa na kuondolewa kwa mifumo iliyokuwa inafanana na hivyo

kupunguza muda wa kuondoa mizigo bandarini, kuongeza uwazi na kurahisisha mawasiliano;

Mheshimiwa Mwenyekiti, utakumbuka kwamba kwa muda mrefu Serikali imekuwa ikipiga kelele juu ya umuhimu wa kuunganisha mifumo hii, lakini sasa imewezekana imeunganishwa na imerahisisha sana kuweza kuondoa mizigo bandarini;

(x) Mapato ya kodi ya Mamlaka ya Mapato Tanzania *(TRA)* yameongezeka hadi kufikia trilioni moja mwezi Septemba, 2024 ukilinganisha na wastani wa bilioni 850 kwa mwezi. Hii imetokana na *TRA* kuweza kuchakata mizigo mingi zaidi ndani ya muda mfupi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ujumla wake, maboresho yanayoendelea katika Bandari ya Dar es Salaam kufuatia kukabidhiwa kwa *DP World* na makampuni mengine kuendesha Bandari ya Dar es Salaam, yanaonesha kuwa yana faida kubwa kiuchumi kwa kuchochea kuongezeka kwa biashara na kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji nchini. Uwekezaji huu ni sehemu muhimu ya utekelezaji wa azma ya Serikali ya kuifanya Bandari ya Dar es Salaam kuwa lango kuu la usafirishaji mizigo katika ukanda wa Afrika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeeleza kwa kina kidogo yanayoendelea katika maeneo ya Dar es Salaam kutokana na ukweli kwamba kama unavyofahamu, uamuzi wa Serikali wa kuikaribisha kampuni ya *DP World* kuwekeza katika maeneo ya Dar es Salaam ulikumbana na upinzani wa ukosoaji mkali sana kutoka kwa makundi mbalimbali ya wanaharakati na wanasiasa. Nichukue nafasi hii kumshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa ushupavu, ujasiri na ustahimilivu wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, licha ya upinzani mkali na kila aina ya kejeli, Rais wetu alisimama imara. Alichokionesha Rais wetu wakati wa sakata la *DP World* ni kile ambacho Rais wa tatu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Hayati Benjamin William Mkapa aliuita ushupavu wa uongozi katika hotuba yake kwenye Mkutano wa Halmashauri Kuu ya CCM, Rais Mkapa aliyoitoa

tarehe 25 Agosti, 2004 aliainisha sifa nne kuu za ushupavu wa uongozi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ni upeo mkubwa wa kubuni malengo na dira; pili, ni uongozi mathubuti wa watu na rasilimali kuelekea kwenye malengo hayo na kuzingatia dira hiyo; tatu, muhimu kabisa, baada ya kuridhia malengo ni ung'ang'anizi na kukataa kuyumbishwa bila sababu za msingi; na nne, ni ujasiri wa kusimamia na kutetea maadili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni maoni yangu kwamba Rais wa Awamu ya Sita wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, amejibainisha wazi kuwa anazo sifa hizi. Rais wetu ni kiongozi madhubuti ambaye tukishakubaliana malengo na dira hakubali kuyumbishwa bila sababu za msingi. Ni kwa msingi huo katika hili suala la uwekezaji wa *DP World* Rais wetu alisimama imara na alikataa kuyumbishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni rai yangu kwa wenzetu waliokuwa wanapinga mradi huu wakisema hauna faida yoyote, kwa ujasiri ule ule na ushupavu ule ule walioonesha katika kuupinga kutokana na mafanikio makubwa yanayopatikana, ni uungwana watoke hadharani wakiri mafanikio haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi wa pili ambao ningependa kuuelezea kwa kirefu kidogo hasa kutokana na mafanikio yake makubwa kiuchumi na kijamii ni Mradi wa Ujenzi wa Reli ya Kiwango cha *Standard Gauge (SGR)*. Kama unavyofahamu, katika mwaka 2023/2024 Serikali iliendelea na utekelezaji wa mradi huu muhimu wenye lengo la kuifanya Tanzania kuwa kitovu cha usafiri na usafirishaji katika ukanda wa Kusini mwa Jangwa la Afrika na Afrika kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa Serikali, kupitia Shirika la Reli nchini *(TRC)* inaendelea na ujenzi wa awamu ya kwanza kutoka Dar es Salaam hadi Mwanza yenye urefu wa kilometa 1,219 na awamu ya pili inayojumuisha ujenzi wa vipande vya Tabora – Kigoma; Uvinza – Malagarasi - Musongati; na Kaliua – Mpanda – Karema yenye urefu wa Kilometa 1,010.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa awamu ya kwanza kama unavyofahamu, upo katika vipande vitano na tumevieleza kwa kina katika vitabu ukurasa wa 24. Hadi sasa Serikali imeshawekeza kiasi cha Dola za Kimarekani Bilioni 10, sawa na zaidi ya shilingi trilioni 23 tangu ujenzi wa mradi huu ulipoanza tarehe 2 Mei, 2017. Hadi sasa kipande cha Dar es Salaam hadi Dodoma kimeshakamilika na kinafanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imefanya tathmini ya awali kuhusu manufaa ya mradi huu ya kiuchumi na kijamii na tumebainisha manufaa ya awali tisa yafuatayo: -

(i) Hadi sasa mradi umeshazalisha ajira zaidi ya 30,176 za moja kwa moja na ajira zaidi ya 150,000 zisizo za moja kwa moja. Ajira hizi zimetengeneza pato la shilingi bilioni 358.74;

(ii) Mradi umeshatoa fursa kwa viwanda, wazabuni na wakandarasi ambapo hadi sasa jumla ya kampuni 2,460 zinashiriki katika mradi huu na kandarasi zenye thamani ya shilingi trilioni 3.69 zimetolewa tangu mradi uanze;

(iii) Mradi umechochea kuongezeka kwa mahitaji ya saruji, nondo, na vifaa vingine vya ujenzi na kuongeza mchango wa sekta ya viwanda katika uchumi;

(iv) Kupungua kwa muda wa safari kati ya Dar es Salaam na Dodoma kutoka wastani wa masaa kumi kwa basi hadi masaa matatu na nusu kwa Treni;

(v) Kupunguza ajali na kuokoa maisha ya watu;

(vi) Kutunza mazingira na kupungua kwa uzalishaji wa hewa ya ukaa kwa kuwa usafiri wa treni unatumia nishati ya umeme na kwa kuwa safari za mabasi zimepungua;

(vii) Kuzalisha kipato ambapo hadi kufikia Septemba, 2024 jumla abiria 645,421 walisafirishwa na kiasi cha shilingi 15.695 bilioni kilipatikana;

(viii) Kuchochea shughuli za utalii katika ukanda ambao reli inayopita, hususan Hifadhi ya Mikumi na Hifadhi ya Ruaha kupitia Stesheni ya Kilosa, na vilevile tutakapoendelea kujenga Hifadhi ya Katavi kupitia Stesheni ya Tabora, Hifadhi ya Gombe kupitia Stesheni ya Kigoma, na Hifadhi ya Serengeti kupitia Stesheni za Malampaka na Mwanza. Taarifa zilizopo ni kwamba Mbuga yetu ya Wanyama ya Mikumi imechangamka sana tangu usafiri wa treni uanze; na

(ix) Ujenzi wa mradi huu unatarajiwa kuchochea mazingira ya biashara na uwekezaji kwa kupunguza muda wa safari na gharama za usafirishaji wa mizigo na abiria na hivyo kuchochea ukuaji wa biashara za ndani na kimataifa. Hadi Septemba, 2024 jumla ya miradi 519 imesajiliwa na Kituo cha Uwekezaji *(TIC)* katika ushoroba wa reli yenye kuvutia mtaji wa Dola za Marekani bilioni 4.59 na unaotarajiwa kuzalisha ajira 115,566. Tayari baadhi ya miradi imeshaanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho niseme hili, ukiacha faida za kiuchumi na kijamii mradi huu umeleta furaha, Watanzania wengi wanajisikia vizuri sana kuona treni yao. Wana furaha na hilo ni jambo la msingi sana katika maisha kwa sababu maisha ni mchakato wa kuongeza furaha, mradi umeongeza furaha ya Watanzania, tunashukuru sana. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa uamuzi wake thabiti wa kuhakikisha kwamba tunatekeleza miradi hii kwa kina.

Mheshimiwa Mwenyekiti na Waheshimiwa Wabunge, pale ambapo tunagundua kwamba baadhi ya miradi imeathirika tuelewe kwa sababu miradi hii miwili peke yake, hiyo ambayo tumeitaja niseme mradi huu wa *SGR* na mradi wa bwawa letu, imekula fedha nyingi na kupanga ni kuchagua. Kwa hiyo, hili jambo ni muhimu sana tukalizingatia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeeleza miradi yote, lakini pia niseme kwamba ujenzi wa Daraja la Kigongo - Busisi na wenyewe umefikia 92.15%. Kukamilika kwa mradi huu utakuwa ni ukombozi sana wa kiuchumi katika kanda ya ziwa. Ni mradi muhimu sana ambao tunatarajia ufungue fursa nyingi za kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa nijielekeze eneo la mwisho nielezee mapendekezo ya vipaumbele na malengo kwa mwaka 2025/2026. Kama unavyofahamu Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2025/2026 utakuwa ni mpango wa mwisho katika kutekeleza Dira yetu ya Maendeleo ya Taifa ya Mwaka 2025, lakini pia mpango wetu wa miaka mitano 2021/2022 hadi 2025/2026.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapendekezo ya Mpango huu ni kiungo kati ya mipango inayokamilika na mipango mipya inayotarajiwa kutekelezwa kupitia Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo, vigezo vya kuchagua vipaumbele katika mpango ujao wa maendeleo tumeviainisha katika vitabu vyetu na vipo vipaumbele vifuatavyo: -

(i) Tunazingatia ukuaji endelevu wa uchumi;

(ii) Tutazingatia miradi itakayochochea kupunguza umaskini;

(iii) Miradi ambayo itazalisha ajira kwa wananchi;

(iv) Tutazingatia miradi ambayo inaimarisha uwezo wetu wa kushindana na hususan uwezo wetu wa kuuza bidhaa nje ya nchi ambazo zimeongezwa thamani;

(v) Maendeleo endelevu kwenye miradi ambayo itazingatia utunzaji wa mazingira; na mwisho

(vi) Miradi ambayo itazingatia utawala bora na utawala wa sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vipaumbele vinayopendekezwa katika Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2025/2026 vimezingatia kikamilifu kama nilivyoeleza awali, malengo tarajiwa na matokeo ambayo yamo katika Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano. Mpango huu una vipaumbele vikubwa vitano ambavyo tunaendelea kuvitekeleza:-

(i) Kuchochea uchumi shindani na shirikishi. Hapa tunaendelea na ujenzi wa miundombinu ya usafiri na usafirishaji ikiwemo reli ambayo nimeieleza pamoja na barabara, nishati, kuwekeza katika maji safi na salama, teknolojia na miradi mingine ikiwemo uchakataji wa gesi;

(ii) Kuimarisha uwezo wa uzalishaji wa bidhaa viwandani na utoaji huduma. Hapa tunaendelea na mpango wetu wa kuendelea kuimarisha uzalishaji katika bidhaa zetu viwandani lakini muhimu zaidi ni kuendelea kuwekeza katika madini ya kimkakati kwa maana ya *strategic mineral resources*, kuongeza thamani ndani ya nchi yetu;

(iii) Kukuza uwekezaji na biashara;

(iv) Kuchochea maendeleo ya watu tukijikita katika kuimarisha mifumo na usimamizi wa uendelezaji wa elimu, afya, maji na hifadhi ya mazingira; na katika upande wa elimu kuhakikisha kwamba tunaanza kikamilifu kutekeleza mitaala na sera mpya ya elimu ambayo tumeshaipitisha; na

(v) Kuendeleza rasilimali watu ikiwemo kukuza ujuzi kwa vijana, kuwezesha na kuendeleza ujuzi kwa makundi mbalimbali katika ngazi zote za elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mafanikio ya utekelezaji wa vipaumbele ambavyo nimevieleza kwa mwaka ujao yatajengwa katika misingi tisa ifuatayo: -

(i) Kuendelea kuwepo kwa amani, usalama na utulivu wa ndani ya nchi na katika nchi jirani;

(ii) Kuendelea kudumisha utawala bora na utawala wa sheria nchini;

(iii) Kuimarika kwa upatikanaji na usalama wa chakula nchini;

(iv) Kuongezeka kwa ushiriki wa sekta binafsi katika shughuli za uwekezaji na biashara;

(v) Kuendelea kuhimili athari za mabadiliko ya tabianchi na majanga ya asili na yasiyo ya asili;

(vi) Kuwa na nidhamu katika utekelezaji wa mpango na bajeti;

(vii) Kutekeleza kikamilifu mfumo wa ufuatiliaji na upimaji unaozingatia viashiria vya matokeo;

(viii) Kuimarika kwa uchumi wa dunia na utulivu wa bei katika masoko ya fedha na bidhaa; na

(ix) Kuendelea kwa utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapohitimisha, nichukuwe nafasi hii kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwanza kwa kuendelea kuniamini kuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mipango, ni heshima na bahati kubwa. Pili, niendelee kumshukuru sana kwa maono yake na usimamizi imara wa sera za Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, niruhusu niwashukuru viongozi wengine wakuu: Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais; Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Mbunge na Waziri Mkuu; na Mheshimiwa Dkt. Doto Mashaka Biteko, Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati kwa uongozi wao makini na maelekezo yao thabiti katika usimamizi wa shughuli za Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii pia kukushukuru wewe, Mheshimiwa Spika wetu, siyo tu kwa jinsi ambavyo unaongoza Bunge hili kwa umahiri mkubwa, lakini kwa jinsi ambavyo kama nilivyosema jana unavyoijengea nchi yetu heshima nje ya nchi huko duniani. Watanzania wanajisikia furaha na fahari sana kuwa nawe kama Spika wetu lakini muhimu kama Rais wa Umoja wa Mabunge Duniani, Mungu aendelee kukubariki sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwashukuru watumishi wenzangu wakiongozwa na Mheshimiwa Stanslaus Haroon Nyongo, Mbunge wa Maswa Mashariki, Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Mipango na

Uwekezaji kwa jinsi ambavyo ananisaidia sana katika kutekeleza majukumu haya ambayo Mheshimiwa Rais ametupatia. Nimshukuru sana Dkt. Tausi Mbaga Kida, Katibu Mkuu, ambaye ni msimamizi muhimu na mahiri sana wa Ofisi ya Rais Mipango na Uwekezaji, Ofisi yetu imetulia sana kwa sababu ya utendaji wake mahiri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Katibu Mtendaji wa Tume ya Mipango, Ndugu Lawrence Mafuru, na timu yake ya mipango kwa ushirikiano wanaotupa katika kutekeleza majukumu yetu. Aidha, kwa upekee, ninawashukuru sana Katibu Mkuu, Katibu Mtendaji akiwemo Kaimu Katibu Mtendaji Dkt. Milanzi kwa maandalizi mazuri ya nyaraka ambazo zimeniwezesha kuwasilisha hotuba hii hapa Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo, naomba sasa Kamati yako ipokee na kujadili Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka 2025/2026 kwa ajili ya maandalizi ya mpango na ustawi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

## HOTUBA YA WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UWEKEZAJI, MHE. PROF. KITILA ALEXANDER MKUMBO (MB.), AKIWASILISHA BUNGENI MAPENDEKEZO YA MPANGO WA MAENDELEO WA TAIFA WA MWAKA 2025/26 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

### I. UTANGULIZI

**1.** ***Mheshimiwa Spika,*** Kwa kuzingatia Kanuni ya 113 (1) na (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari 2023, ninaomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako likae kama Kamati ya Mipango ili kupokea na kujadili Mapendekezo ya Mpango wa Taifa wa Maendeleo kwa Mwaka 2025/2026.

**2.** ***Mheshimiwa Spika,*** Ninaishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti, wakiongozwa na Mwenyekiti wake Mheshimiwa Oran Manase Njeza, Mbunge wa Mbeya Vijijini (CCM) na Makamu Mwenyekiti Mheshimiwa Twaha Ally Mpembenwe, Mbunge wa Kibiti (CCM), kwa maoni na ushauri wakati wa vikao

vya kamati. Ninapenda kukuhakishia kuwa maoni na ushauri wa Kamati umezingatiwa na utaendelea kuzingatiwa katika kuandaa Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka 2025/26.

**3.** ***Mheshimiwa Spika,*** Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo yamezingatia maudhui ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025; Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/22 - 2025/26; Ilani ya Chama Cha Mapinduzi kwa ajili ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020; Agenda ya Maendeleo ya Afrika 2063; Malengo ya Maendeleo Endelevu 2030 na mipango mingine ya kikanda.

**4.** ***Mheshimiwa Spika,*** Aidha, mapendekezo haya yamezingatia kikamilifu maono ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, hususani misingi iliyojengwa katika falsafa ya ***4R*** (***Reconciliation, Resilience, Reform*** and ***Rebuilding***) yaani Maridhiano, Ustahimilivu, Mageuzi na Kujenga Upya.

**5.** ***Mheshimiwa Spika,*** Kitabu cha Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2025/26 yanawasilishwa katika Sura Tano. Sura *ya Kwanza* ni Utangulizi. *Sura ya Pili* ni tathmini ya mwenendo wa hali ya uchumi na *Sura ya Tatu* ni mapitio ya ya utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2023/2024. *Sura ya Nne* ni mapendekezo ya vipaumbele na malengo ya kuzingatiwa katika maandalizi ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2025/2026. *Sura ya Tano* ni Ufuatiliaji, Tathmini na Vihatarishi.

**6.** ***Mheshimiwa Spika***, katika Utangulizi (uk.2-5), tumeanisha mawanda ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/22 2025/26 ambayo yanaweka msingi wa maudhui ya Mpango wa mwaka 2025/26. Aidha, Utangulizi umeainisha mapendekezo ya malengo ya mpango wa mwaka 2025/26.

**7.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2025/2026, Serikali inatarajia kutumia TZS bilioni 16,459.43 (trilioni 16.459) kwa ajili ya kugharamia programu na miradi ya maendeleo. Vyanzo vya fedha hizi ni pamoja na mapato ya ndani, misaada, mikopo ya

ndani yenye masharti ya biashara na mikopo ya nje yenye masharti nafuu na masharti ya kibiashara. Aidha, serikali itaendelea kuimarisha njia mbadala za ugharamiaji wa miradi ya maendeleo kwa kuendelea kuweka mazingira mazuri ya biashara na uwekezaji, pamoja na utekelezaji wa miradi kwa njia ya ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafsi (PPP).

## II. MWENENDO WA HALI YA UCHUMI WA DUNIA

**8.** ***Mheshimiwa Spika,*** Hali ya Uchumi imeelezwa katika Sura ya pili (uk. 7-21).

**9.** ***Mheshimiwa Spika,*** Pato halisi la Taifa kwa bei za mwaka 2015 lilifikia shilingi bilioni 148,399.76 kwa mwaka 2023 ikilinganishwa na shilingi bilioni 141,247.19 mwaka 2022, sawa na ukuaji wa asilimia 5.1. Malengo na shabaha za uchumi jumla (uk.21) ni kama ifuatavyo:

i) Pato halisi la taifa linakadiriwa kukua kwa asilimia 5.4 mwaka 2024 na kuongezeka hadi asilimia 5.8 mwaka 2025 na asilimia 6.1 mwaka 2026;

ii) Mfumuko wa bei unatarajiwa kubaki kwenye wigo wa tarakimu moja na wastani wa asilimia kati ya 3.0 – 5.0 katika muda wa kati;

iii) Mapato ya ndani kufikia asilimia 16.1 na mapato ya kodi asilimia 13.0 ya pato la Taifa kwa mwaka 2025/26;

iv) Kuwa na akiba ya fedha za kigeni kwa kiwango kinachokidhi mahitaji ya uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje kwa kipindi kisichopungua miezi minne.

**10.** ***Mheshimiwa Spika,*** Thamani ya mauzo ya bidhaa na huduma nje iliongezeka kwa asilimia 14.7 na kufikia dola za Marekani milioni 14,663.9, ikichangiwa zaidi na mauzo ya dhahabu na bidhaa asilia pamoja na mapato ya utalii. Thamani ya bidhaa na huduma zilizoagizwa kutoka nje ilipungua kwa asilimia 5.6 na kufikia dola za Marekani milioni 16,027.0. Mwenendo huu ulitokana na kupungua kwa gharama ya uagizaji

wa bidhaa, hususan mafuta ya petroli, mitambo, na vifaa vya viwandani na mbolea na kuongezeka kwa mauzo ya bidhaa na huduma nje. Kupungua kwa nakisi ya malipo ya nje ni ishara nzuri inayoonesha uwezo wa kudhibiti mahitaji ya fedha za kigeni na kujenga akiba ya fedha za kigeni.

**11.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha mwaka 2023/24, kiwango cha akiba ya fedha za kigeni ilifikia dola za Marekani milioni 5,345.5 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 5,208.3 kipindi kama hicho mwaka 2022/23 hivyo kuendelea kukidhi mahitaji ya uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje ya nchi. Kiasi hicho kinatosheleza malipo ya uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje ya nchi kwa kipindi cha miezi 4.4, zaidi ya lengo la nchi la kuwa na akiba ya fedha za kigeni inayokidhi uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje kwa miezi isiyopungua minne.

**12.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa ujumla, kama ambavyo taasisi mbalimbali za kimataifa (WB, IMF,) zimekuwa zikieleza, uchumi wa Tanzania umeendelea kuhimili vyema changamoto za dunia zilizojitokeza katika miaka ya hivi karibuni. Kwa mujibu wa taasis hizo, pamoja na changamoto zilizojitokeza, uchumi wetu umeendelea kuimarika kutokana na sababu kuu tatu. Mosi, utekelezaji wa mageuzi makubwa yaliyolenga katika kuchochea na kuimarisha ushindani katika uchumi, sambamba na eneo la kwanza la kipaumbele katika ***Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/22 – 2025/26*** -“***Kuchochea Uchumi Shindani na Shirikishi***”. Pili, kuendelea kuboresha na kuimarisha mazingira ya biashara na uwekezaji nchini. Tatu, kuendelea kuaminiwa na taasisi za fedha duniani, pamoja na wadau wetu wa maendeleo.

**13.** ***Mheshimiwa Spika,*** Ili kuhakikisha kuwa ukuaji wa uchumi unakuwa na athari chanya katika kuinuia kiwango cha miasha ya watu wetu na kupunguza umaskini, Dira ya Taifa ya Maendeleo inayoandaliwa, na mipango itakayoambatana nayo, itajikita katika kuhakikisha kuwa ukuaji wa uchumi wetu ***unakuwa jumuishi, unapunguza umaskini, unazalisha ajira nyingi, na unachochea mauzo ya bidhaa zilizoongezwa thamani nje ya nchi***. Ili kufikia azima hii, mkazo mahususi utawekwa katika sekta

za uzalishaji ambazo zinahusisha watu wengi. Mkazo wa kipekee utaendelea kuwekwa katika ***kuchochea maendeleo kijamii na kiuchumi vijijini*** (rural socio-economic development).

## III. MAFANIKIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA MAENDELEO 2023/2024

**14.** ***Mheshimiwa Spika,*** kama sehemu ya utekelezaji wa Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano, pamoja na mambo mengine, Serikali ilipanga kutekeleza miradi 17 ya kielelezo inayolenga kuleta matokeo makubwa katika maeneo hayo matano ya kipaumbele. Miradi hii imegawanyika makundi mawili, ambayo ni miradi ya miundombinu ya usafiri na usafirishaji na miradi ya kuongeza uzalishaji viwandani. Taarifa ya kina kuhusu utekelezaji wa miradi hii ipo katika ***Sura ya Tatu (uk. 23-56)***.

**15.** ***Mheshimiwa Spika,*** ninapenda kuchukua nafasi hii kueleza kwa upana kidogo kuhusu mafanikio yaliyopatikana na yanayoendelea kupatikana kutokana na utekelezaji wa baadhi ya miradi ya kimkakati.

**16.** ***Mheshimiwa Spika,*** tarehe 22 Oktoba 2023 Serikali, kupitia Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA), ilisaini mikataba mitatu ya uwekezaji na kampuni ya DP World (Dubai). Mkataba huu unahusisha uendeshaji wa shughuli za bandari katika uhudumiaji wa Makasha, Mzigo Mchanganyiko, Mzigo wa Kichele na Shehena ya Magari. Ili kutoa huduma hizi, kwa kuzingatia sheria zetu, Kampuni ya DP World ilifungua kampuni ya Tanzania inayoitwa DP World Dar es Salaam. Kampuni hii ilikabidhiwa rasmi shughuli za uendeshaji wa bandari tarehe 15 Aprili 2024.

**17.** ***Mheshimiwa Spika***, tangu kampuni hii ianze uendeshaji wa shughuli za bandari mafanikio mbalimbali yamepatikana kama ifuatavyo:

i) Kwa mujibu wa mkataba, Kampuni ya DPW inapaswa kuwekeza Dola za Kimarekani milioni 250 (TZS bilioni 675) katika kipindi cha miaka mitano. Katika kipindi cha miezi

mitano tayari wameshawekeza TZS 214.425 bilioni (31%) kwa ajili ya manunuzi ya mitambo ya kisasa; ukarabati wa mitambo iliyokuwa ya TPA; na usanifu na usimikaji wa mfumo wa TEHAMA wa kisasa wa uendeshaji wa Bandari;

ii) Wastani wa muda wa meli kusubiri nangani umepungua kutoka siku 46 mwezi Mei 2024 hadi kufikia wastani wa siku saba (7) ikiwa ni siku 0 kwa meli za makasha; siku 12 kwa meli za kichele; na siku 10 kwa meli za Mzingo Mchanganyiko;

iii) Kutokana na matumizi ya vitendea kazi vya kisasa (SSG na RTG) katika kupakia na kushusha mizigo, muda wa kuhudumia meli za makasha gatini umepungua kutoka wastani wa siku saba (7) hadi wastani wa siku tatu (3), na hivyo kupunguza idadi ya meli zinazosubiri angani kutoka wastani wa meli 35 mwezi Septemba 2023 hadi wastani wa meli 15 mwezi Septemba 2024;

iv) Kuongezeka kwa shehena zinazohudumiwa kutoka shehena 141,889 mwezi Mei 2024 hadi kufikia shehena 168,336 mwezi Septemba 2024, ikiwa ni ongezeko la asilimia 18.6 katika kipindi cha miezi mitano;

v) Kuongezeka kwa idadi ya makasha yanayohudumiwa (Twenty-Feet Equivalent Units-TEUs) katika Bandari ya Dar es Salaam kutoka wastani wa makasha 12,000 kwa mwezi hadi kufikia makasha 27,000 kwa mwezi Septemba 2024. Idadi hii ya makasha ilikuwa haijawahi kufikiwa katika historia ya Bandari ya Dar es Salaam. Kiwango cha juu kabisa kabla ya hii ilikuwa ni makasha 15,000;

vi) Katika kipindi cha miezi mitano gharama za matumizi ya uendeshaji wa bandari zimepungua hadi kufikia asilimia 2.7 ya makusanyo wakati ambapo matumizi yalikuwa yanaongezeka kwa asilimia 15.1 kwa mwezi kabla ya kukabidhiwa uendeshaji wa bandari kwa kampuni;

vii) Katika kipindi cha miezi mitano (Aprili hadi Septemba 2024) tangu DPW Dar es Salaam waanze kuendesha Gati 0-7

katika Bandari ya Dar es Salaam Serikali imeshakusanya jumla ya shilingi bilioni 325.3 ikiwa ni mapato yanayotokana na shughuli za mikataba iliyoingiwa kati ya TPA na DP World, ikijumuisha tozo ya pango (land rent), tozo ya mrahaba (royalty), na Ardhia (warfage);

viii) Kutokana na kuongezeka kwa mapato na kupungua kwa gharama za uendeshaji kufuatia maboresho yaliyofanyika, serikali, kupitia TPA, imeanza uwekezaji katika miradi yenye thamani ya TZS 1.922 trilioni (USD 686.628 milioni) kwa kutumia makusanyanyo yanayopatikana. Miradi hii ni Ujenzi wa Kituo cha Kupokwa Mafuta (SRT); Ujenzi wa Bandari ya Kisiwa Mgao (Mtwara); na Ujenzi wa Gati za Majahazi (Dhow Wharf) Dar es Salaam;

ix) Kuunganishwa kwa mifumo ya forodha (Tanzania Customs Integrated System – TANCIS) na ile ya bandari (Tanzania Electronic Single Window System-TeSWS). Hii imewezesha kupunguzwa/kuondolewa kwa mifumo iliyokuwa inafanana na hivyo kupunguza muda wa kuondoa mizigo bandarini, kuongeza uwazi na kurahisisha mawasiliano;

x) Mapato ya kodi ya Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) yameongezeka hadi kufikia TZS Trilioni Moja mwezi Septemba 2024 ukilinganisha na wastani wa TZS 850 bilioni kwa mwezi. Hii imetokana na TRA kuweza kuchakata mizigo mingi zaidi ndani ya muda mfupi;

xi) Kwa ujumla wake, maboresho yanayoendelea katika Bandari ya Dar es Salaam kufuatia kukabidhiwa kwa DP World na makampuni mengine kuendesha Bandari ya Dar es Salaam yanaonesha kuwa na faidi kubwa kiuchumi kwa kuchochea kuongezeka kwa biashara na kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji nchini. Uwekezaji huu ni sehemu muhimu ya utekelezaji wa azima ya serikali ya kuifanya Bandari ya Dar es Salaam kuwa lango kuu la usafirishaji mizigo katika ukanda wa Afrika.

**18. *Mheshimiwa Spika,*** nimeeleza kwa kina kidogo yanayoendelea katika Bandari ya Dar es Salaam kutokana na

ukweli kwamba, kama unavyofahamu, uamuzi wa Serikali wa kuikaribisha Kampuni ya DP World kuwekeza katika Bandari ya Dar es Salaam ulikumbana na upinzani na ukosoaji mkali sana kutoka kwa makundi mbalimbali ya wanaharakati na wanasiasa, na hata baadhi ya taasisi za dini. Nichukue nafasi hii kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa ushupavu, ujasiri na ustahimilivu. Licha ya upinzani mkali na kila aina ya kejeli Rais wetu alisimama imara.

**19.** ***Mheshimiwa Spika,*** Alichokionesha Rais wetu wakati wa sakata la DP World ni kile ambacho Rais wa Tatu wa Jamhuri ya Muungano, Hayati Benjamin Mkapa, aliuita ushupavu wa uongozi. Katika hotuba yake kwenye Mkutano wa Halmashauri Kuu ya CCM Rais Mkapa alioitoa tarehe 25 Agosti 2004 alianisha sifa nne kuu za ushupavu wa uongozi. Kwanza, ni upeo mkubwa wa kubuni malengo na dira. Pili, ***ni uongozi madhubuti wa watu na raslimali kuelekea kwenye malengo hayo na kuzingatia dira hiyo; tatu, baada ya kuridhia malengo ni ung'ang'anizi na kukataa kuyumbishwa bila sababu za msingi***, na ***nne ni ujasiri wa kusimamia na kutetea maadili***. Ni maoni yangu kwamba Rais wa Awamu ya Sita wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, amejibainisha wazi wazi kuwa anazo sifa hizi. Rais wetu ni kiongozi madhubutu ambaye tukishakubaliana malengo na dira hakubali kuyumbishwa bila sababu za msingi, na ni kwa msingi huo katika hili suala la uwekezaji wa DP World hakuyumba na ndio maana leo tunaona matunda yake.

**20.** ***Mheshimiwa Spika,*** mradi wa pili ambao ni muhimu kuutolea maelezo zaidi ni Mradi wa Ujenzi wa Reli ya Kiwango cha Standard Gauge (SGR). Katika mwaka 2023/2024, Serikali iliendelea na utekelezaji wa mradi huu muhimu wenye lengo la kuifanya Tanzania kuwa kitovu cha usafiri na usafirishaji katika ukanda wa Kusini mwa Jangwa la Sahara na Afrika kwa ujumla. Kwa sasa Serikali, kupitia Shirika la Reli nchini (TRC) inaendelea na ujenzi wa awamu ya kwanza kutoka Dar es Salaam hadi Mwanza yenye urefu wa KM 1,219 na awamu ya pili inayojumuisha ujenzi wa vipande vya Tabora – Kigoma; Uvinza –

Malagarasi -Musongati; na Kaliua – Mpanda – Karema yenye urefu wa Kilometa 1,010.

**21.** ***Mheshimiwa Spika,*** ujenzi wa awamu ya kwanza unatekelezwa katika vipande vitano (5) ambavyo ni: Dar es Salaam – Morogoro (KM 300); Morogoro -Makutupora (KM 422); Makutupora – Tabora (KM 368); Tabora – Isaka (KM 165); na Isaka – Mwanza (KM 341). Hatua iliyofikiwa katika utekelezaji wa awamu imeelezwa kwa kina katika Sura ya Tatu ya Kitabu nilichowasilisha (uk. 24).

**22.** ***Mheshimiwa Spika,*** hadi sasa Serikali imeshawekeza kiasi cha ***Dola za Kimarekani Bilioni 10 (sawa na TZS trilioni 23)*** tangu ujenzi wa mradi huu ulipoanza tarehe 02 Mei 2017. Hadi sasa kipande cha Dar es Salaam hadi Dodoma kimeshakamilika na kinafanya kazi.

**23.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imefanya tathmini ya awali ya manufaa ya mradi huu kiuchumi na kijamii na kubaini faida zifuatazo:

i) Hadi sasa mradi umeshazalisha ajira zaidi ya 30,176 za moja kwa moja na ajira zaidi ya 150,000 zisizo za moja kwa moja. Ajira hizi zimetengeneza pato la TZS bilioni 358.74;

ii) Mradi umetoa fursa kwa viwanda, wazabuni na wakandarasi ambapo hadi sasa jumla ya kampuni 2,460 zinashiriki katika mradi huu na kandarasi zenye thamani ya TZS 3.69 trilioni zimetolewa tangu mradi uanze;

iii) Mradi umechochea kuongezeka kwa mahitaji ya saruji, nondo, na vifaa vingine vya ujenzi na kuongeza mchango wa sekta ya viwanda katika Uchumi;

iv) Kupungua kwa muda wa safari kati ya Dar es Salaam na Dodoma kutoka wastani wa masaa kumi kwa basi hadi masaa matatu na nusu kwa Treni;

iv) Kupunguza ajali na kuokoa maisha ya watu;

v) Kutunza mazingira/kupungua kwa uzalishaji wa hewa ya ukaa kwa kuwa usafiri wa treni unatumia nishati ya umeme na kwa kuwa safari za mabasi zimepungua;

vi) Kuzalisha kipato ambapo hadi kufikia Septemba 2024 jumla abiria 645,421 walisafirishwa na kiasi cha TZS 15.695 bilioni kupatikana;

vii) Kuchochea shughuli za utalii katika ukanda ambao reli inayopita, hususan Hifadhi ya Mikumi na Hifadhi ya Ruaha (kupitia Stesheni ya Kilosa), Hifadhi ya Katavi (Stesheni ya Tabora), Hifadhi ya Gombe (Stesheni ya Kigoma), na Hifadhi ya Serengeri (kupitia Stesheni za Malampaka na Mwanza); na

viii) ix) Ujenzi wa mradi huu unatarajiwa kuchochea mazingira ya biashara na uwekezaji kwa kupunguza muda wa safari na gharama za usafirishaji wa mizigo na abiria na hivyo kuchochea ukuaji wa biashara za ndani na kimataifa.

Hadi Septemba 2024 jumla ya miradi 519 imesajiliwa na Kituo cha Uwekezaji (TIC) katika ushoroba wa reli yenye kuvutia mtaji wa Dola za Marekani 4.59 bilioni na kutarajia kuzalisha ajira 115,566. Miradi hii ipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji huku baadhi yake ikiwa imeshakamilika na kuanza uzalishaji.

## V: MAPENDEKEZO YA VIPAUMBELE NA MALENGO KWA MWAKA 2025/26

**24.** ***Mheshimiwa Spika,*** Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2025/26 yanaongozwa na Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 inayolenga kuwezesha Tanzania kuingia katika kundi la nchi za uchumi wa kati ifikapo mwaka 2025 na kuwa na kiwango cha juu cha maendeleo ya watu. Hivyo, mapendekezo ya mpango yamejikita katika kuendeleza na kukamilisha utekelezaji wa afua zinazotoa matokeo ya maeneo matano ya kipaumbele ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano.

**25.** ***Mheshimiwa Spika,*** Mapendekezo ya Mpango huu ni kiungo kati ya mipango inayokamilika na mipango mipya inayotarajiwa kutekelezwa na Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050. Hivyo, Mapendekezo haya yatajielekeza kwenye Mpango wa mwaka 2025/26 katika kuainisha na kutekeleza afua muhimu ambazo hazikukamilika ili kuandaa mazingira shirikishi na endelevu kwa mipango ijayo kwa kufanya uchambuzi wa kina wa wadau (watakaoshiriki katika kutekeleza mipango ya nchi.

**26.** ***Mheshimiwa Spika***, vigezo vya kuchagua vipaumbele vya Mapendekezo ya Mpango kwa mwaka 2025/26 ni kama ifuatavyo: -

i) **Ukuaji Endelevu wa Uchumi**: Hii inalenga kufikia ukuaji wa uchumi wa juu wenye ustahimilivu zaidi kwa kuongeza tija, mahitaji ya jumla na kulenga uwekezaji wa kimkakati katika sekta muhimu (kilimo, viwanda na huduma);

ii) **Kupunguza Umaskini:** Hii inalenga kuongeza kasi ya ukuaji wa uchumi jumuishi unaozingatia upatikanaji wa huduma za kijamii, programu zinazolenga kinga ya jamii na zenye kutengeneza fursa za kiuchumi;

iii) **Kuzalisha Ajira kwa Wananchi:** Hii inahusisha kuainisha afua zitakazoimarisha ushirikiano kati ya Serikali na Sekta Binafsi zilizopo na zinazoanzishwa ili kutengeneza nafasi za ajira hususan vijana na wanawake;

iv) **Kuimarishwa kwa Ushindani katika Masoko ya Kikanda na Kimataifa**: Hii inajumuisha kuboresha miundombinu, kuweka mazingira wezeshi ya biashara, kufuata taratibu za kimataifa, kuimarisha rasilimali watu, kukuza uwekezaji wa ndani na nje;

v) **Maendeleo Endelevu**: Kuhakikisha matumizi endelevu ya maliasili na kupunguza uharibifu wa mazingira na upotevu wa viumbe hai; na

vi) **Utawala Bora na Utawala wa Sheria**: Hii inajumuisha hatua madhubuti za kupunguza rushwa, kuwezesha upatikanaji wa haki, kuimarisha uwajibikaji, na kulinda haki za binadamu.

**27.** ***Mheshimiwa Spika,*** Vipaumbele vinayopendekezwa katika Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2025/2026 vimezingatia malengo tarajiwa na matokeo ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano. Katika kuhakikisha ufanisi wakati wa utekelezaji, Serikali kwa kushirikiana na Sekta Binafsi itaweka mkazo katika maeneo ya miradi ya kielelezo yenye manufaa na matokeo makubwa na kujielekeza katika vipaumbele kama ifuatavyo:-

i) **Kuchochea Uchumi Shindani na Shirikishi**: *katika eneo hili Serikali itaendelea na* ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya Reli ikiwemo reli ya SGR pamoja na uimarishaji wa huduma za usafiri na usafirishaji wa abiria na mizigo; ujenzi wa miundombinu ya barabara kuu na za mikoa; barabara za kimkakati na za kupunguza foleni; uzalishaji, wa nishati ya umeme kutoka vyanzo mbalimbali na teknolojia ya matumizi ya nishati safi; usambazaji wa umeme kwa vijijini vilivyobakia; utafutaji gesi asilia na ujenzi wa miundombinu ya uchakataji wa gesi; kuimarisha utoaji wa huduma za hali ya hewa; na kuendelea kutekeleza Mkakati wa Kitaifa wa Kuimarisha Upatikanaji wa Fedha za Kigeni.

ii) **Kuimarisha uwezo wa Uzalishaji wa Bidhaa Viwandani na Utoaji Huduma**: *eneo hili linajumuisha uongezaji thamani ya mazao mbalimbali ambapo baadhi ya vipaumbele vinavyopendekezwa ni* utafutaji na uhamasishaji wa uwekezaji wa madini ya kimkakati (strategic mineral resources) yakiwemo madini ya chuma na magadi soda; kutekeleza mikakati ya kulinda viwanda vya ndani ili kuvutia wawekezaji; kuboresha mazingira wezeshi ikiwa ni pamoja na ujenzi wa miundombinu kwenye maeneo ya viwanda (industrial clusters) kwa ajili ya viwanda vidogo na vya kati.

iii) **Kukuza Uwekezaji na Biashara:** *katika eneo hili Serikali,* itaimarisha mifumo kwa ajili ya kuchochea uwekezaji kwa kutunga Sera, Sheria, Kanuni, Mikakati na Miongozo; kuimarisha upatikanaji wa huduma kwa wawekezaji katika ngazi zote; kuboresha mazingira ya biashara ili kuvutia wawekezaji kutoka sekta binafsi; kuimarisha uwekezaji wa kimkakati na kufungamanisha sekta zenye mnasaba na

Uchumi wa Buluu; kuboresha mifumo ya ukusanyaji na usambazaji wa taarifa za biashara na masoko; na kuimarisha diplomasia ya uchumi.

iv) **Kuchochea Maendeleo ya Watu:** Kuimarisha mifumo na usimamizi wa uendeshaji wa elimu, afya, maji na hifadhi ya mazingira ili kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi; kuimarisha na kuhamasisha uwekezaji katika programu za mtindo wa maisha na lishe bora; kujenga na kukarabati miundombinu ya michezo, sanaa na ubunifu; kuongeza kasi ya upangaji, upimaji, umilikishaji na usajili wa ardhi mijini, vijijini na maeneo ya kimkakati; na kuimarisha usalama wa raia na mali zao ili kudumisha amani na utulivu nchini.

v) **Kuendeleza Rasilimali Watu:** kukuza ujuzi kwa vijana, kuwezesha na kuendeleza ujuzi kwa makundi mbalimbali katika ngazi zote za elimu; kuimarisha ujuzi katika majadiliano ya mikataba hususan ya mafuta, gesi na madini, uandishi wa Sheria, utafiti wa sheria na uendeshaji wa mashauri ya madai dhidi ya Serikali ndani na nje ya nchi; na kuwezesha utekelezaji wa Mkakati wa Taifa wa Maendeleo ya Ujuzi wa Mwaka 2016/17 – 2025/26.

**28.** ***Mheshimiwa Spika*****,** Mafanikio ya utekelezaji wa Vipaumbele vya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2025/26 yatajengwa katika misingi ifuatayo:

i) Kuendelea kuwepo kwa amani, usalama na utulivu wa ndani ya nchi na katika nchi jirani;

ii) Kuendelea kudumisha utawala bora na utawala wa sheria nchini;

iii) Kuimarika kwa upatikanaji na usalama wa chakula nchini;

iv) Kuongezeka kwa ushiriki wa sekta binafsi katika shughuli za uwekezaji na biashara;

v) Kuendelea kuhimili athari za mabadiliko ya tabia nchi na majanga ya asili na yasiyo ya asili (ukame, vita, magonjwa ya mlipuko na mafuriko);

vi) Kuwa na nidhamu katika utekelezaji wa mpango na bajeti;

vii) Kutekeleza kikamilifu mfumo wa ufuatiliaji na upimaji unaozingatia viashiria vya matokeo;

viii) Kuimarika kwa uchumi wa dunia na utulivu wa bei katika masoko ya fedha na bidhaa; na

ix) Kuendelea kwa utekelezaji wa miradi ya maendeleo;

**29.** ***Mheshimiwa Spika,*** ninapoitimisha ninawashukuru watumishi wenzangu wakiongozwa **Mheshimiwa Stanslaus Haroon Nyongo**, Mbunge wa Maswa Mashariki - Naibu Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, Dkt. Tausi Kida, Katibu Mkuu, pamoja na Katibu Mtendaji wa Tume ya Mipango, Ndugu Lawrence Mafuru, kwa ushirikiano wanaonipa katika kutekeleza majukumu yetu. Aidha, kwa upekee, ninawashukuru kwa maandalizi mazuri ya nyaraka nilizowasilisha leo katika Bunge lako.

**30.** ***Mheshimiwa Spika***, baada ya maelezo hayo, naomba Kamati yako ipokee na kujadili Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka 2025/26 kwa ajili ya maandalizi ya Mpango na ustawi wa Taifa letu.

**31.** **Mheshimiwa Spika**, ninaomba kutoa hoja.

Prof. Kitila Alexander Mkumbo **(Mb.)**,
**WAZIRI WA NCHI,**
**OFISI YA RAIS – MIPANGO NA UWEKEZAJI.**
**01 Novemba 2024**

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono, ahsante sana Mheshimiwa Waziri.

*(Hapa Waziri wa Fedha alikumbatiana na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji)*

**SPIKA:** Wapiga picha sijui kama wameipata hiyo! Mmefanya haraka sana. Au mrudie?

*(Hapa Waziri wa Fedha - Mhe. Dkt. Mwigulu L. Nchemba alikumbatiana na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji - Mhe. Prof. Kitila A. Mkumbo)*

**SPIKA:** Wapiga picha, haya ahsanteni sana.

Mheshimiwa Waziri ahsante sana kwa wasilisho hilo, sasa Waheshimiwa Wabunge tunakwenda kumsikiliza Waziri wa Fedha ambaye ni Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba Madelu aje awasilishe hoja yake.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu lipokee na kujadili Mapendekezo ya Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2025/2026.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, napenda kutumia fursa hii kumshukuru Mungu kwa kutuwezesha kuwa na afya njema na kuwezesha kukutana hapa kujadili mada hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpongeze kwa dhati Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambaye pia ni Amiri Jeshi Mkuu na Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi kwa uongozi wake mahiri wa kuwatumikia Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, natambua kuwa katika awamu ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Serikali imetekeleza miradi ya kimkakati kwa ufanisi wa juu sana kama ambavyo Waziri wa Mpango ametoka kuanisha hapa. Imewekeza kwenye sekta za uzalishaji na kukuza ajira na kipato cha Watanzania, imekuza

uwekezaji na kuboresha mazingira ya biashara na imejenga miundombinu na kuboresha huduma za jamii kama ilivyoainishwa katika Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2020.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, napenda kumpongeza Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa busara na hekima na weledi katika kazi zake za kumsaidia Mheshimiwa Rais. Kadhalika nampongeza Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Mbunge wa Jimbo la Ruangwa na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi wake shupavu kama kiongozi wa shughuli za Serikali Bungeni kwa uongozi wake mahiri na kumsaidia Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze pia Mheshimiwa Dkt. Doto Mashaka Biteko, Mbunge wa Jimbo la Bukombe, Naibu Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Waziri wa Nishati kwa kuendelea kumsaidia Mheshimiwa Waziri Mkuu katika utekelezaji wa majukumu yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie fursa hii pia kumpongeza Katibu Mkuu wa CCM Mheshimiwa Balozi Dkt. Emmanuel Nchimbi na Sekretarieti yake ya CCM Taifa, mikoa pamoja na Wilaya kwa ufuatiliaji mzuri wa utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM. Kipekee nivipongeze vyombo vya ulinzi na usalama kwa shughuli zao wanazofanya vikiongozwa na Jenerali Jacobo Mkunda, Mkuu wa Majeshi ya ulinzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kadhalika nimpongeze Jaji Mkuu, Prof. Ibrahim Juma na mhimili mzima wa Mahakama kwa kazi nzuri wanazozifanya. Ulinzi na usalama, haki na sheria ni nguzo muhimu sana za maendeleo katika nchi yoyote duniani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie fursa hii kukupongeza wewe binafsi pamoja na Naibu Spika kwa kuendelea kuliongoza Bunge letu kwa umahiri mkubwa mkisaidiwa na Wenyeviti wa Bunge kwa kuzingatia sheria na kanuni zilizopo hapa Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nawapongeza Waheshimiwa Wabunge wote kwa kuendelea kutekeleza ipasavyo wajibu wao wa kikatiba wa kutunga sheria pamoja na

kuisimamia Serikali. Niwahakikishie Watanzania kwamba wana Wabunge bora sana wa majimbo yote na mikoa yote, wana Wabunge makini sana wanaotimiza wajibu wao ipasavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda niishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge inayoongozwa na Mwenyekiti Mheshimiwa Oran Njeza, Mbunge wa Mbeya Vijijini pamoja na Makamu Mwenyekiti Mheshimiwa Twaha Mpembenwe, Mbunge wa Kibiti pamoja wa Wajumbe wote wa Kamati kwa miongozo yao wanayotupatia tunapohudhuria kwenye Kamati yetu ya Bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutumia fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Faustine Engelbert Ndungulile, Mbunge wa Jimbo la Kigamboni, Dar es Salaam, kwa kuchaguliwa kuwa Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Afya Duniani, Kanda ya Afrika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kadhalika, napenda kuchukua fursa hii kumpongeza Mtanzania mwenzetu, Dkt. Zarau Wendelini Kibwe, kwa kuchaguliwa na Benki ya Dunia kuwa Mkurugenzi Mtendaji wa benki hiyo, Kanda namba moja ya Afrika yenye nchi 22. Hii inatokea baada ya zaidi ya miaka 50 tokea Tanzania kupata fursa tena, na ni matokeo ya diplomasia ya uchumi ambayo Mheshimiwa Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan kuikuza kwa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutumia fursa hii pia kutoa shukrani za dhati kwa Naibu Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Hamad Hassan Chande, Mbunge, na Watendaji wote wa Wizara wakiongozwa na Katibu Mkuu, Dkt. Natu El-Maamry Mwamba kwa ushirikiano walionipa katika kutekeleza majukumu haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2025/2026 ni wa mwisho katika utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 pamoja na Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2021/2022 – 2025/2026). Maandalizi ya Mwongozo yamezingatia yafuatayo: Mpango wa Taifa wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/2022 – 2025/2026,

Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2020, Makubaliano ya Paris kuhusu Mabadiliko ya Tabianchi, Agenda 2063 ya Maendeleo ya Afrika, Malengo ya Maendeleo Endelevu 2030, na makubaliano mbalimbali ya kikanda (*EAC* na *SADC*) pamoja na maelekezo mahususi ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapendekezo haya yanaakisi juhudi ambazo Serikali ya awamu ya sita imeendelea kuchukua katika kuboresha maisha ya Watanzania kwa kuboresha mazingira ya uwekezaji na kuongeza ushiriki wa sekta binafsi kwenye shughuli za uzalishaji pamoja na biashara, kutoa fursa za ajira, kuimarisha utoshelevu wa chakula nchini, kuimarisha upatikanaji wa huduma za jamii na kuimarisha uhusiano na ushirikiano wa kikanda na kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2025/2026, unajumuisha mwenendo na mwelekeo wa hali ya uchumi, vipaumbele vya mpango na bajeti kwa mwaka 2025/2026, usimamizi wa vihatarishi na utekelezaji wa mpango na bajeti, mapitio ya utekelezaji wa mpango na bajeti kwa mwaka 2023/2024, mapitio ya utekelezaji wa Mwongozo wa Mpango na Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2024/2025 na maelekezo mahususi yanayotakiwa kuzingatiwa na Maafisa Masuuli wakati wa uandaaji, utekelezaji, ufuatiliaji na tathmini ya mpango na bajeti kwa mwaka 2025/2026. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu viashiria vya Uchumi, shughuli za uchumi zimeendelea kuimarika kama ambavyo taarifa imetolewa hivi punde na Mheshimiwa Waziri wa Mipango na Uwekezaji. Mfumuko wa bei umeendelea kuwa 3.2% kwa mwaka 2023/2024 kiwango ambacho kipo ndani ya lengo la kati ya asilimia tatu hadi tano, ambacho kimekubalika Ukanda wa Afrika Mashariki na Ukanda wa *SADC*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2023/2024, dola moja ya Marekani ilibadilishwa kwa wastani wa shilingi 2,519.91 sawa na upungufu wa thamani ya shilingi kwa 8.5% ikilinganishwa na 2022/2023. Upungufu huo ulitokana na changamoto mbalimbali

ikiwemo athari za kubana fedha katika nchi zilizoendelea pamoja na ongezeko la bei katika bidhaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, akiba ya fedha za kigeni imeendelea kuwa ya kutosha ambapo hadi kufikia Juni, 2024, akiba ilikuwa ya dola za Marekani milioni 5,345.5 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 5,446.1 kwa mwezi Juni 2023. Kiasi hicho kilitosha akiba kwa takribani miezi minne ya uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje ya nchi kama ambavyo inakubalika kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, akiba ya dhahabu *(monetary gold)* ya Benki Kuu ya Tanzania imefikia kilo 976.51, yenye thamani ya Dola za Marekani milioni 89.96 kama ambavyo tulitoa taarifa wakati tunaanza utaratibu huu katika mwaka huu wa fedha. Kiasi hicho cha dhahabu na fedha ni sawa na 16.3% ya lengo la kukusanya kilo 6,000 kwa mwaka 2024/2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, akiba ya chakula kwa sasa katika ghala la Taifa kwa Hifadhi ya *NFRA* ni *metric tonnes* 826,000. Uzalishaji wa chakula umefika tani milioni 22, sawa na 128% ambapo lengo la nchi ni kufika tani 130 mwaka 2025/2026. Hii haijapata kutokea, hii ni mpya. Akiba ya chakula, akiba ya dhahabu, na akiba ya fedha za kigeni, hii haijawahi kutokea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, riba ya dhamana za Serikali iliongezeka hadi wastani wa 9.14% kwa mwaka 2023/2024 kutoka 5.73% mwaka 2022/2023. Mikopo kwa sekta binafsi iliongezeka kwa 17.2% na kufikia shilingi bilioni 34,980.85 kwa Taarifa ya Juni, 2024 kutoka shilingi bilioni 29,835.56 kwa Juni, 2023.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia Juni, 2024, deni la Serikali lilikuwa shilingi bilioni 96,884.18 ambapo deni la nje lilikuwa shilingi bilioni 64,932.94 na deni la ndani lilikuwa shilingi bilioni 31,951.24. Tathmini ya uhimilivu wa deni iliyofanyika Juni, 2024 imeonesha kuwa deni hili ni himilivu na viashiria vya deni la Serikali viko ndani ya wigo unaokubalika kimataifa katika kipindi cha muda wa kati na mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2023/2024, Kampuni za *Fitch Ratings* na *Moody's Investors Service* zilifanya mapitio ya tathmini ya nchi kukopesheka katika masoko ya mitaji ya kimataifa na kuchapisha matokeo ya daraja B1 na B+ mtawalia. Matokeo haya yalitokana na ukuaji mzuri wa kiuchumi. Hivi ndivyo wenzetu magwiji wa kuangalia chumi za nchi wanavyotuona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa *Moody's Rating,* waliweka matokeo kwamba, Tanzania sasa ni miongoni mwa nchi tano bora kiuchumi kati ya nchi 25 kusini mwa Jangwa la Sahara zinazotathminiwa na Moody's, ikifuata Botswana ambayo ilikuwa na A3, Mauritius iliyokuwa na Baa3, Cote d'Ivoire iliyokuwa na Ba2, Afrika Kusini Ba2 na Tanzania ikiwemo, ambazo ni nchi tano zenye uchumi imara Kusini mwa Jangwa la Sahara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Afrika Mashariki, Tanzania iko juu ya nchi zote, ambapo nchi nyingine zinazofuatia, zinaifuatia Kenya yenye B3, Rwanda yenye B2, Uganda yenye B2 pamoja na nyinginezo. Nchi nyingine zinazoshika daraja la B1 kama Tanzania kwa mujibu wa Moody's ni Namibia, Benin, na Senegal, nchi tatu ambako na Tanzania iko; zenye uchumi imara kwa tathmini ya vigezo vya makampuni haya magwiji ya kuangalia tathmini za chumi kwa mwenendo wa sasa na ujao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa *Fitch Ratings*, nchi za Afrika zinazoshikilia daraja kama Tanzania ni Rwanda na Benin. Iko kwenye kundi la nchi mbili ambazo uchumi wake umewekwa juu B+ imara. Aidha, kwa Nchi za Afrika Mashariki, nchi zilizo kundi la Tanzania, ni Tanzania na Rwanda na nyingine zikifuatia. *Fitch Ratings* imetoa daraja B+ kwa nchi za *SADC* ikiwa inamaanisha Tanzania pekee na nchi nyingine zinafuatia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Moodys *Ratings,* Daraja la B1 kwa Afrika Mashariki ipo Tanzania pekee. Unaweza ukaona jinsi ambavyo Tanzania uchumi wake unaonekana na matokeo haya mazuri yanakuja kufuatia jitihada za Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ikiwemo ukuaji wa uchumi stahimilivu; Tanzania imeonesha uwezo wake wa kiuchumi kuhimili majanga mbalimbali, ambapo wakati wa *Covid* ilionesha vile

pamoja na majanga mengine yaliyofuatia ikiwemo mzozo wa kisiasa kati ya Urusi na Ukraine pamoja na matatizo mengine ya uchumi huko duniani. Mageuzi ya kimuundo na yenyewe yamechangia kuimarika kwa mageuzi ya kimuundo na kuboresha utendaji wa taasisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais wetu haongei sana, lakini ameimarisha sana taasisi zinazofanya kazi ya kusimamia masuala ya kuichumi, masuala ya kiutawala na masuala mengine kama taratibu za kisasa za uendeshaji wa nchi zinavyotaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu nidhamu ya mapato na usimamizi wa fedha za umma, Tanzania imekuwa kinara wa ukusanyaji wa mapato pamoja na usimamizi wa mapato hayo, jambo lililoruhusu utekelezaji wa miradi mikubwa ya kimkakati. Hii ni miradi ya mfano kwa nchi zinazoendelea kuweza kutekeleza miradi kama ambavyo Mheshimiwa Waziri wa Mipango ametoka kuelezea. Reli itakapokamilika itakuwa ni moja ya reli ndefu zaidi kwa Afrika na itakuwa moja ya reli tano ndefu zaidi duniani. Hivyo hivyo, kukamilika kwa daraja pamoja na miradi mingine ni ishara ya usimamizi wa fedha za umma na kutumia fedha za umma katika masuala yaliyokusudiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwenendo wa viashiria vya uchumi yanapatikana katika Kiambatisho cha kwanza A cha Mwongozo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Mwaka 2023/2024, Serikali ilikadiria kukusanya na kutumia shilingi bilioni 44,338.07, na katika kipindi hicho, shilingi bilioni 42,920.62 sawa na asilimia 96.7 ya bajeti iliyoidhinishwa kilikusanywa. Kiasi hiki kinajumuisha shilingi bilioni 29,829.89 ya mapato ya ndani, ambayo ni sawa na 95.1% ya lengo la mwaka la shilingi bilioni 31,381.01; shilingi bilioni 5,581.61, ikiwa ni misaada na mikopo nafuu kutoka kwa washirika wa maendeleo na hii ikiwa ni 102.1% ya lengo na shilingi bilioni 7,509.11 ni mikopo ya kibiashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi hicho, Serikali imetumia shilingi bilioni 42,945.21. Kwa upande wa mafanikio, ni

kama ambavyo tumetoka kubainishiwa na Mheshimiwa Waziri wa Mipango na Uwekezaji na kwenye kitabu chetu tumeweka kwenye kiambatanisho namba 1C cha Mwongozo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2025, misingi na shabaha, pamoja na viashiria vya kiuchumi ni kama ifuatavyo:

(i) Kuimarika kwa uchumi wa dunia na utulivu wa bei katika masoko ya fedha na bidhaa;

(ii) Kuongezeka kwa ushiriki wa sekta binafsi katika uwekezaji na biashara;

(iii) Kuendelea kuhimili athari za mabadiliko ya tabianchi;

(iv) Kuimarika kwa upatikanaji na usalama wa chakula nchini; na

(v) Kuendelea kuwepo kwa amani, usalama na utulivu wa ndani ya nchi na katika nchi jirani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na uchambuzi na maoteo yaliyofanyika, shabaha na malengo ya uchumi jumla yatakayozingatiwa ni pamoja na haya yafuatayo:

(i) Pato halisi la Taifa linakadiriwa kukua kwa 5.8% kwa mwaka 2025. Ikiwa ni kuongezeka hadi 6.1% kwa Mwaka 2026;

(ii) Mfumuko wa bei unatarajiwa kuendelea kuwa katika wigo wa tarakimu moja ambayo ni ndani ya asilimia kati ya tatu hadi tano kama ambavyo imekubalika katika ukanda;

(iii) Mapato ya ndani kufikia 16.1% ya pato la kodi na 13.0% ya Pato la Taifa kwa mwaka 2025/2026;

(iv) Kuwa na nakisi ya bajeti isiyozidi asilimia tatu ya pato la Taifa; na

(v) Kuwa na akiba ya fedha za kigeni kwa kiwango kinachokidhi mahitaji ya uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje kwa kipindi kisichopungua miezi minne.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa vipaumbele ambavyo vimezingatiwa na maeneo mahususi yatakayopewa kipaumbele cha bajeti ya mwaka 2025/2026, ni pamoja na haya. Undani zaidi ipo kwenye kitabu:-

(i) Uendelezaji wa miundombinu;

(ii) Uimarishaji wa sekta za uzalishaji na huduma za jamii;

(iii) Usimamizi wa mazingira na mabadiliko ya tabianchi;

(iv) Kuboresha usimamizi na mifumo ya kitaasisi ili kuimarisha utawala bora;

(v) Kukuza usawa wa kijinsia na uwezeshaji wa makundi maalum; na

(vi) Kugharamia maandalizi ya uchaguzi mkuu wa Mwaka 2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwaka 2025/2026, Serikali inakadiria kukusanya mapato kutoka kwenye vyanzo vyake vyote jumla ya shilingi bilioni 55,061.61. Kati ya kiasi hicho, mapato ya ndani ni shilingi bilioni 38,962.49 ikilinganishwa na maoteo ya shilingi bilioni 34,610.65 mwaka 2024/2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nirudie. Kwa mwaka 2025/2026, Serikali inakadiria kukusanya mapato kutoka kwenye vyanzo vyake vyote jumla ya shilingi bilioni 55,061.61. Kati ya kiasi hicho, mapato ya ndani ni shilingi bilioni 38,962.49 ikilinganishwa na maoteo ya shilingi bilioni 34,610.65 mwaka 2024/2025. Ongezeko hilo limezingatia misingi ya uchumi jumla, mikakati na hatua zinazoendelea zinazochukuliwa na Serikali na kuimarisha ukusanyaji wa mapato ikiwemo kuhimiza matumizi ya mifumo ya TEHAMA, kudhibiti utoaji wa misamaha ya kodi, na kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji zitakazowezesha uibuaji wa vyanzo vipya vya mapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, dhamira ya Serikali ni kuhakikisha kuwa mapato ya ndani yanaendelea kugharamia kiasi kikubwa zaidi cha bajeti ya Serikali kisichopungua 70% ya bajeti yote. Hivyo, Serikali kupitia Mamlaka ya Mapato Tanzania na taasisi nyingine za Serikali itaendelea kutekeleza mkakati wa muda wa kati wa ukusanyaji wa mapato wenye lengo la kuongeza mapato ya ndani na kupunguza utegemezi wa mikopo na misaada katika bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, misaada kutoka kwa washirika wa maendeleo inakadiriwa kuwa shilingi bilioni 1,024.88, mikopo nafuu kutoka kwa washirika wa maendeleo inatarajiwa kuwa shilingi bilioni 5,667.04 na mikopo ya kibiashara kutoka vyanzo vya ndani na nje shilingi bilioni 9,407.20.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matumizi ya Serikali yanatarajiwa kufikia shilingi bilioni 55,061.61 kwa mwaka 2025/2026. Kati ya kiasi hicho, matumizi ya kawaida ni shilingi bilioni 38,602.18 na matumizi ya maendeleo shilingi bilioni 16,459.43. Aidha, makadirio ya mapato na matumizi ya Serikali kwa mwaka 2025/2026 yameainishwa katika Sehemu ya Pili ya Mwongozo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa maelekezo mahususi ya Mwongozo, baadhi ya maelekezo hayo ni kuzingatia ukamilishaji wa miradi inayoendelea kabla ya kuibua miradi mipya sambamba na kulipa madeni ya miradi inayoendelea kama Bunge lilivyoshauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maelekezo mengine mahususi niKuhakikisha kuwa mapato yote yanayokusanywa yanaingizwa Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali kwa mujibu wa matakwa ya Kifungu 58 (a) cha Sheria ya Bajeti, Sura 439 isipokuwa pale ilipoelekezwa vinginevyo kwa mujibu wa sheria husika; kuhakikisha matumizi sahihi ya mifumo ya kielektroniki; kutekeleza Mwongozo wa Utaratibu wa Maombi na Utoaji wa Fedha wa Mwaka 2021; kuzingatia matakwa ya Sheria ya Ununuzi wa Umma, Sura 410; kutoingia mikataba na wazabuni bila kuzingatia sheria, taratibu na miongozo iliyopo; kutekeleza Mkakati wa Taifa wa Kuimarisha Upatikanaji wa Fedha za Kigeni ikiwemo: kudhibiti matumizi yasiyo ya lazima ya fedha za kigeni; kuendelea kufuatilia kwa karibu

utendaji wa mashirika ya umma hususan yale yanayojiendesha; ushirikishaji wa sekta husika katika utekelezaji wa miradi inayohusisha sekta zaidi ya moja kabla; na kuzingatia masuala ya mazingira na mabadiliko ya tabianchi pamoja na masuala ya jamii katika upangaji na utekelezaji wa bajeti za maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maelekezo mahususi ya mwongozo yanapatikana katika Sehemu ya Nne ya Mwongozo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuhitimisha, naomba kuridhiwa kwa Mapendekezo ya Mwongozo kutakaowezesha kukamilika kwa maandalizi ya bajeti za mafungu kwa wakati; kuimarika kwa usimamizi wa matumizi ya fedha za umma; kuimarika kwa ukusanyaji wa mapato ya ndani; kuimarika kwa kushirikishwa kwa wadau mbalimbali ikiwemo sekta binafsi katika uandaaji, utekelezaji pamoja na ufuatiliaji na tathmini ya bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie fursa hii kuwapongeza wananchi waliojitokeza kwa wingi kujiandikisha kushiriki Uchaguzi wa Serikali za Mitaa unaopangwa kufanyika Novemba, 2024, chini ya uratibu mzuri wa Mheshimiwa Mohamed Omary Mchengerwa, Mbunge wa Bunge la Rufiji, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) pamoja na timu yake yote. Niseme tu, wananchi wameupiga mwingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, nawashawishi wananchi wenzangu kama tulivyojiandikisha tujitokeze kwa wingi pia siku hiyo ya uchaguzi ili kuwapigia kura viongozi wetu watakaotuongoza kwa kipindi cha miaka mitano ijayo katika ngazi za mitaa, vijiji pamoja na vitongoji. Pia ninawasisitiza wananchi wenzangu kuchagua viongozi wenye maono, uadilifu na uwezo mzuri wa kusimamia vizuri maendeleo na ustawi wa jamii zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuwashukuru na kuendelea kuwaomba Waheshimiwa Wabunge, Waandishi wa Habari, Viongozi wa Dini, Viongozi wa Kimila, Taasisi za Kiraia, Wasanii, Vyama vya Siasa na wadau wengine kuendelea na jitihada za uelimisha na uhasishaji wa wananchi kuhusu umuhimu wa kushiriki katika uchaguzi hususan uchaguzi wa Serikali za Mitaa

wenye kauli mbiu isemayo, "Serikali za Mitaa, Sauti ya Wananchi, Jitokeze Kushiriki Uchaguzi."

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, ninawahimiza wananchi wote wenye vigezo na sifa za kugombea nafasi mbalimbali waendelee kujitokeza kugombea nafasi hizo. Hivyo ninawatakia uchaguzi mwema, wenye amani na utulivu katika kipindi chote kuanzia uteuzi wa wagombea, kampeni, upigaji wa kura, wakati wa kutangaza na kupokea matokeo ya uchaguzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho lakini siyo kwa umuhimu, leo Simba *Sports Club* wanacheza, tuwaombee washinde. Simba wasiposhinda, wazee wanakosa raha, hata humu Bungeni wazee wapo. Wazee wakikosa raha, wanaacha kutushauri. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo, naomba sasa Bunge lako Tukufu lipokee na kujadili Mapendekezo ya Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2025/2026.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

## HOTUBA YA WAZIRI WA FEDHA, MHE. MWIGULU LAMECK NCHEMBA MADELU (MB) AKIWASILISHA BUNGENI MAPENDEKEZO YA MWONGOZO WA MAANDALIZI YA MPANGO WA BAJETI YA SERIKALI KWA MWAKA 2025/2026 - KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

### 1.0 UTANGULIZI

**1.** ***Mheshimiwa Spika***, naomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako Tukufu lipokee na kujadili mapendekezo ya Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2025/26.

**2.** ***Mheshimiwa Spika***, awali ya yote, napenda kutumia fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia afya njema na kutuwezesha kukutana tena hapa ili kupokea na kujadili Mapendekezo ya Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2025/26.

**3.** ***Mheshimiwa Spika***, naomba nimpongeze kwa dhati **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan**, **Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**, ambaye pia ni Amiri Jeshi Mkuu na Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), kwa uongozi wake mahiri wa kuwatumikia watanzania. **Natambua katika awamu yake Mheshimiwa Dr Samia Suluhu Hassan, Serikali Imetekeleza Miradi ya kimkakati kwa ufanisi wa juu, Imewekeza kwenye Sekta za uzalishaji na kukuza ajira na kipato kwa mtanzania, Imekuza uwekezaji na kuboresha mazingira ya kibiashara, Imejenga miundombinu, imeboresha huduma za jamii kama ilivyoainishwa katika Ilani ya CCM ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020.** Vilevile, napenda kumpongeza **Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango**, **Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**, kwa busara, hekima na weledi katika kazi zake za kumsaidia na kumshauri Mheshimiwa Rais kuongoza Taifa letu.

**4.** ***Mheshimiwa Spika,*** kadhalika, nampongeza **Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa Mbunge wa jimbo la Ruangwa - Lindi**, **Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania** na Kiongozi wa shughuli za Serikali bungeni, kwa uongozi wake mahiri na kumsaidia Mheshimiwa Rais kufuatilia utekelezaji wa mpango na bajeti ya Serikali. Nitumie fursa hii pia kumpongeza **Mheshimiwa Dkt. Dotto Mashaka Biteko, Mbunge wa jimbo la Bukombe - Geita**, **Naibu Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Waziri wa Nishati** kwa kuendelea kumsaidia Mhe. Waziri Mkuu katika utekelezaji wa majukumu yake.

**5.** ***Mheshimiwa Spika***, nitumie fursa hii pia kumpongeza Katibu Mkuu wa CCM, Balozi Dkt. Emmanuel Nchimbi na Sekretarieti yake ya CCM Taifa, Mikoa na Wilaya kwa ufuatiliaji mzuri sana wa utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM. Kipekee nivipongeze Vyombo vyote vya Ulinzi na Usalama vikiongozwa na Generali Jacob Mkunda Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi. Kadhalika nimpongeze Jaji Mkuu Profesa Ibrahim Juma na Mhimili wote wa Mahakama kwa kazi nzuri wanazozifanya hapa nchini. Ulinzi na Usalama na Haki na Sheria ni nguzo mhimu sana ya Maendeleo katika Nchi yeyote Duniani.

**6.** ***Mheshimiwa Spika***, nitumie fursa hii pia kukupongeza wewe binafsi, pamoja na Naibu Spika kwa kuendelea kuliongoza Bunge

letu kwa umahiri na kwa kuzingatia sheria na kanuni zinazoliongoza Bunge hili. Vilevile, ninawapongeza waheshimiwa wabunge wote kwa kuendelea kutekeleza ipasavyo wajibu wao wa kikatiba wa kutunga sheria pamoja na kuisimamia Serikali. **Niwahakikishie watanzania wa majimbo yote na Mikoa yote, mna wabunge Makini sana wanaotimiza wajibu wao ipasavyo.**

**7.** ***Mheshimiwa Spika***, napenda kuishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti chini ya **Mwenyekiti** wake **Mheshimiwa Oran Manase Njeza, Mbunge wa Mbeya Vijijini** na **Mheshimiwa Twaha Ally Mpembenwe, Mbunge wa Kibiti, Makamu Mwenyekiti** kwa maoni na ushauri wakati wa vikao vya Kamati. Maoni na ushauri wa Kamati umezingatiwa katika kuboresha Mapendekezo ya Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2025/26 ninayowasilisha katika Bunge hili leo.

**8.** ***Mheshimiwa Spika***, ningependa kutumia fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Faustine Engelbert Ndungulile **Mbunge wa jimbo la Kigamboni – Dar es Salaam**, kwa kuteuliwa kuwa Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Afya Duniani – Kanda ya Afrika. Hii ni fahari na heshima kubwa kwa nchi yetu kwani inaonesha ukuaji wa diplomasia na kielelezo cha imani kubwa ambayo mataifa mengi duniani wanayo juu ya nchi yetu. Napenda pia kuchukua fursa hii kumpongeza mtanzania mwenzetu **Dkt. Zarau Wendelini Kibwe** kwa kuchaguliwa na **Benki ya Dunia kuwa Mkurugenzi Mtendaji** wa benki hiyo kanda Na. 1 ya Afrika yenye nchi 22. Hii inatokea baada ya zaidi ya miaka 50 kwa Tanzania kunapata tena fursa na ni matokeo ya diplomasia ya uchumi ambayo Mhe. Rais wetu amekuwa anaipigania na kuikuza.

**9.** ***Mheshimiwa Spika***, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa **Naibu Waziri wa Fedha**, **Mheshimiwa Hamad Hassan Chande (Mb),** na watendaji wote wa Wizara ya Fedha wakiongozwa na **Katibu Mkuu**, **Dkt. Natu El-maamry Mwamba** kwa ushirikiano walionipa katika utekelezaji wa majukumu yangu ikiwemo maandalizi ya mapendekezo ya Mwongozo huu. Aidha, ninawashukuru sana Wizara, Idara Zinazojitegemea, Wakala wa Serikali, Ofisi za Wakuu wa Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Washirika wa Maendeleo na wadau wengine kwa maoni na

michango yao katika kukamilisha Mapendekezo ya Mwongozo huu.

**10.** ***Mheshimiwa Spika***, Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2025/26 ni wa mwisho katika utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 pamoja na Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/22 – 2025/26. Maandalizi ya Mwongozo yamezingatia yafuatayo: Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/22 – 2025/26, Ilani ya CCM ya Uchaguzi wa Mwaka 2020, Makubaliano ya Paris kuhusu Mabadiliko ya Tabianchi, Agenda 2063 ya Maendeleo ya Afrika, Malengo ya Maendeleo Endelevu 2030, makubaliano mbalimbali ya kikanda (EAC na SADC) na maelekezo mahsusi ya Serikali.

**11.** ***Mheshimiwa Spika***, mapendekezo haya yanaakisi juhudi ambazo Serikali ya awamu ya sita imeendelea kuchukua katika kuboresha maisha ya Watanzania kwa: kuboresha mazingira ya uwekezaji na kuongeza ushiriki wa sekta binafsi kwenye shughuli za uwekezaji na biashara; kutoa fursa za ajira; kuimarisha utoshelevu wa chakula nchini; kuimarisha upatikanaji wa huduma za jamii kwa wote; kuimarisha uhusiano na ushirikiano wa kikanda na kimataifa; kuweka msukumo katika kuimarisha sekta za uzalishaji; pamoja na kudumisha amani, usalama, utawala bora, umoja na utulivu nchini. Mapendekezo yanayowasilishwa yameainisha masuala muhimu ya kuzingatiwa na Maafisa Masuuli wakati wa kuandaa, kutekeleza, kufuatilia, kutathmini na kutoa taarifa za utekelezaji wa mipango na bajeti za mafungu yao ili kufikia malengo yalikusudiwa.

**12.** ***Mheshimiwa Spika***, Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2025/26 unajumuisha mwenendo na mwelekeo wa hali ya uchumi; vipaumbele vya mpango na bajeti kwa mwaka 2025/26; usimamizi wa vihatarishi vya utekelezaji wa mpango na bajeti; mapitio ya utekelezaji wa mpango na bajeti kwa mwaka 2023/24; mapitio ya utekelezaji wa Mwongozo wa Mpango na Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2024/25; na maelekezo mahsusi yanayotakiwa kuzingatiwa na Maafisa Masuuli wakati wa uandaaji, utekelezaji, ufuatiliaji na tathmini ya mpango na bajeti kwa mwaka 2025/26.

## 2.0 MWENENDO WA VIASHIRIA VYA UCHUMI

**13.** ***Mheshimiwa Spika***, shughuli za uchumi zimeendelea kuimarika licha ya kukabiliana na changamoto zilizotokana na utekelezaji wa sera ya fedha ya kupunguza ukwasi katika nchi zilizoendelea, migogoro ya kikanda na kimataifa, kuongezeka kwa bei za bidhaa za petroli, gharama kubwa za mikopo na mabadiliko ya tabianchi. Pamoja na changamoto hizo, Pato halisi la Taifa lilikua kwa wastani wa asilimia 5.1 mwaka 2023 ikilinganishwa na asilimia 4.7 mwaka 2022. Ukuaji huo ulichangiwa kwa kiasi kikubwa na shughuli za kilimo, ujenzi na uchimbaji madini.

**14.** ***Mheshimiwa Spika***, viashiria vya uchumi kwa nusu ya kwanza ya mwaka 2024 vinaonesha uchumi kuendelea kuimarika kutokana na jitihada zinazoendelea kuchukuliwa na Serikali ya awamu ya sita za kuboresha mazingira ya uwekezaji na biashara na kuimarisha sekta za uzalishaji na huduma za jamii. Kufuatia jitihada hizo, Pato halisi la Taifa kwa kipindi cha Januari hadi Juni 2024 lilikua kwa wastani wa asilimia 5.4 ikilinganishwa na asilimia 4.8 katika kipindi kama hicho mwaka 2023. Pato la Taifa linatarajiwa kukua kwa wastani wa asilimia 5.8 mwaka 2025 na asilimia 6.1 mwaka 2026. Ukuaji huu utategemea utekelezaji endelevu wa miradi ya kimkakati inayohusisha miundombinu ya nishati na usafirishaji, kuongezeka kwa mikopo kwa sekta binafsi, jitihada za Serikali katika kuboresha mazingira ya uwekezaji na biashara, utekelezaji wa Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo Awamu ya Pili – ASDP II, utekelezaji wa mapendekezo na Mkakati wa Tume ya Haki Jinai, uwepo wa utawala bora pamoja na uwekezaji wa Serikali katika sekta za huduma za jamii.

**15.** ***Mheshimiwa Spika***, mfumuko wa bei ulikuwa asilimia 3.2 mwaka 2023/24, kiwango ambacho kipo ndani ya lengo la nchi la kati ya asilimia 3 hadi asilimia 5 na sawia na malengo ya mtangamano wa kiuchumi kikanda (EAC na SADC). Aidha, kiwango hicho kilikuwa chini ya asilimia 4.7 ya mwaka 2022/23. Kupungua huko kulitokana na utekelezaji wa sera madhubuti za fedha na bajeti, kuimarika kwa bei za baadhi ya bidhaa muhimu zinazoagizwa kutoka nje ya nchi, na utoshelevu wa chakula nchini. Mfumuko wa bei nchini unatarajiwa kubaki ndani ya lengo

la nchi la asilimia 3 hadi 5, ukichangiwa na matarajio ya upatikanaji wa chakula cha kutosha nchini, kuimarika kwa upatikanaji wa umeme, utulivu wa bei za bidhaa katika soko la dunia na utekelezaji wa sera madhubuti za fedha na bajeti.

**16.** ***Mheshimiwa Spika***, sekta ya nje iliimarika ikichagizwa na kuendelea kuimarika kwa uchumi wa dunia. Nakisi ya urari wa malipo ya nje ilipungua kwa asilimia 50.2 na kufikia dola za Marekani milioni 2,469.5 mwaka 2023/24 kutoka dola za Marekani milioni 4,955.6 mwaka 2022/23. Thamani ya mauzo ya bidhaa na huduma nje ya nchi iliongezeka kwa asilimia 14.7 na kufikia dola za Marekani milioni 14,663.9, ikichangiwa zaidi na mauzo ya dhahabu na bidhaa asilia pamoja na mapato ya utalii. Thamani ya bidhaa na huduma zilizoagizwa kutoka nje ya nchi ilipungua kwa asilimia 5.6 na kufikia dola za Marekani milioni 16,027.0.

**17.** ***Mheshimiwa Spika***, mwaka 2023/24, dola moja ya Marekani ilibadilishwa kwa wastani wa shilingi 2,519.91, sawa na upungufu wa thamani ya shilingi wa asilimia 8.5 ikilinganishwa na mwaka 2022/23. Upungufu huo ulitokana na changamoto mbalimbali ikiwemo athari za kubana sera za fedha katika nchi zilizoendelea pamoja na ongezeko la bei za bidhaa katika soko la dunia hususan bidhaa za petroli, hali iliyosababisha kuongezeka kwa mahitaji ya fedha za kigeni katika uchumi.

**18.** ***Mheshimiwa Spika,*** hata hivyo, akiba ya fedha za kigeni imeendelea kuwa ya kutosha ambapo hadi kufikia Juni 2024, akiba ilikuwa dola za Marekani milioni 5,345.5 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 5,446.1 kwa mwezi Juni 2023. Kiasi hicho kilitosheleza uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje ya nchi kwa kipindi cha takriban miezi 4. Akiba ya Dhahabu fedha (monetary gold) ya Benki Kuu ya Tanzania imefikia kilo 976.51, yenye thamani ya dola za marekani milioni 89.96. Kiasi hicho cha dhahabu fedha ni sawa na asilimia 16.3 ya lengo la kukusanya kilo 6000 kwa mwaka 2024/25. Akiba ya chakula kwa sasa katika ghala la Taifa kwa hifadhi ya NFRA ni 826,000 *metric tonnes*, Uzalishaji wa chakula umefika tani milioni 22, sawa na asilimia 128% ambapo lengo la nchi ni kufika tani 130 mwaka 2025/26. ***Hii ni Serikali inayotenda inachokisema. Mheshimiwa Spika, HII NI MPYA, HII HAIJAWAHI KUTOKEA.***

**19.** ***Mheshimiwa Spika***, riba za dhamana za Serikali ziliongezeka hadi wastani wa asilimia 9.14 mwaka 2023/24 kutoka asilimia 5.73 mwaka 2022/23. Hali hii ilitokana na kupungua kwa ukwasi katika masoko ya fedha, kama ilivyokuwa katika nchi nyingine kufuatia benki kuu duniani kutekeleza sera ya fedha yenye lengo la kukabiliana na ongezeko la mfumuko wa bei. Riba za mikopo zilipungua hadi wastani wa asilimia 15.47 mwaka 2023/24 kutoka asilimia 16.04 mwaka 2022/23. Riba za amana ziliongezeka hadi asilimia 7.32 kutoka asilimia 7.16 mwaka 2022/23. Serikali itaendelea kuchukua hatua za kiutawala na kisera bila kuathiri nguvu ya soko ili kuhakikisha kuwa riba za mabenki zinavutia wananchi kuweka fedha zao benki na wakati huo huo kuvutia ukopaji wa sekta binafsi ili kuchachua shughuli za kiuchumi na kuimarisha sekta ya fedha.

**20.** ***Mheshimiwa Spika***, mikopo kwa sekta binafsi iliongezeka kwa asilimia 17.2 na kufikia shilingi bilioni 34,980.85 Juni 2024 kutoka shilingi bilioni 29,835.56 Juni 2023. Ongezeko hilo limetokana na jitihada za Serikali kuboresha mazingira ya kufanya biashara, kuendelea kuimarika kwa uchumi, na utekelezaji madhubuti wa sera za fedha na bajeti. Aidha, kiwango cha mikopo chechefu kilipungua kutoka asilimia 5.3 Juni 2023 hadi asilimia 4.1 Juni 2024. Upungufu huo ulichangiwa na kuboreshwa kwa mazingira ya biashara ambayo yameimarisha uwezo wa wakopaji kurejesha mikopo kwa wakati. Serikali kupitia Benki Kuu imeendelea kuchukua hatua kadhaa kupunguza mikopo chechefu, ikiwa ni pamoja na kuziagiza benki kuboresha usimamizi wa mikopo, kuwasilisha mikakati ya kupunguza uwiano wa mikopo chechefu, na kuhamasisha matumizi ya kanzidata ya taarifa za wakopaji.

**21.** ***Mheshimiwa Spika***, hadi Juni 2024, deni la Serikali lilikuwa shilingi bilioni 96,884.18 ambapo deni la nje lilikuwa shilingi bilioni 64,932.94 na deni la ndani lilikuwa shilingi bilioni 31,951.24. Tathmini ya uhimilivu wa deni iliyofanyika Juni 2024 imeonesha kuwa deni ni himilivu na viashiria vya deni la Serikali viko ndani ya wigo unaokubalika kimataifa katika kipindi cha muda wa kati na mrefu.

**22.** ***Mheshimiwa Spika***, mwaka 2023/24, Kampuni za ***Fitch Ratings*** na ***Moody's Investors Service*** zilifanya mapitio ya tathmini ya nchi kukopesheka katika masoko ya mitaji ya kimataifa na

kuchapisha matokeo ya daraja B1 na B+ mtawalia. Matokeo haya yalitokana na ukuaji mzuri wa uchumi unaoweza kuhimili mitikisiko ya kiuchumi, utekelezaji wa mageuzi ya kimuundo yanayoboresha mazingira ya biashara, ufanisi wa ukusanyaji wa mapato na usimamizi wa fedha za umma.

**23.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa ***Moodys rating***, Tanzania sasa ni miongoni mwa nchi tano bora kiuchumi kati ya nchi 25 za kusini mwa Jangwa la Sahara zinazotathminiwa na ***Moody's,*** ikifuata Botswana (A3), Mauritius (Baa3), Cote d'Ivoire (Ba2), na Afrika Kusini (Ba2). Katika Afrika Mashariki, Tanzania iko juu ya nchi zote za EAC ambapo Kenya (B3), Rwanda (B2), na Uganda (B2). Nchi zingine za Afrika zinazoshikilia daraja B1 kulingana na Moody's ni Namibia, Benin, na Senegal. Kwa upande wa tathmini ya ***Fitch Ratings***, nchi za Afrika zinazoshikilia daraja kama Tanzania (B+) ni Rwanda na Benin. Aidha, kwa Nchi za Afrika Mashariki zipo nchi mbili ambazo ni Tanzania na Rwanda na zingine zipo chini ya hapo (Kenya, Uganda na zingine). Fitch - Daraja la B+ kwa Nchi za SADC ipo Tanzania pekee na nchi 4 zipo chini ya hapo (Angola, Lesotho, Mozambique na Zambia) na nchi 3 zipo juu ya hapo (Namibia, Seychelles na South Africa).

**24.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa *Moodys rating*, – Daraja la B1 kwa Afrika Mashariki ipo Tanzania pekee na nchi zingine zipo chini ya hapo (Rwanda, Kenya, DRC, Uganda na zingine) Aidha, Daraja la B1 kwa Nchi za SADC zipo nchi mbili zikiwemo Tanzania na Namibia na nchi 2 zipo chini ya hapo (Angola na DRC) na Tanzania inazifuatia Nchi za (Botswana, Mauritius na South Africa

**25.** ***Mheshimiwa Spika,*** Matokeo mazuri ya Tanzania yanakuja kufuatia jitihada za serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na ***Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan*** ikiwemo Ukuaji wa Uchumi na Ustahimilivu. Tanzania imeonyesha uwezo wa kiuchumi kuhimili majanga mbalimbali ya kimataifa kama COVID-19 na vita ya Urusi-Ukraine, kutokana na utekelezaji thabiti wa sera za bajeti na fedha, ambazo zimechochea ukuaji wa uchumi na kudhibiti mfumuko wa bei. Mageuzi ya Kimuundo; Kuimarika kwa mageuzi ya kimuundo yameboresha utendaji wa taasisi za serikali na mazingira ya biashara nchini. Hii imeonekana kupitia ongezeko la

mikopo kwa sekta binafsi na kuvutia uwekezaji kutoka ndani na nje ya nchi.

**26.** ***Mheshimiwa Spika,*** kuhusu nidhamu ya Mapato na Usimamizi wa Fedha za Umma; Serikali imeimarisha ukusanyaji wa mapato na usimamizi wa fedha, ikiruhusu kuendeleza miradi mikubwa kama Bwawa la Mwalimu Nyerere, Reli ya SGR na Daraja la Magufuli. Kuongezeka huku kwa mapato na usimamizi mzuri vinachangia deni la Serikali kuendelea kuwa himilivu.

**27.** ***Mheshimiwa Spika***, maelezo ya kina kuhusu mwenendo wa viashiria vya uchumi yanapatikana katika **Kiambatisho Na. 1A cha Mwongozo**.

## 3.0 MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI YA MWAKA 2023/24

**28.** ***Mheshimiwa Spika***, mwaka 2023/24, Serikali ilikadiria kukusanya na kutumia shilingi bilioni 44,338.07. Katika kipindi hicho, Serikali ilikusanya jumla ya shilingi bilioni 42,920.62, sawa na asilimia 96.7 ya bajeti iliyoidhinishwa. Kiasi hiki kinajumuisha shilingi bilioni 29,829.89 mapato ya ndani, sawa na asilimia 95.1 ya lengo la mwaka la shilingi bilioni 31,381.01; shilingi bilioni 5,581.61 ni misaada na mikopo nafuu kutoka kwa Washirika wa Maendeleo, sawa na asilimia 102.1 ya lengo la shilingi bilioni 5,466.21; na shilingi bilioni 7,509.11 ni mikopo ya kibiashara ya ndani na nje ya nchi, sawa na asilimia 99.6 ya lengo la mwaka la shilingi bilioni 7,540.84.

**29.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi hicho, Serikali imetumia shilingi bilioni 42,945.21 kugharamia utekelezaji wa shughuli na miradi mbalimbali ya Serikali ikiwemo miradi ya kimkakati na kielelezo. Kati ya kiasi hicho, shilingi bilioni 28,308.79 ni matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 14,636.42 ni matumizi ya maendeleo.

**30.** ***Mheshimiwa Spika***, mafanikio yaliyopatikana katika utekelezaji wa Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2023/24 ni pamoja na:

(i) Kukamilika kwa ujenzi wa reli ya SGR kipande cha Dar es Salaam – Morogoro – Dodoma (KM 722) na kuanza kutoa huduma pamoja na kuendelea na ujenzi katika vipande vingine;

(ii) Kuanza uzalishaji wa umeme wa maji katika Bwawa la Julius Nyerere ambapo megawati 705 za umeme zinazalishwa kupitia mitambo mitatu (3) kati ya tisa (9) na hivyo kuimarisha hali ya upatikanaji wa umeme nchini;

(iii) Kuendelea na utekelezaji wa mradi wa Usambazaji wa Umeme Vijijini ambapo hadi sasa vimefikiwa vijiji 12,167 na vitongoji 32,827;

(iv) Kuongezeka kwa ukuaji wa uchumi na kuendelea kudhibiti mfumuko wa bei nchini;

(v) Kuendelea kutekeleza programu ya elimu ya awali, Elimumsingi na Sekondari bila ada kwa kujenga miundombinu ikiwemo shule za msingi mpya 302;

(vi) Kutoa mikopo kwa wanafunzi 229,652 wa elimu ya juu pamoja na wanafunzi 2,299 wa ngazi ya stashahada wanaosoma fani za kipaumbele ikiwemo afya, sayansi na ufundi katika vyuo vya elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi;

(vii) Kujenga na kukamilisha miundombinu pamoja na ununuzi wa vifaa na vifaa tiba kwa ajili ya zahanati, vituo vya afya na hospitali za wilaya;

(viii) Ujenzi na upanuzi wa miundombinu ya kutolea huduma za afya katika Hospitali ya Taifa, Hospitali za Rufaa za Kanda na mkoa pamoja na Hospitali Maalum ya magonjwa ambukizi ya Kibong'oto;

(ix) Ukamilishaji wa miradi 705 katika vijiji 1,733 na miradi 85 ya maji mijini ambapo imewezesha wastani wa wananchi wanaopata huduma za maji kufikia asilimia 79.6 vijijini na asilimia 90 kwa mijini.

(x) Kuendelea na ujenzi na ukarabati wa miradi mipya ya skimu za umwagiliaji yenye jumla ya hekta 143,482 na mabwawa yenye jumla ya mita za ujazo 936,535,700;

(xi) Kuendelea na ukamilishaji wa ujenzi wa daraja la Kigongo – Busisi ambapo ujenzi umefikia asilimia 91;

(xii) Ujenzi wa barabara zenye jumla ya km 4,202.36 za mijini na vijijini kupitia TARURA ambapo kati ya hizo, barabara za lami km 284.40 na barabara za changarawe kilometa 3,917.96;

(xiii) Ujenzi wa jumla ya km 1,261.06 za barabara kuu na barabara za Mikoa kupitia TANROADS; na

(xiv) Kuendelea na ujenzi wa Miundombinu ya Mabasi Yaendayo Haraka katika Jiji la Dar es Salaam ambapo barabara ya City Center – Mbagala (km 20.3) imekamilika.

**31.** ***Mheshimiwa Spika***, pamoja na mafanikio hayo, utekelezaji wa bajeti ya Serikali kwa mwaka 2023/24 ulikabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwemo: kutofikiwa kwa malengo ya makusanyo ya mapato ya ndani hususan mapato yasiyo ya kodi; kushuka kwa thamani ya shilingi kulikosababisha kuongezeka kwa malipo ya deni la Serikali na gharama za uagizaji wa bidhaa nje ya nchi; mabadiliko ya tabianchi ikiwemo mvua juu ya wastani iliyoathiri baadhi ya miundombinu na uzalishaji wa mazao ya kilimo na shughuli nyingine za kiuchumi; na kuongezeka kwa gharama za mikopo kwenye masoko ya fedha duniani.

**32.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kukabiliana na changamoto hizo, Serikali imeendelea kuchukua hatua zifuatazo: kuimarisha mifumo ya ukusanyaji na usimamizi wa mapato yasiyo ya kodi ili kuongeza ufanisi; kuangalia upya mfumo wa kodi, aina na viwango vya kodi na usimamizi wake kupitia tume ya Rais iliyoundwa na kuzinduliwa na Mheshiwa Rais hivi karibuni, kuendelea kuhamasisha umma juu ya umuhimu wa kulipa kodi, na kutoa na kudai risiti za malipo za kielektroniki za EFD; kutekeleza Mkakati wa Taifa wa Kuimarisha Upatikanaji wa fedha za Kigeni; kuendelea kutekeleza Mpango Kabambe wa Taifa wa Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (2022 - 2032); na kuendelea kuboresha mazingira wezeshi ili kuongeza tija katika sekta za uzalishaji na mauzo nje pamoja na kupunguza uagizaji wa bidhaa zinazoweza kuzalishwa nchini.

**33.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha robo ya kwanza ya mwaka 2024/25, Serikali imekusanya shilingi bilioni 11,553.33 kutoka vyanzo vyote vya ndani na nje. Kati ya kiasi hicho, shilingi bilioni 7,930.02 ni mapato ya ndani, sawa na asilimia 99.4 ya lengo la shilingi bilioni 7,976.35. Misaada na mikopo nafuu ilifikia shilingi bilioni 1,373.09. Aidha, mikopo ya kibiashara kutoka masoko ya ndani ilifikia shilingi bilioni 1,656.56 na mikopo ya kibiashara kutoka nje ilifikia shilingi bilioni 593.65.

**34.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha robo ya kwanza ya utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2024/25, ridhaa ya shilingi bilioni 11,667.53 ilitolewa kwa ajili ya matumizi ya kawaida na maendeleo. Kati ya kiasi hicho, matumizi ya kawaida ni shilingi bilioni 7,549.62 na matumizi ya maendeleo ni shilingi bilioni 4,117.91. Ridhaa ya matumizi ya shilingi bilioni 114.20 iligharamiwa kwa mkopo wa muda mfupi kutoka Benki Kuu ambayo yapo ndani ya kiwango kinachokubalika kisheria.

**35.** ***Mheshimiwa Spika***, maelezo ya kina kuhusu utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya mwaka 2023/24 yanapatikana katika **Kiambatisho Na. 1C** cha Mwongozo.

## 4.0 MWONGOZO WA MAANDALIZI YA MPANGO NA BAJETI YA SERIKALI KWA MWAKA 2025/26

### 4.1 Misingi na Shabaha za Viashiria vya Uchumi Jumla

**36.** ***Mheshimiwa Spika***, misingi iliyotumika katika kuandaa malengo ya uchumi jumla kwa mwaka 2025/26 ni pamoja na:

(i) Kuimarika kwa uchumi wa dunia na utulivu wa bei katika masoko ya fedha na bidhaa;

(ii) Kuongezeka kwa ushiriki wa sekta binafsi katika uwekezaji na biashara;

(iii) Kuendelea kuhimili athari za mabadiliko ya tabia nchi na majanga ya asili na yasiyo ya asili (ukame, vita, magonjwa ya mlipuko na mafuriko);

(iv) Kuimarika kwa upatikanaji na usalama wa chakula nchini; na

(v) Kuendelea kuwepo kwa amani, usalama na utulivu wa ndani ya nchi na katika nchi jirani.

**37.** ***Mheshimiwa Spika***, kutokana na uchambuzi na maoteo yaliyofanyika, shabaha na malengo ya uchumi jumla yatakayozingatiwa ni pamoja na:

(i) Pato halisi la Taifa linakadiriwa kukua kwa asilimia 5.8 mwaka 2025 na kuongezeka hadi asilimia 6.1 mwaka 2026;

(ii) Mfumuko wa bei unatarajiwa kubaki kwenye wigo wa tarakimu moja wa wastani wa asilimia kati ya 3.0 - 5.0 katika muda wa kati;

(iii) Mapato ya ndani kufikia asilimia 16.1 na mapato ya kodi asilimia 13.0 ya Pato la Taifa kwa mwaka 2025/26;

(iv) Kuwa na nakisi ya bajeti isiyozidi asilimia 3.0 ya Pato la Taifa; na

(v) Kuwa na akiba ya fedha za kigeni kwa kiwango kinachokidhi mahitaji ya uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje kwa kipindi kisichopungua miezi minne (4).

### 4.2 Maeneo ya Vipaumbele

**38.** ***Mheshimiwa Spika***, mwaka 2025/26, Serikali itaendelea kutekeleza vipaumbele vilivyoainishwa katika Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/22 – 2025/26 ambavyo ni kuchochea uchumi shindani na shirikishi, kuimarisha uwezo wa uzalishaji viwandani na utoaji huduma, kukuza uwekezaji na biashara, kuchochea maendeleo ya watu na kuendeleza ujuzi. Aidha, kwa kuzingatia vipaumbele vya Mpango wa Maendeleo, maeneo mahsusi yatakayopewa kipaumbele cha bajeti kwa mwaka 2025/26 ni:

(i) Uendelezaji wa miundombinu;

(ii) Uimarishaji wa sekta za uzalishaji na huduma za jamii;

(iii) Usimamizi wa mazingira na mabadiliko ya tabianchi;

(iv) Kuboresha usimamizi na mifumo ya kitaasisi ili kuimarisha utawala bora;

(v) Kukuza usawa wa kijinsia na uwezeshaji wa makundi maalum; na

(vi) Kugharamia maandalizi ya uchaguzi mkuu wa mwaka 2025.

**4.3 Makadirio ya Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2025/26**

**39.** ***Mheshimiwa Spika***, mwaka 2025/2026, Serikali inakadiria kukusanya mapato kutoka kwenye vyanzo vyote jumla ya shilingi bilioni 55,061.61. Kati ya kiasi hicho, mapato ya ndani ni shilingi bilioni 38,962.49 ikilinganishwa na maoteo ya shilingi bilioni 34,610.65 mwaka 2024/25. Ongezeko hilo limezingatia misingi ya uchumi jumla, mikakati na hatua zinazoendelea kuchukuliwa na Serikali kuimarisha ukusanyaji wa mapato ikiwemo kuhimiza matumizi ya mifumo ya TEHAMA, kudhibiti utoaji wa misamaha ya kodi, na kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji zitakazowezesha uibuaji wa vyanzo vipya vya mapato. Dhamira ya Serikali ni kuhakikisha kuwa mapato ya ndani yanaendelea kugharamia kiasi kikubwa kwenye bajeti ya Serikali kisichopungua asilimia 70 ya bajeti yote. Hivyo, Serikali kupitia Mamlaka ya Mapato Tanzania na taasisi nyingine za Serikali itaendelea kutekeleza mkakati wa muda wa kati wa ukusanyaji wa mapato wenye lengo la kuongeza mapato ya ndani na kupunguza utegemzi wa mikopo na misaada katika bajeti. Aidha, misaada kutoka kwa washirika wa maendeleo inakadiriwa kuwa shilingi bilioni 1,024.88, mikopo nafuu kutoka kwa Washirika wa Maendeleo shilingi bilioni 5,667.04 na mikopo ya kibiashara kutoka vyanzo vya ndani na nje shilingi bilioni 9,407.20.

**40.** ***Mheshimiwa Spika***, matumizi ya Serikali yanatarajiwa kufikia shilingi bilioni 55,061.61 kwa mwaka 2025/26. Kati ya kiasi hicho, matumizi ya kawaida ni shilingi bilioni 38,602.18 na matumizi ya maendeleo shilingi bilioni 16,459.43. Aidha, makadirio ya mapato

na matumizi ya Serikali kwa mwaka 2025/26 yameainishwa katika **Sehemu ya Pili ya Mwongozo**.

### 4.4 Maelekezo Mahsusi ya Mwongozo

**41.** ***Mheshimiwa Spika***, Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2025/26 umeainisha maelekezo mbalimbali ambayo Maafisa Masuuli wanaelekezwa kuzingatia kikamilifu wakati wa uandaaji, utekelezaji, ufuatiliaji na tathmini ya mpango na bajeti. Miongoni mwa maelekezo hayo ni kama ifuatavyo:

(i) Kuzingatia ukamilishaji wa miradi inayoendelea kabla ya kuibua miradi mipya sambamba na kulipa madeni ya miradi inayoendelea au iliyokamilika;

(ii) Kuhakikisha kuwa mapato yote yanayokusanywa yanaingizwa Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali kwa mujibu wa matakwa ya Kifungu 58(a) cha Sheria ya Bajeti, Sura 439 isipokuwa pale ilipoelekezwa vinginevyo kwa mujibu wa Sheria husika. Aidha, Mafungu yanaelekezwa kuzingatia matumize ya mfumo wa MUSE wanapofanya malipo;

(iii) Kuhakikisha matumizi sahihi ya mifumo ya kielektroniki ya Serikali ya ukusanyaji wa mapato kwa kufanya uhakiki, usuluhishi na ukaguzi wa mifumo mara kwa mara kwenye vituo vyote vya makusanyo ili kudhibiti mianya ya upotevu wa mapato;

(iv) Kutekeleza Mwongozo wa Utaratibu wa Maombi na Utoaji wa Fedha wa mwaka 2021 unaosisitiza kutoingia mikataba bila kuwa na uhakika wa fedha ili kuzuia ulimbikizaji wa madeni;

(v) Kuzingatia matakwa ya Sheria ya Ununuzi wa Umma, Sura 410 iliyoweka ukomo wa zabuni zinazoweza kutolewa kwa wasio wazawa ili kuwawezesha wazawa (local content) na kuongeza mzunguko wa fedha katika uchumi; pamoja na kuzingatia matumizi ya mfumo wa kielektroniki wa ununuzi wa umma;

(vi) Kutoingia mikataba na wazabuni bila kuzingatia sheria, taratibu na miongozo iliyopo ikiwemo sheria za kodi, miradi mipya

isiyokuwa na maandalizi ya msingi kama vile malipo ya fidia kupisha mradi au upembuzi yakinifu;

(vii) Kutekeleza Mkakati wa Taifa wa Kuimarisha Upatikanaji wa Fedha za Kigeni ikiwemo: kudhibiti matumizi yasiyo ya lazima ya fedha za kigeni; kuongeza uzalishaji wa bidhaa na huduma kwa mauzo ya nje; kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji ili kuvutia mitaji kutoka nje ya nchi; na kutoa kipaumbele kwa bidhaa na huduma za ndani;

(viii) Kuendelea kufuatilia kwa karibu utendaji wa mashirika ya umma hususani yale yanayojiendesha kibiashara na kuyaandalia mkakati wa kuyawezesha kujiorodhesha katika soko la hisa ili kupunguza wajibu wa Serikali kudhamini na kugharamia uendeshaji wa mashirika hayo;

(ix) Ushirikishaji wa sekta husika katika utekelezaji wa miradi inayohusisha sekta zaidi ya moja kabla, wakati na baada ya utekelezaji; na

(x) Kuzingatia masuala ya mazingira na mabadiliko ya tabianchi pamoja na masuala ya jamii katika upangaji na utekelezaji wa bajeti ya miradi ya maendeleo.

Maelezo ya kina kuhusu maelekezo mahsusi ya Mwongozo yanapatikana katika **Sehemu ya Nne ya Mwongozo**.

## 5.0 Hitimisho

**42.** ***Mheshimiwa Spika***, kuridhiwa kwa mapendekezo ya Mwongozo kutawezesha kukamilika kwa maandalizi ya Bajeti za Mafungu kwa wakati; kuimarika kwa usimamizi wa matumizi ya fedha za umma; kuimarika kwa ukusanyaji wa mapato ya ndani; kuimarika kwa utawala bora na utawala wa sheria; na kuongezeka kwa uwajibikaji na ushiriki wa wadau mbalimbali ikiwemo sekta binafsi katika uandaaji, utekelezaji pamoja na ufuatiliaji na tathmini ya Mpango na Bajeti. Hivyo, Maafisa Masuuli wa Wizara, Idara Zinazojitegemea, Wakala za Serikali, Ofisi za Wakuu wa Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Taasisi na Mashirika ya Umma wanaelekezwa kuzingatia kikamilifu

maelekezo yote yaliyopo kwenye Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2025/26 sambamba na Sheria ya Bajeti, Sura 439 na Kanuni zake.

**43.** ***Mheshimiwa Spika***, nitumie fursa hii kuwapongeza wananchi ambao wamejitokeza kwa wingi kujiandikisha kushiriki Uchaguzi wa Serikali za Mitaa uliopangwa kufanyika tarehe 27 Novemba 2024, chini ya uratibu mzuri wa **Mheshimiwa Mohamed Omary Mchengerwa Mbunge wa jimbo la Rufiji – Pwani na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais – TAMISEMI pamoja na Timu yake.** ***NISEME TU WANANCHI WAMEUPIGA MWINGI***. Aidha, niwasihi wananchi wenzangu, kama tulivyojiandikisha, tujitokeze kwa wingi pia siku hiyo ya uchaguzi ili kuwapigia kura viongozi watakaoongoza kwa kipindi cha miaka mitano ijayo katika ngazi za Mitaa, Vijiji na Vitongoji. Pia niwasisitize wananchi wenzangu kuchagua viongozi wenye maono, uadilifu na uwezo mzuri watakaosimamia vizuri maendeleo na ustawi wa jamii zetu.

**44.** ***Mheshimiwa Spika***, napenda kuwashukuru na kuendelea kuwaomba waheshimiwa wabunge, waandishi wa habari, viongozi wa dini, viongozi wa kimila, taasisi za kiraia, wasanii, vyama vya siasa na wadau wengine kuendelea na jitihada za uelimishaji na uhamasishaji wa wananchi kuhusu umuhimu wa kushiriki katika uchaguzi hususan uchaguzi wa Serikali za Mitaa wenye kaulimbiu isemayo ***"Serikali za Mitaa, Sauti ya Wananchi, Jitokeze Kushiriki Uchaguzi"***. Aidha, ninawahimiza wananchi wote wenye vigezo na sifa za kugombea nafasi mbalimbali waendelee kujitokeza kugombea nafasi hizo. Hivyo, ninawatakia uchaguzi mwema, wenye amani na utulivu katika kipindi chote kuanzia uteuzi wa wagombea, kampeni, upigaji kura, wakati wa kutangaza na kupokea matokeo ya uchaguzi.

**45.** ***Mheshimiwa Spika***, mwisho lakini sio kwa umhimu, leo ***Simba Sports Club*** wanacheza, tuwaombee washinde, Simba wasiposhinda wazee wanakosa raha, wazee ni watu wakubwa, hata humu ndani ya Bunge wapo na wakikosa raha wanaacha kutushauri.

**46.** ***Mheshimiwa Spika,*** baada ya maelezo hayo, naomba sasa Bunge lako Tukufu lipokee na kujadili Mapendekezo ya

Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2025/26.

**47.** ***Mheshimiwa Spika***, naomba kutoa hoja.

Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba Madelu (Mb)
**Waziri wa Fedha**
01 Novemba 2024

**WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MWENYEKITI:** Haya, hoja imeungwa mkono na nawaona wazee wameamua wasiunge mkono hoja, ahsante sana. *(Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, sasa namwita Mwenyekiti wetu wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti, Mheshimiwa Oran Manase Njeza aje awasilishe maoni kuhusu hoja hizi mbili ambazo zimewasilishwa mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, karibu.

**MHE. ORAN M. NJEZA – MWENYEKITI KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kifungu cha 9 (4)(1) kipengele (a) cha Sheria ya Bajeti Sura 439 pamoja na Kanuni ya 113 (4) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Februari, 2023, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti kuhusu Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2025/2026 pamoja na mapendekezo ya mwongozo wa maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2025/2026.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2025/2026 ni Mpango wa mwisho katika mfululizo wa utekelezaji wa Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/2022 kufikia

2025/2026 uliobeba dhima ya "Kujenga Uchumi Shindani na Viwanda kwa Maendeleo ya Watu."

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imefanya uchambuzi wa kina wa Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Mwaka 2025/2026 pamoja na Mapendekezo ya Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2025/2026 kama ilivyowasilishwa na Serikali na kutoa ushauri wake. Nyaraka zilizotumika kwenye uchambuzi wa Kamati ni kama zinavyoonekana kwenye taarifa ya Kamati, taarifa imegawanyika katika sehemu 10 kama zinavyoonekana kwenye Taatifa ya Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kipekee kabisa naomba nimpongeze Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa hatua za makusudi na za kibunifu alizochukua katika kutekeleza miradi kwenye sekta mbalimbali za kiuchumi. Pongezi hii naitoa baada ya Kamati kufanya uchambuzi wa kina wa utekelezaji wa miradi na matokeo chanya yanayoonekana kwa uwekezaji katika bandari, reli ya SGR na Bwawa la Mwalimu Nyerere.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii inanikumbusha msemo wa kiongozi aliyekuwa mke wa Mheshimiwa Rais wa Marekani Michelle Obama aliwahi kusema *"The best revenge is success and hard work you don't have to say anything to haters."* Hili limethibitishwa na Mheshimiwa Rais kwa sababu wote ambao hawakupenda tufanikiwe katika uwekezaji wa bandari nafikiri leo wanaona aibu kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba taarifa yote ya Kamati iingie kwenye Taarifa Rasmi za Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mapitio ya hali ya uchumi, uchambuzi wa hali ya uchumi jumla, kutokana na takwimu za mwenendo wa ukuaji wa uchumi wa dunia, Kamati inatoa ushauri ufuatao kwa Serikali:

(a) Kutumia fedha zinazotokana na mwenendo wa uchumi wa dunia kwa kuongeza uzalishaji wenye tija wa mazao ya kilimo,

viwanda, madini na utalii kwa lengo la kuongeza mauzo ya nje ya nchi.

(b) Kuongeza ufanisi wa utendaji kazi wa uchukuzi na usafirishaji ili kulinda ushindani wa kikanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatia mwenendo wa mfumuko wa bei Kamati inatoa ushauri ufuatao:-

(a) Serikali kuiwezesha kifedha Mamlaka ya Hifadhi ya Chakula Nchini *(NFRA)* pamoja na Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko *(CPB)* ili ziweze kuhifadhi akiba ya kutosha ya chakula na hivyo kudhibiti mfumko wa bei. Ushauri huu unatokana na tahadhari iliyotolewa kuhusu mabadiliko ya tabianchi yanayoweza kuathiri shughuli za kilimo kwa mwaka 2024 na 2025;

(b) Serikali pia kuchukua hatua stahiki kupunguza mfumko wa bei kutokana na tahadhari ya kuongezeka kwa bei za mafuta katika soko la dunia kwa 0.9% sawa na Dola za Marekani 81 kwa pipa pamoja na kuanzisha mkakati wa kuhifadhi akiba ya mafuta *(Strategic oil reserve)* ili kuiwezesha nchi kununua mafuta pindi bei zinaposhuka na kuyatumia pindi bei zinapopanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatia ukuaji huo, Kamati inashauri Masuala yafuatayo: -

(a) Takwimu zinaonyesha kwamba sekta za huduma zimekua kwa kasi ukilinganisha na Sekta za uzalishaji kwa sababu ya uwekezaji mkubwa wa Serikali. Kamati inaishauri Serikali kuweka uwiano sawa wa uwekezaji baina ya sekta ya huduma na sekta ya uzalishaji ili sekta za uzalishaji nazo zikue kwa kasi na kuchochea ukuaji wa uchumi ili kufikia lengo la asilimia nane hadi 10% kama ilivyotarajiwa katika Dira ya Maendeleo ya Taifa ya mwaka 2025;

(b) Serikali kuhakikisha kwamba inawekeza kikamifu katika kukuza sekta zenye mchango mkubwa katika pato la Taifa ikiwemo sekta ya kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Deni la Serikali. Licha ya kwamba Deni la Serikali ni himilivu kwa muda mfupi wa kati na mrefu Kamati inaishauri Serikali kufanya yafuatayo ili kuhakikisha deni hili linaendelea kuwa himilivu:-

(a) Kuongeza wigo na ukusanyaji wa mapato ya ndani ili yawe na uwezo wa kugharamia deni;

(b) Mikopo yote inayopatikana ni vema Serikali ikaielekeza katika miradi inayochochea kasi ya ukuaji wa uchumi na mauzo ya bidhaa na huduma nje ya nchi ili kuhakikisha linaendelea kuwa himilivu; na

(c) Kutoa kipaumbele kwa mikopo yenye masharti nafuu na yenye masharti ya kati ili kupunguza mzigo wa riba pamoja na muda mfupi wa neema ambao unaambatana na mikopo ya kibiashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ya umaskini na maendeleo ya watu. Dira ya Maendeleo ya Taifa ya 2025 ilibainisha kwamba ili Tanzania iondokane na umaskini ni lazima uchumi ukue kwa asilimia nane hadi 10%. Kamati inaipongeza Serikali kwa kuendelea kutekeleza Sera, programu na miradi mbalimbali yenye lengo la kupunguza umaskini na kuchochea maendeleo ya watu. Hata hivyo, Kamati inatoa ushauri kwa Serikali kwa masuala yafuatayo:-

(a) Sekta ya kilimo ina uhusiano mkubwa na hali ya umaskini nchini. Jumla ya watu milioni 28 sawa na 45.9% ya watu wote Tanzania wanajishughulisha na sekta ya kilimo. Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kwamba inakamilisha miradi yote ya kilimo kwa wakati ili kupunguza hali ya umaskini nchini.

(b) Kamati inaishauri Serikali kutenga bajeti kwa mwaka wa fedha 2025/2026 kwa ajili ya kufanya utafiti wa mapato na matumizi ya kaya ili kupata takwimu ya hali ya umaskini nchini kwa kuangalia viashiria vyote 17.

(c) Kwa mujibu wa Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2022, idadi ya watu ilikuwa ni 66.74, na inakadiriwa kufika ifikapo

mwaka 2035 idadi ya watu nchini itakuwa 87.51 kutokana na ongezeko la watu la 3.2% kila mwaka. Ongezeko hili la idadi ya watu nchini haliendani na ukuaji wa uchumi. Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kwamba ongezeko la watu linaendana na ukuaji wa uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mapitio ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo, Kamati imefanya uchambuzi wa utekelezaji wa Vipaumbele vya Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano katika Mwaka 2023/2024 na Utekelezaji katika Kipindi cha Robo ya Kwanza Mwaka 2024/2025. Miradi iliyofanyiwa uchambuzi ni miradi 17 inayolenga kuleta matokeo katika maeneo matano ya kipaumbele ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo, maeneo hayo ni kama yanavyoonekana kwenye taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa utekelezaji wa miradi; ujenzi wa reli ya kisasa kwa kiwango cha Kimataifa, *SGR*. Uongozi ni kuonyesha njia. Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ataingia kwenye kumbukumbu za historia za nchi hii, kama Mheshimiwa Rais aliyezindua safari ya kwanza ya reli ya *SGR* ambayo hivi sasa Watanzania wananufaika nayo. Hakika kongole kwako Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imefanya uchambuzi kuhusu utekelezaji wa mradi na inatoa ushauri ufuatao: -

(a) Serikali itumie mpango wa kufadhili ujenzi wa Reli ya Kisasa ya *SGR* kwa kutumia *ECGA (Export Credit Guarantee Agency)* ili kukamilisha vipande vyote vilivyobaki kwa haraka, hususan vipande vya Uvinza – Malagarasi - Msongati na Kaliua – Mpanda - Kalema;

(b) Serikali itumie fursa ya uwepo wa Sheria ya mfumo wa kukaribisha sekta binafsi kutumia miundombinu ya reli kwa makubaliano ya malipo *(Open Access)* ili kuvutia wawekezaji katika reli ya *SGR*;

(c) Kutenganisha usimamizi wa reli ya Kisasa ya *SGR* na reli ya *MGR* na kulifanya Shirika la *TRC* kuwa Shirika Hodhi linalosimamia Mashirika mawili.

(d) Ujenzi wa vituo vya reli uende sambamba na ujenzi wa miundombinu ya kuziunganisha na barabara ili kurahisisha usafiri wa abiria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ununuzi wa meli na ujenzi wa bandari ya uvuvi. Kamati inaipongeza Serikali kwa kuwa na mikakati ya kukuza sekta ya uvuvi ili nchi inufaike na rasilimali za bahari kwa lengo la kukuza uchumi wa bluu. Baada ya uchambuzi Kamati ina ushauri ufuatao:-

(a) Ujenzi wa bandari ya uvuvi uende sambamba na kuweka mazingira ya biashara nyingine zinazoendana na bandari ya uvuvi kama vile maeneo ya kuchagulia *(sorting area)*, kuhifadhia na kuchakata Samaki, kuwe na *sorting area;*

(b) Aidha, ujenzi wa bandari uende sambamba na ujenzi wa miundombinu ya Kanda maalumu ya mauzo nje *(EPZ* na *SEZ)* ili kusaidia usindikaji wa mazao ya samaki na kuyauza nje ya nchi; na

(c) *TAFICO* isitegemee fedha za Serikali pekee katika kununua meli na badala yake ishirikishe sekta binafsi, kununua meli nyingi zaidi kwa kupitia mfumo wa Ubia baina ya Sekta Binafsi na Sekta ya Umma *(Public Private Partnership)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu miundombinu ya Nishati, Kamati inatambua juhudi zinazofanywa na Serikali katika kuongeza uzalishaji wa umeme nchini, ikiwa ni pamoja na kukamilisha ujenzi wa mradi wa Bwawa la Umeme la Mwalimu Julius Nyerere ambalo hivi sasa linaingiza katika gridi ya Taifa megawati 1,175 na hivyo kufanya uzalishaji wa umeme nchini kufikia Megawati 3,113.35 sawa na ongezeko la 61%. Uchambuzi wa mradi katika sekta ya Nishati umebaini masuala yafuatayo ambayo Kamati imeyatolea mapendekezo:-

(a) Kamati inaishauri Serikali kupitia Shirika la *TANESCO* kutumia fursa ya uwekezaji kwa njia ya Ubia ili kuendeleza miradi kama ile ya Ruhuji Megawati 358 na Rumakali Megawati 222 kuliko kusubiria fedha za bajeti pekee;

(b) Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kwamba miundombinu ya usambazaji wa umeme inaimarishwa ili kuimarisha upatikanaji wa umeme kwa wananchi. Hivi sasa Taifa lina ziada ya umeme wa Megawati 606. Hata hivyo, ziada hiyo inaweza kuwa inatokana na wananchi wengi kutounganishwa kwenye gridi ya Taifa na kutowafikia wananchi kutokana na ubovu wa miundombinu;

(c) Serikali iongeze vituo vya kujaza gesi katika Jiji la Dar es Salaam, na kuendelea na mradi wa usambazaji wa gesi kwa matumizi ya nyumbani na viwandani;

(d) Serikali iwekeze katika vyanzo vingine vya nishati kama nishati ya joto ardhi *(Geothermal)* ili kuongeza kiwango cha nishati ya umeme;

(e) Serikali iimarishe na kutekeleza miradi ya gridi imara ili kuboresha usafirishaji na usambazaji wa umeme;

(f) Upotevu wa umeme hivi sasa ni 16% ambayo ni kiwango cha juu ya kiwango cha upotevu na haikubaliki Kimataifa ni asilimia nne tu hadi 10%, hivyo ni wazi kwamba upotevu huu unaliongezea Shirika la *TANESCO* hasara jambo ambalo linaenda sambamba na umuhimu wa kuimarisha gridi ya umeme; na

(g) Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha wakandarasi wote wanaotekeleza miradi ya umeme vijijini wana uwezo wa kifedha ili kutekeleza miradi hiyo. Kamati imebaini kuwa wakandarasi wengi wa ndani wana uwe uwezo mdogo wa kifedha na hivyo kuchelewesha utekelezaji wa miradi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu programu ya miradi ya kimkakati sekta ya ujenzi. Kamati imefanya uchambuzi na kubaini

kuwa sekta ya ujenzi wa barabara inakabiliwa na changamoto zifuatazo: -

(a) Utekelezaji kutokuzingatia ujenzi wa barabara za kimkakati;

(b) Kuanza ujenzi wa barabara nyingi kwa pamoja bila kuzingatia uwezo wa kifedha;

(c) Malimbikizo ya madeni ya wakandarasi na kusababisha sehemu kubwa ya bajeti kutumika kulipa madeni ya miaka ya nyuma;

(d) Uwezo mdogo wa kifedha wa wakandarasi wa ndani katika kushiriki kwenye ujenzi wa barabara unatokana na Serikali kutokuwalipa madeni na hati za malipo kwa wakati pamoja na riba kubwa za mikopo inayotozwa na taasisi za kifedha nchini;

(e) Ukosefu wa fedha za kutosha za kufanya ukarabati na matengenezo ya barabara;

(f) Barabara kujengwa chini ya kiwango, na hivyo kuharibika ndani ya muda mfupi;

(g) Barabara nyingi hujengwa kwa vipande na hivyo kutokukamilika kwa wakati; na

(h) Barabara nyingi za vijijini zinajengwa kwa udongo na hivyo kuathirika na mvua za msimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaishauri Serikali masuala yafuatayo: -

(a) Serikali kutoa kipaumbele katika ujenzi na ukarabati wa barabara za kimkakati na zenye manufaa makubwa kiuchumi;

(b) Serikali kutenga fedha za kutosha kila mwaka kwa ajili kufanya ukarabati na matengenezo ya barabara kuu, barabara za mijini na vijijini;

(c) Serikali irejeshe utaratibu wa zamani wa kuwa na timu ya ukaguzi wa barabara mara kwa mara ili kurekebisha maeneo yanayoharibika ili kuzuia uharibifu mkubwa baadaye;

(d) Serikali kutoa kipaumbele cha kulipa madeni ya wakandarasi wa barabara kwa wakati;

(e) Serikali kuhakikisha inawasilisha fedha zinazotokana na vyanzo mahususi *(earmarked source)* kwa Mfuko wa Barabara kama vilivyokusanywa; na

(f) Serikali kuhakikisha barabara zinajengwa kwa kuzingatia ubora na viwango vinavyokubalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye sekta ya habari, mawasiliano na teknolojia ya Habari, Kamati inaishauri Serikali mambo yafuatayo: -

(a) Kukamilisha mradi wa minara kwa wakati ili kuimarisha mawasiliano ya simu vijijini pamoja na kuongeza mtandao kwa ajili ya shughuli za kiuchumi na kijamii;

(b) Kuongeza matumizi ya teknolojia ya akili bandia *(Artificial Intelligence – AI)* katika Taasisi za Serikali; na

(c) Serikali kushirikisha sekta binafsi kukamilisha ujenzi na usambazaji wa Mkongo wa Taifa ili kuongeza matumizi ya mtandao na kukuza uchumi wa kidigitali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye sekta ya kilimo, Kamati imefanya uchambuzi na kubaini kuwa bajeti ya kilimo imeongezeka zaidi ya mara nne kutoka shilingi bilioni 294 kwa mwaka 2021/2022 hadi kufikia shilingi trilioni 1.24 kwa mwaka 2023/2024. Changamoto zinazoikabili sekta ya kilimo ni kama zinavyoonekana kwenye taarifa ya kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kukabiliana na changamoto hizo, Kamati inashauri Serikali masuala yafuatayo: -

(a) Serikali isimamie vyema mradi wa ujenzi wa mabwawa makubwa kwa ajili ya umwagiliaji na kuhakikisha kwamba yanakamilika na kutumika ili kuwe na tija iliyokusudiwa. Hivi sasa Serikali ina jumla ya miradi ya mabwawa 18 na kati ya hayo yaliyokamilika ni mabwawa matatu tu;

(b) Serikali iendelee kutafuta masoko ya uhakika na yanayotabirika, sambamba na kutafuta ithibati kwa mazao yanayohitaji ithibati ili yauzwe nje ya nchi;

(c) Serikali iongeze uzalishaji wa pembejeo bora za kilimo ili kuongeza uzalishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile ni vyema Serikali ikafanya tathmini ya ongezeko la bajeti ya kilimo kwa miaka miwili iliyopita ili kubaini mchango wa bajeti iliyoongezeka katika kukuza uchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye sekta ya utalii, sote tunakumbuka juhudi za Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika kutangaza utalii kupitia filamu ya *The Royal Tour;* hakika matunda yake yameonekana. Narudia tena, hongera Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imefanya uchambuzi na kubaini kwamba, kiwango cha mchango wa sekta ya utalii kwa kuliingizia Taifa fedha za kigeni ulifikia 25% ikilinganishwa na lengo la 27% ifikapo mwaka 2025/2026, na idadi ya watalii imeongezeka kufikia watalii takribani 3,800,000. Kati ya watalii hao watalii wa ndani walikuwa ni 1,976,000 na wageni wa nje walikuwa ni 1,808,000 kwa mwaka 2023/2024, ikilinganishwa na lengo la watalii 5,000,000 ifikapo mwaka 2025/2026.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha changamoto zinazoikabili sekta ya utalii ni kama zinavyoonekana kwenye Taarifa ya Kamati. Kufuatia changamoto hizo Kamati inashauri Serikali masuala yafuatayo: -

(a) Kujenga na kukarabati miundombinu ya msingi katika hifadhi, mbuga na mapori tengefu;

(b) Kuwekeza na kuendeleza maeneo ya Kanda ya Kusini;

(c) Kutenga bajeti ili kutangaza maeneo na vivutio vipya vya utalii kama vile utalii wa kitamaduni, utalii wa mazingira, utalii wa fukwe, utalii wa afya, utalii wa michezo na utalii wa mikutano; na

(d) Kuiongezea fedha Bodi ya Utalii Tanzania *(TTB)* ili iweze kutangaza fursa na vivutio vya utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kwenye sekta ya diplomasia ya uchumi, Kamati imefanya uchambuzi wa misingi ya dhana ya diplomasia ya uchumi ili kubaini endapo Tanzania imepiga hatua katika utekelezaji wake. Misingi ya sekta ya diplomasia pamoja na changamoto ni kama inavyoonekana kwenye taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatia changamoto hizo Kamati inaushauri mambo yafuatayo: -

(a) Serikali ianzishe mfumo ya kupima na kutathmini utendaji kazi wa mabalozi kwa kutumia kigezo cha nchi wanazowakilisha;

(b) Mabalozi kuwa na utaratibu wa kutangaza fursa za ajira kwa Watanzania na masomo ya kimkakati katika nchi wanazotuwakilisha;

(c) Serikali kutenga bajeti ya kutosha kwa ajili ya uendeshaji, ukarabati na ujenzi wa miundombinu ya balozi;

(d) Kuboresha na kuimarisha mfumo wa kusajili *diaspora* na sehemu waliyopo; na

(e) Benki Kuu kuweka vigezo na mifumo rahisi ya kutuma fedha nchini ili kurahisisha zoezi la ufanyaji wa malipo kwa hao wananchi wetu wanaoishi nje ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye sekta ya elimu na maendeleo ya ujuzi, Kamati inatambua jitihada mbalimbali zilizofanywa na Serikali ili kukuza sekta ya elimu kwa kuajiri jumla ya

walimu 37,879 kwa kipindi cha miaka minne. Hata hivyo, bado sekta hii inakabiliwa na changamoto zifuatazo: -

(a) Uhaba wa walimu katika shule za sekondari na msingi ambapo viwango vya Kimataifa vinavyoelekeza uwiano wa mwalimu mmoja kufundisha wanafunzi 45;

(b) Uhaba wa vitendea kazi vya kufundisha na kujifunzia;

(c) Changamoto ya miundombinu mashuleni kama vile madarasa, mabweni, vyoo na maabara hasa kwa shule zile zilizojengwa miaka mingi iliyopita;

(d) Wataalam wanaozalishwa na mfumo wa elimu kutoendana na mahitaji ya soko la ajira; na

(e) Matumizi madogo ya teknolojia ya kisasa katika ufundishaji *(online platforms)* ili kukabiliana na tatizo la uhaba wa walimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatia changamoto hizo, Kamati inaishauri Serikali masuala yafuatayo: -

(a) Kuajiri walimu wa kutosha katika ngazi zote, pamoja na kutenga bajeti kwa ajili ya vitendea kazi pamoja na maabara za kisasa;

(b) Kutoa elimu na mafunzo yanayokuza ujuzi ili kukidhi mahitaji halisi ya soko la ajira;

(c) Kuimarisha miundombinu ya kujifunza na kujifunzia kwa vyuo vya ufundi na vyuo vya kati kama *VETA* na *SIDO*;

(d) Kuanzisha kozi fupi za ufundi na mafunzo ya amali kama vile simu, useremala, ujenzi na umeme;

(e) Kuharakisha utekelezaji wa mtaala mpya wa elimu ambao unajumuisha fani za masuala mbalimbali. Mfano, useremala, uashi, ushonaji, umeme, ufugaji wa kuku, ufugaji wa samaki, na mifugo mingine kwa njia za kisasa; na

(f) Serikali ianze kutumia madarasa janja ili kupunguza changamoto ya uhaba wa walimu katika mafunzo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye sekta ya afya, Kamati imefanya uchambuzi na kubaini kuwa sekta hii ina changamoto zifuatazo: -

(a) Uhaba wa wataalamu wa afya, vifaatiba na madawa hasa katika maeneo ya vijijini;

(b) Ukosefu wa miundombinu ya msingi kama umeme na maji katika vituo vya afya;

(c) Ukosefu wa huduma za msingi;

(d) Uhaba wa vifaatiba na madawa katika baadhi ya Vituo vya Afya, Zahanati na Hospitali za Wilaya;

(e) Uwepo wa madeni ya washitiri na wazabuni; na

(f) Wananchi wengi kushindwa kumudu gharama za matibabu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaishauri Serikali kuongeza idadi ya wataalamu wa afya, kujenga nyumba za madaktari, kuongeza vifaa tiba pamoja na kutoa huduma bora za afya kwa wananchi. Aidha, mchakato wa bima ya afya kwa wote uanze ili kuwapa wananchi matibabu nafuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2025/2026, Serikali imepanga kutumia shilingi trilioni 16.32 kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo, sawa na 29.89% ya bajeti yote ya mwaka 2025/2026 ambapo, imeshuka ikilinganishwa na 32.32% ya bajeti ya maendeleo ya mwaka huu tunaoendelea nao. Aidha, bajeti ya maendeleo imeongezeka kutoka shilingi trilioni 15.33 ya mwaka 2024/2025 hadi kufikia shilingi trilioni 16.46 kwa mwaka 2025/2026 sawa na ongezeko la 7.44% ambazo ni trilioni 1.14. Jedwali namba nane linaonesha asilimia ya bajeti ya maendeleo ya Serikali kwa mwaka 2025/2026.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo ya kipaumbele kwa mwaka 2025/2026, uzalishaji viwandani. Kwa mwaka 2023 mchango wa sekta ya uzalishaji viwandani katika pato ulikuwa asilimia saba ikiwa ni chini ya lengo la 12% ifikapo 2026. Kamati inaishauri masuala yafuatayo: -

(a) Kutekeleza Mpango wa Kuboresha Mazingira ya Uwekezaji Nchini ili kuvutia wawekezaji;

(b) Serikali kupitia viashiria vya kiushindani vya Kimataifa ili iweza kutambua viashiria ambavyo Tanzania haifanyi vizuri;

(c) Serikali kulinda viwanda vilivyopo kwenye *EPZ*;

(d) Serikali kurejesha mpango wake wa "*Road Map for Improvement of Business Environment in Tanzania*" ili kuendelea kujipima na kuboresha mazingira ya Biashara; na

(e) Serikali kuharakisha majadiliano ya mikataba ya uwekezaji hasa kwenye Mradi wa *LNG,* na Mradi wa Mchuchuma na Liganga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye sekta ya fedha, uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa tangu kutungwa kwa Sheria Ndogo Sura ya 407 kumekuwa na usimamizi hafifu wa utekelezaji wa sheria hiyo, na kusababisha matatizo makubwa katika jamii. Hivyo, Kamati inaitaka Serikali kuhakikisha kwamba inasimamia masharti ya Sheria ya Sekta Ndogo ya Fedha kuwa jambo la kipaumbele ili kupunguza malalamiko ya wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Sheria ya Benki Kuu inaipa mamlaka taasisi hiyo kufanya mapitio ya gharama ya huduma za kibenki, Kamati inaishauri Serikali kupitia taasisi hiyo kufanya mapitio ya gharama za uendeshaji wa benki za kibiashara ili kubaini sababu za vihatarishi vinavyosababisha tozo za huduma za kibenki pamoja na riba za mikopo kuendelea kuwa juu nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na changamoto zilizoikumba sekta ya maji nchini, Kamati inashauri yafuatayo: -

(a) Kufanya tathmini ya upatikanaji wa maji nchini kuanzia ngazi ya vijiji, kata, na tarafa;

(b) Kamati inaishauri Serikali kuweka mikakati ya kuendeleza miundombinu ya majisafi sambamba na miundombinu ya majitaka;

(c) Kulipa madeni ya wakandarasi na wazabuni hadi Juni, 2024 yaliyokuwa na thamani ya shilingi bilioni 415;

(d) Kuwasilisha fedha za mfuko wa maji kama zilivyo kusanywa kutoka kwenye chanzo;

(e) Kuhakikisha mitambo ya kuchimba mabwawa na visima inapata fedha za kutosha za kuendesha shughuli zao; na

(f) Kuhakikisha miradi ya maji inatekelezwa na wakandarasi wenye uwezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2025/2026 Serikali inakusudia kukusanya shilingi trilioni 55.06 sawa na ongezeko la 11.58%, ambazo ni shilingi trilioni 5.72 ikilinganishwa na bajeti ya mwaka huu ambao tunautekeleza sasa hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa Kamati umebaini kwamba mapato ya ndani yanayokusanywa na Mamlaka ya Mapato Tanzania *(TRA)* pamoja na maduhuli ya Wizara, idara na wakala pamoja na Mapato ya Msajili wa Hazina yanatarajiwa kuongezeka kwa 12.57% sawa na shilingi trilioni 4.351. Aidha, mikopo kwa ajili ya kudumisha deni la ndani *(rollover)* malipo yameshuka kwa 17.32% kutokana na kupungua kwa kiasi kitakacholipwa *(redemption profile)* ambazo ziko kwenye jedwali namba tisa linaonyesha makadirio ya bajeti ya Serikali kwa mwaka huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, madeni ya wazabuni, wakandarasi na watoa huduma. Uchambuzi wa Kamati umebaini kwamba hadi Juni, 2023 jumla ya madeni yaliyohakikiwa na Serikali yalikuwa ni shilingi bilioni 3,299 na kiasi cha madeni ambayo hayajahakikiwa ni shilingi bilioni 64.72. Hata hivyo, Serikali

haijabainisha endapo madeni ya wazabuni, wakandarasi na watoa huduma ni kihatarishi. Kihatarishi hiki kinaweza kisikidhi tafsiri sahihi ya kihatarishi ila kinaathiri utekelezaji wa Bajeti ya Serikali kila mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, kwenye sekta ya barabara, maji, kilimo na mifugo imekuwa vigumu kutekeleza miradi mipya kwa sababu ya madeni haya. Mwaka 2023 Serikali kupitia Katibu Mkuu wa Hazina ilitoa Waraka ujulikanao kama *The Treasury Circular No. 2 of 2022/2023 on Government Domestic Expenditure Arrears and Other Outstanding Obligations* kwa lengo la kuendelea kusimamia na kutekeleza mkakati wa kudhibiti na kuzuia malimbikizo ya madeni. Hata hivyo, Kamati imebaini kwamba waraka huu haujaweza kudhibiti malimbikizo ya madeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kati ya maeneo muhimu yanayopaswa kuzingatiwa na Maafisa Masuuli wakati wa upangaji wa bajeti ni pamoja kutenga bajeti ya ulipaji wa madeni kwa kuzingatia umri wa madeni na kutoa kipaumbele kwenye madeni yenye riba na adhabu. Hivyo, Kamati inashauri Mwongozo huu uweke wazi kiasi ambacho kitatengwa na Serikali kwa ajili ya kulipa madeni ya wakandarasi na wazabuni wa ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Maoni ya jumla kuhusu Mwongozo wa Mpango na Bajeti kwa Mwaka 2025/2026. Uchambuzi wa Kamati umebaini masuala mbalimbali kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa ratiba ya mpango, Serikali inawaelekeza Maafisa Masuuli kuandaa Mpango na Bajeti ya Muda wa Kati *(MTEF)* ya mwongozo huu kuidhinishwa. Aidha, vitabu vya *MTEF* viwasilishwe Tume ya Mipango na Wizara ya Fedha. Hata hivyo, uzoefu unaonyesha, ukomo wa bajeti kwa mafungu huwasilishwa kati ya mwezi Januari hadi Februari kwa Maafisa Masuuli na kuwasilisha randama ifikapo tarehe 10 Machi. Muda huo ni mchache kwa Maafisa Masuuli kufanya marekebisho kulingana na ukomo wa bajeti hasa pale wanapopaswa kupunguza bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaishauri Serikali, kuhakikisha ukomo wa Bajeti kwa Mafungu uendane sambamba

na uidhinishwaji wa mwongozo wa bajeti ili kuwapa Maafisa Masuuli nafasi ya kuandaa bajeti inayoendana na ukomo wa bajeti. Vilevile, kwa mahitaji maalum yanayohitaji nyongeza ya bajeti, maombi hayo yafanyike mapema. Kamati inapendekeza kufanya mabadiliko kwenye ratiba kama inavyoonekana kwenye taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mkakati wa kuongeza fedha za kigeni, katika kukabiliana na changamoto ya upungufu wa fedha za kigeni, Serikali imependekeza kwa Maafisa Masuuli, kuingia mikataba yote ya manunuzi kwa kutumia shilingi ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pendekezo hilo lina nia njema, ila utekelezaji wake una kasoro kwa sababu ya kushuka na kupanda kwa thamani ya shilingi. Ili pendekezo hili litekelezwe, Kamati inaishauri Serikali kwa mikataba inayohusu ununuzi wa bidhaa na huduma ndani ya Tanzania, itumike shilingi. Pia, kwa mikataba inayohusisha ununuzi wa bidhaa nje ya Tanzania, zitumike fedha za kigeni ili kuepusha hasara kwa pande zote. Vilevile, namna nyingine ya kuondokana na changamoto hii, ni Serikali kuruhusu mikataba iwe na kipengele cha kufanya mabadiliko ya kiwango cha kubadilisha fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Maelekezo Mahsusi kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa. Mwongozo unaelekeza kutenga bajeti kwa ajili ya kukamilisha miradi viporo hususani maboma yaliyoanzishwa kwa nguvu za wananchi. Aidha, jukumu hili limekuwa linatekelezeka kwa kasi ndogo kutokana na ufinyu wa bajeti za Serikali za Mitaa. Hata hivyo, mwezi Machi, 2024 mahitaji ya ujenzi na ukamilishaji wa maboma ya zahanati, vituo vya afya, maabara na madarasa yaliyokuwepo ni shilingi bilioni 267.66. Kiasi hicho cha fedha ni kikubwa kwa Serikali za Mitaa kukitenga kwa mapato ya ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, itakumbukwa kwamba katika mwaka wa fedha 2023/2024, jambo hili lilijadiliwa katika kikao chako cha Kamati ya Uongozi ambapo Serikali iliahidi kutoa fedha kwa ajili ya kukamilisha maboma hayo. Licha ya ahadi ya

Serikali, mwongozo unaelekeza Mamlaka za Serikali za Mitaa kutenga fedha kutoka mapato ya ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa Kamati umebaini kwamba, itachukua takribani miaka tisa na miezi mitatu kwa Serikali za Mitaa kukamilisha maboma kulingana na bajeti wanazotenga kila mwaka. Hivyo, Kamati inaitaka Serikali kutenga fedha kupitia ruzuku ya Maendeleo *(General Purpose Grant-GPG)* inayotegemewa kurejeshwa kwa mwaka wa fedha unaokuja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mazingira na Mabadiliko ya Tabianchi. Kamati imebaini Tanzania haipati fedha kutoka mifuko ya kimataifa ya kupambana na uharibifu wa mazingira kwenda kwenye Mfuko wa Taifa wa Mazingira kutokana na sababu zifuatazo: -

(i) Bodi ya mfuko huo ni bodi ya Ushauri sio Bodi ya uendeshaji;

(ii) Mfuko huo uko chini ya Idara iliyopo katika Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira na siyo chini ya Mamlaka au Wakala;

(iii) Fedha za mfuko hujumuishwa kwenye Bajeti ya Mfuko Mkuu na hivyo kutokuwa na uhakika kwamba zitaelekezwa kwenye shughuli ya mazingira;

(iv) Mfuko kutokuwa na chanzo cha fedha cha uhakika; na

(v) Mfuko kutokuwa na watumishi wa kutosha kutokana na muundo wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaitaka Serikali kufanya mapitio ya Muundo wa Usimamizi wa Mfuko pamoja na kutafuta chanzo kwa ajili ya Mfuko wa Mazingira, kwa sababu athari za mazingira siyo kihatarishi tena bali imekuwa janga. Serikali ione haja ya kutenga walau asilimia moja ya mapato yanayotokana na biashara ya hewa ukaa *(Carbon Credit)* ili yaelekezwe kwenye Mfuko wa Mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni ya jumla. Ili mfumo wa usimamizi wa kodi uwe na ufanisi unatakiwa kuepusha masuala makuu matatu ambayo ni:-

(i) Kuondoa ugumu wa kulipa kodi;

(ii) Kuepusha matumizi ya fedha tasilimu katika kulipa kodi; na

(iii) Kuondoa mwingiliano kati ya mlipa kodi na mkusanya kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, njia pekee inayoweza kuleta matokeo ya haraka ni matumizi ya mifumo ya TEHAMA. Kamati inatambua kwamba, Mamlaka ya Mapato imekuwa ikiendeleza ujenzi na matumizi ya mifumo kama *e-filling, IDRAS, ITAX*, *ETS* na *TANCIS*. Hata hivyo, Kamati imebaini mamlaka ilihitaji shilingi bilioni 400 kwa ajili ya kukamilisha mifumo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha miaka mitatu Serikali imekuwa haitengi Bajeti ya kutosha ili kukamilisha zoezi hilo. Hivyo, Kamati inaitaka Serikali kuhakikisha kwamba, katika mwaka wa fedha 2025/2026 suala la kukamilisha mifumo ya ukusanyaji wa mapato linapewa kipaumbele ili kuongeza mapato ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Midaki *(luggage scanners)* katika mipaka yetu hasa ya mizigo, imekuwa ni changamoto kubwa. Pamoja na athari za kiusalama zinazoweza kujitokeza kutokana na kukosekana kwa midaki, kukosekana kwa vifaa hivyo kumesababisha Maafisa Forodha kulazimika kukagua mizigo kwa kufungua na kuangalia hali ambayo inawakutanisha walipa kodi na kufanya majadiliano, na hivyo kufungua changamoto ya utawala bora. Hivyo, Kamati inaitaka Serikali kuhakikisha kwamba katika mwaka wa fedha 2025/2026 ni lazima Serikali itenge bajeti kwa ajili ya ununuzi wa midaki ya mizigo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupunguza matumizi ya Serikali yasiyo ya lazima. Ni muda sasa Serikali imekuwa ikitanabaisha dhamira yake ya kupunguza matumizi ya Serikali yasiyo ya lazima. Hata hivyo, uchambuzi wa Kamati umebaini kwamba, hakuna maelekezo yoyote mahususi kwa Maafisa Masuuli ya kupunguza matumizi yasiyo ya lazima. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali kuunda

timu chini ya Wizara ya Fedha itakayohusisha wataalamu kutoka Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi, Tume ya Mipango na Ofisi ya Waziri Mkuu pamoja Wizara, Idara na Mamlaka yoyote kadri itakavyoonekana inafaa ili kupitia matumizi ya Serikali na kutoa mapendekezo ni matumizi yapi yanaweza kupunguzwa bila kuathiri utendaji kazi wa Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa mpango huu ni wa mwisho katika mfululizo wa mipango ya miaka mitano na tunakwenda sasa kuwa na mpango wa kwanza wa dira inayotarajiwa ya mwaka 2050, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, anakwenda kutengeneza historia nyingine. Hii ni historia ya kuliongoza Taifa katika kuandaa dira ya miaka mitano ijayo. Hii ni historia nyingine anayokwenda kuiandika. Mheshimiwa Rais, hongera sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, nitumie fursa hii kukupongeza kwa namna unavyoiwakilisha Tanzania kwenye medani za kimataifa hasa ukiwa Rais wa Umoja wa Mabunge Duniani *(IPU)*. Hakika umethibitisha uwezo wako kwa Taifa na Kimataifa katika kusimamia shughuli za Kibunge. Aidha, napenda kumshukuru Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu, Mbunge na Naibu Spika, kwa ushirikiano wake na Kamati katika kipindi chote cha utendaji kazi wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, nitumie fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Mbunge na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, pamoja na Mheshimiwa Dkt. Doto Mashaka Biteko, Mbunge na Naibu Waziri Mkuu, kwa namna wanavyosimamia utendaji kazi wa Serikali. Haya mafanikio yote tunayoyasema ni sehemu ya utendaji wao wa kazi na wao wameonesha alama kubwa katika haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya kipekee naomba niwashukuru Mheshimiwa Prof. Kitila Mkumbo, Mbunge na Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Mipango na Uwekezaji, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba, Mbunge na Waziri wa Fedha pamoja na Mheshimiwa Hamad Hassan Chande, Mbunge na Naibu Waziri wa Fedha kwa ushirikiano wao na Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Kamati inampongeza Mheshimiwa Stanslaus Nyongo, Mbunge na Naibu Waziri, Ofisi ya Rais Mipango na Uwekezaji kwa kuteuliwa kuwa Naibu Waziri na kwa ushiriki wake kwenye mchakato wa Kamati yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inawashukuru Dkt. Tausi Kida, Katibu Mkuu Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, Bi. Jenifa Omolo, Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Fedha, Dkt. Milanzi, Kaimu Katibu Mtendaji wa Tume ya Mipango, pamoja na Watendaji wa Tume ya Mipango na Wizara ya Fedha kwa kushirikiana na Kamati wakati wa majadiliano ya Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo ya Mwaka 2025/2026 pamoja na Mwongozo wa Uandaaji wa Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwapongeza Wajumbe wa Kamati wakiongozwa na Mheshimiwa Twaha Ally Mpembenwe, Mbunge wa Kibiti na Makamu Mwenyekiti wa Kamati kwa umahiri na ushirikiano wao katika kuchambua Mpango na Mwongozo wa kuboresha hadi kufikia hatua hii. Naomba kuwatambua Wajumbe hao kama majina yao yanavyoonekana kwenye Taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya kipekee ninamshukuru pia Ndg. Baraka Ildephonce Leonard, Katibu wa Bunge, kwa niaba ya watumishi wote kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kikamilifu. Naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

## TAARIFA YA KAMATI YA BUNGE YA BAJETI KUHUSU MAPENDKEZO YA MPANGO WA MAENDELEO WA TAIFA WA MWAKA 2025/26 PAMOJA NA MAPENDEKEZO YA MWONGOZO WA MAANDALIZI YA MPANGO NA BAJETI YA SERIKALI KWA MWAKA 2025/26 - KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

### 1.0. UTANGULIZI

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, kwa mujibu wa Kifungu cha 9(1) kipengele (a) cha Sheria ya Bajeti Sura 439 pamoja na Kanuni ya 113 (4) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Februari, 2023

naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti kuhusu Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2025/26 pamoja na Mapendekezo ya Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2025/26.

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2025/26 ni Mpango wa mwisho katika mfululizo wa utekelezaji wa Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2021/22-2025/26) uliobeba Dhima ya "Kujenga Uchumi Shindani na Viwanda kwa Maendeleo ya Watu".

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Kamati imefanya uchambuzi wa kina wa Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa mwaka 2025/26 pamoja na Mapendekezo ya Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2025/26 kama ilivyowasilishwa na Serikali na kutoa ushauri wake. Uchambuzi wa Kamati ulifanyika kwa kurejea nyaraka zifuatazo:-

(i) Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa miaka mitano (2021/22-2025/26);

(ii) Ilani ya Chama cha Mapinduzi (CCM) kwa ajili ya uchaguzi mkuu wa mwaka 2020;

(iii) Taarifa ya utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2022/23; iv. Tathmini ya Utekelezaji wa Dira ya Maendeleo ya Taifa ya Mwaka 2025;

(iv) Taarifa ya Hali ya Uchumi wa Dunia ya mwezi Oktoba, 2024 inayotolewa na Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF); na

(v) Nyaraka na miongozo mbalimbali ya Serikali inayohusu uandaaji wa Mipango na Bajeti.

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, Taarifa hii imegawanyika katika sehemu kumi. Sehemu ya kwanza ni Utangulizi, Sehemu ya pili ni Mapitio ya Hali ya Uchumi, sehemu ya tatu ni Mapitio ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo ya Mpango kwa Mwaka – 2023/24 na Robo ya Kwanza 2024/25, sehemu ya nne ni Ugharamiaji wa Mpango wa Maendeleo kwa Mwaka 2025/26, sehemu ya tano ni Maeneo

ya Kipaumbele ya Mpango kwa Mwaka 2025/26, sehemu ya sita ni Makadirio ya Bajeti kwa mwaka 2025/26, sehemu ya saba ni Usimamizi wa vihatarishi vya utekelezaji wa Mpango na Bajeti, sehemu ya nane ni Maoni ya jumla kuhusu Mwongozo wa Mpango na Bajeti kwa Mwaka 2025/26, sehemu ya tisa ni Maoni ya ujumla na sehemu ya kumi ni Hitimisho.

## 2.0. MAPITIO YA HALI YA UCHUMI

### *2.1. UCHAMBUZI WA VIASHIRIA VYA UCHUMI JUMLA*

#### 2.1.1. Ukuaji wa Uchumi wa Dunia

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, kwa mujibu wa taarifa ya Shirika la Fedha la Kimataifa - IMF *World Economic Outlook* – WEO, toleo la Oktoba 2024, uchumi wa dunia ulikua kwa wastani wa **asilimia 3.3** mwaka 2023 ikilinganishwa na **asilimia 3.5** mwaka 2022 na unatarajiwa kukua kwa **asilimia 3.2** na **asilimia 3.3** mwaka 2024 na 2025 mtawalia. Aidha, taarifa hiyo kwa nchi zilizoendelea inaonyesha kwamba uchumi ulikua kwa wastani wa **asilimia 1.7** mwaka 2023 ikilinganishwa na **asilimia 2.6** mwaka 2022 na unatarajiwa kukua kwa **asilimia 1.7** na **asilimia 1.8** mwaka 2024 na 2025, mtawalia. Kwa upande wa nchi zinazoibukia kiuchumi na zinazoendelea, uchumi ulikua kwa wastani wa **asilimia 4.4** mwaka 2023 ikilinganishwa na **asilimia 4.1** mwaka 2022. Uchumi wa nchi hizo unatarajiwa kukua kwa wastani wa **asilimia 4.3** mwaka 2024 na 2025.

**Jedwali Namba 1. Mwenendo wa Ukuaji wa Uchumi wa Dunia**

| Mwaka | Ukuaji wa Uchumi wa Dunia (Asilimia) |
|---|---|
| 2021 | 6.3 |
| 2022 | 3.5 |
| 2023 | 3.3 |
| 2024 | 3.2* |
| 2025 | 3.3* |

**Chanzo:** *IMF World Economic Outlook* – WEO, *Toleo la Oktoba, 2024*

*** = Matarajio**

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** mambo mengine yaliyoainishwa katika Taarifa ya IMF ni kama ifuatavyo:-

(i) Bei za mlaji duniani (World consumer prices) kwa nchi zinazoendelea na kuibukia kiuchumi zinatarajiwa kushuka kutoka **asilimia 8.1** ya mwaka 2023 hadi **asilimia 7.9** mwaka 2024 na **asilimia 5.9** mwaka 2025. Hali hii inaashiria kwamba katika kipindi husika mfumuko wa bei utapungua. Vilevile, uwezo wa watu kununua bidhaa na huduma utaongezeka;

(ii) Migogoro na mivutano ya kisiasa kwa Ulaya Mashariki na Mashariki ya Kati, itasababisha kuvurugika kwa mnyororo wa ugavi pamoja na kuongezeka kwa gharama ya usafirishaji majini *(Freight Charges)*. Mfano, badala ya meli kupita katika Mfereji wa Suez zitalazimika kupita katika Rasi ya Tumaini Jema ambapo itaongeza gharama ya usafirishaji kutokana na umbali kwa wastani wa **Dola za Marekani 300,000** kwa safari moja; na iii. Uchumi wa nchi zilizoendelea unatarajiwa kukua kwa kasi ndogo ya **asilimia 1.7** na **asilimia 1.8** mwaka 2024 na 2025 mtawalia.

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** kutokana na takwimu za mwenendo wa ukuaji wa uchumi wa dunia, Kamati inatoa ushauri ufuatao kwa Serikali:-

(i) Kutumia fursa hizo kuongeza uzalishaji wenye tija wa mazao ya kilimo na biashara ikiwemo maua na mboga mboga ili kuongeza mauzo nje ya nchi pamoja na kuchochea ukuaji wa sekta ya utalii;

(ii) Kuongeza ufanisi wa utendaji kazi wa Bandari zetu ili kupunguza gharama zinazotokana na meli kukaa bandarini kwa muda mrefu (Demurrage charges) na hivyo kuongeza gharama za bidhaa zinazoingizwa nchini;

(iii) Serikali iweke mkazo katika kuboresha makusanyo ya ndani ili kupunguza nakisi inayoweza kujitokeza kutokana na uwezekano wa kupungua kwa misaada kutoka nchi wahisani; na


(iv) Kuboresha mazingira ya biashara ili kuvutia mitaji ya uwekezaji.

**2.1.2. Ukuaji wa Uchumi wa Nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara**

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** uchambuzi wa Kamati umebaini kwamba ukuaji wa uchumi kwa nchi zilizo Kusini mwa jangwa la Sahara umeshuka kutoka wastani wa **asilimia 4.7** mwaka 2021 hadi **asilimia 3.4** mwaka 2023. Hata hivyo, uchumi wa nchi hizi unatarajiwa kukua kwa wastani wa **asilimia 3.7** mwaka 2024 na **asilimia 4.1** mwaka 2025. Aidha, katika kipindi cha miaka 3 kuanzia mwaka 2022 hadi 2024 nchi ya Ushelisheli, Mauritius na Jamhuri ya kidemokrasia ya Kongo zimekuwa zikifanya vizuri katika ukuaji wa uchumi ikilinganishwa na Tanzania pamoja na kwamba mfumuko wa bei wa nchi hizo umekuwa juu kuliko Tanzania.

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** sekta zilizosaidia nchi hizo kukua kiuchumi ni sekta ya Madini kwa Jamhuri ya kidemokrasia ya Kongo, sekta za Utalii na Uchumi wa buluu kwa nchi za Ushelisheli na Mauritius. Kwa kuwa sekta hizo zote zinapatikana nchini, Kamati inaishauri Serikali kuboresha mazingira ya uwekezaji ili kuvutia uwekezaji kwenye sekta za Madini, Maliasili na Utalii pamoja na uchumi wa buluu nchini ili kuchochea ukuaji wa uchumi.

**Kielelezo Namba 1: Ukuaji wa Uchumi kwa Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC)**




***Chanzo:*** *Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF), Julai 2024*


### 2.1.3. Mwenendo wa Ukuaji wa Uchumi kwa Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC)

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** uchumi wa nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki - EAC, ulikua kwa wastani wa **asilimia 4.6** mwaka 2023 ikilinganishwa na **asilimia 4.2** mwaka 2022 na unatarajiwa kukua kwa wastani wa **asilimia 5.4** mwaka 2024 na **asilimia 6.1** mwaka 2025. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali mambo yafuatayo:-

i. Jumuiya ya Afrika Mashariki ina jumla ya watu **milioni 302.2.** Hivyo, Tanzania itumie fursa hiyo kama soko la kuzalisha na kuuza bidhaa ambazo Tanzania ina nguvu ya ushindani kama vile bidhaa za kilimo, mifugo, uvuvi madini na utalii; na

ii. Kuboresha mazingira ya uwekezaji wa ndani ili kuvutia wawekezaji ambao watataka kutumia Tanzania kama kitovu cha kuingia katika soko la pamoja la Jumuiya ya Afrika Mashariki hasa kwa sekta ambazo Tanzania ina nguvu ya soko la ushindani.

**Kielelezo Namba 2: Mwenendo wa Ukuaji wa Uchumi kwa Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC)**




***Chanzo:*** *Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF), Julai 2024*

### 2.1.4. Mfumuko wa Bei

#### 2.1.4.1. Mfumuko wa Bei wa Dunia, Nchi zilizoendelea na zinazoibukia kiuchumi

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** mwenendo wa mfumuko wa bei duniani unaonyesha kwamba mfumuko wa bei umeendelea kupungua kutoka wastani wa **asilimia 8.7** mwaka 2022 hadi **asilimia 6.7** mwaka 2023. Aidha, mfumuko wa bei wa dunia unatarajiwa kupungua na kufikia wastani wa **asilimia 5.9** mwaka 2024 na **asilimia 4.4** mwaka 2025. Kwa nchi zilizoendelea mfumuko wa bei ulipungua kutoka **asilimia 7.3** mwaka 2022 na kufikia wastani wa **asilimia 4.6** mwaka 2023. Aidha, mfumuko wa bei kwa nchi hizi unatarajiwa kupungua kutoka **asilimia 5.8** mwaka 2024 hadi **asilimia 4.4** mwaka 2025.

Mfumuko wa bei kwa nchi zinazoendelea na zinazoibukia kiuchumi ulipungua kutoka wastani wa **asilimia 9.8** mwaka 2022 hadi kufikia wastani wa **asilimia 8.1** mwaka 2023. Aidha, mfumuko huu wa bei unatarajiwa kuongezeka na kufikia wastani wa **asilimia 7.9** mwaka 2024 na kisha kupungua hadi kufikia wastani wa **asilimia 5.9** mwaka 2025.

#### 2.1.4.2. Mfumuko wa Bei kwa Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** kwa nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki mfumuko wa bei umeongezeka na kufikia wastani wa **asilimia 16.9** mwaka 2023, ikilinganishwa na **asilimia 8.3** mwaka 2022. Nchi za Tanzania, Kenya na Uganda ni nchi pekee zilizoendelea kuwa na viwango vya mfumuko wa bei ulio ndani ya lengo la Jumuiya la kati ya **asilimia 3.0** hadi **7.0** kwa mwaka. Kwa Tanzania mfumuko wa bei ulikuwa **asilimia 3.2** mwaka 2023/24, ikilinganishwa na asilimia 4.7 ya mwaka 2022/23, kiwango ambacho kipo ndani ya lengo la nchi la **asilimia 5.0** sawa na malengo ya mtangamano wa kiuchumi kikanda.

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** kufuatia mwenendo wa mfumuko wa bei Kamati inatoa ushauri ufuatao:-

(i) Serikali kuiwezesha kifedha Mamlaka ya Hifadhi ya Chakula Nchini (NFRA) pamoja na Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko (CPB) ili ziweze kuhifadhi akiba ya kutosha ya chakula na hivyo kudhibti mfumuko wa bei. Ushauri huu unatokana na tahadhari iliyotolewa kuhusu mabadiliko ya tabianchi yanayoweza kuathiri shughuli za kilimo kwa mwaka 2024 na 2025;

(ii) Serikali kuchukua hatua stahiki kupunguza mfumuko wa bei kutokana na tahadhari ya kuongezeka kwa bei za mafuta katika soko la dunia kwa **asilimia 0.9** sawa na **dola za Marekani 81** kwa pipa pamoja na kuanzisha mkakati wa kuhifadhi akiba ya mafuta (Strategic oil reserve) ili kuiwezesha nchi kununua mafuta pindi bei zinaposhuka na kuyatumia pindi bei zinapopanda. Ushauri huu wa Kamati unatokana na taarifa ya Umoja wa Nchi zinazozalisha mafuta na kuuza nje (Organization of the Petroleum Exporting Countries - OPEC) na nchi nyingine zisizokuwa wanachama ikiwemo Urusi; na

(iii) Serikali iweke mkakati wa uzalishaji wa mazao ya chakula yenye mahitaji makubwa katika soko la dunia. Ushauri huu wa Kamati unatokana na ukweli kwamba katika kapu la Bidhaa na Huduma, vyakula na vinywaji baridi vinabeba uzito wa **asilimia 28.2** ambayo ni kubwa kuliko bidhaa nyingine.

**2.2. Ukuaji wa Uchumi wa Taifa**

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Taarifa ya Serikali inaonyesha kwamba kwa mwaka 2023, Pato halisi la Taifa kwa bei za mwaka 2015 lilikua na kufikia **shilingi Trillioni 148.39** kutoka **shilingi Trillioni 141.25** mwaka 2022, sawa na ukuaji wa **asilimia 5.1** ikilinganishwa na **asimilia 4.7** mwaka 2022. Shughuli za kiuchumi zilizochangia ukuaji huu ni shughuli za kilimo, ujenzi na uchimbaji madini ya thamani na vito.

**Jedwali Namba 2: Ukuaji wa pato la Taifa kwa baadhi ya shughuli za kiuchumi katika kipindi cha Januari hadi Juni kwa mwaka 2023 na 2024 (asilimia)**

| Sekta | Mwaka2023 Ukuaji-(Asilimia) | Mwaka 2024 Ukuaji-(Asilimia) |
|---|---|---|
| Afya | 6.1 | 4.0 |
| Elimu | 6.7 | 4.4 |
| Utawala na Ulinzi | 6.3 | 6.6 |
| Fedha na Bima | 11.2 | 16.6 |
| Habari na Mawasiliano | 4.8 | 12.3 |
| Malazi na Chakula | 9.7 | 6.3 |
| Usafirishaji na Uhifadhi wa Mizigo | 3.1 | 6.7 |
| Biashara na Matengenezo | 3.4 | 4.8 |
| Ujenzi | 3.6 | 4.6 |
| Umeme | 4.9 | 9.3 |
| Viwanda | 4.8 | 5.2 |
| Uchimbaji na Mawe Madini | 12.3 | 5.0 |
| Kilimo | 4.0 | 3.6 |
| **Jumla ya Ukuaji wa Pato la Taifa** | **4.8** | **5.4** |

**Chanzo:** *Ofisi ya Taifa ya Takwimu*

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** kufuatia ukuaji huo, Kamati inashauri Masuala yafuatayo:-

(i) Takwimu zinaonyesha kwamba sekta za huduma zimekuwa kwa kasi ukilinganisha na Sekta za uzalishaji kwa sababu ya uwekezaji mkubwa wa Serikali. Kamati inaishauri Serikali kuweka uwiano sawa wa uwekezaji baina ya sekta ya huduma na sekta ya uzalishaji ili sekta za uzalishaji nazo zikuwe kwa kasi na kuchochea ukuaji wa uchumi ili kufikia lengo la **asilimia 8 hadi 10** kama ilivyotarajiwa katika Dira ya Maendeleo ya Taifa ya mwaka 2025;

(ii) Serikali kuhakikisha kwamba inawekeza kikamifu katika kukuza sekta zenye mchango mkubwa katika pato la Taifa. Kuna haja ya kuhakikisha kwamba bajeti ya sekta ya kilimo inatolewa kwa wakati na miradi inakamilika kwa wakati kwa sababu sekta ya kilimo huchangia **asilimia 26.5** ya Pato la Taifa; na

(iii) Serikali kulipa madeni ya wakandarasi kwa wakati ili wakamilishe miradi mapema na kwa ubora. Hatua hii itasaidia kuongeza mchango wa sekta ya ujenzi ambapo kwa sasa ni **asilimia 13.2**.

***2.3. Sekta ya Nje***

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, Kamati imebaini kwamba urari wa malipo ya jumla katika mwaka 2023/24 ulikuwa na nakisi ya **dola za Marekani milioni 204** ikilinganishwa na ziada ya **dola za Marekani milioni 273.5** ya mwaka 2022/23. Jedwali Na. 3 linaonyesha mwenendo wa Sekta ya Nje.

**Jedwali Namba 3: Urari wa Jumla Wa Huduma,Bidhaa Na Mtaji (2019/20-2023/24)**

| Urari wa Jumla Wa Huduma,Bidhaa Na Mtaji | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | Milioni za Dola za Marekani (USD) | | | | |
| **Akaunti** | **2019/20** | **2020/21** | **2021/22** | **2022/23** | **2023/24** |
| urari wa malipo ya kawaida | (1,317.1) | (1,809.1) | (3,450.4) | (4,955.6) | (2,469.5) |
| Urari wa Uhamisho na Mitaji | 361.9 | 397.9 | 328.7 | 284.5 | 224.0 |
| Urari wa Rasilimali Fedha | 2,217.7 | 2,582.7 | 2,970.2 | 4,079.1 | 3,634.5 |
| Menineyo | (507.5) | (970.7) | 150.4 | 865.5 | (1,593.3) |
| **Urari wa Malipo ya Jumla** | **755.0** | **200.8** | **(1.1)** | **273.5** | **(204.3)** |

***Chanzo:*** Benki Kuu ya Tanzania, 2024

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** kutokana na taarifa za Urari wa malipo, Kamati inaishauri Serikali yafuatayo:-


(i) Kuhamasisha uzalishaji wa bidhaa zilizoongezwa thamani ili kuzuia uagizwaji wa bidhaa hizo kutoka nje; na

(ii) Kuweka mazingira wezeshi kwa sekta ya madini ili kuchochea ukuaji wa sekta hiyo kwa kuongeza migodi. Vilevile, sekta ya madini imechangia **asilimia 9.0** ya pato la Taifa na imekuwa na ukuaji wa **asilimia12.3**. Hatua hii itasaidia mauzo nje na kupunguza nakisi ya urari.

### *2.4. Deni la Serikali*

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** uchambuzi wa Kamati umebaini kwamba hadi Juni 2024, deni la Serikali lilikuwa **shilingi Trilioni 96.88** ikilinganishwa na **shilingi Trilioni 81.98** katika kipindi kama hicho mwaka 2023, sawa na ongezeko la **asilimia 18.18** (**Trilioni 14.90**). Katika deni la sasa la shilingi **Trilioni 96.88**, deni la ndani lilikuwa shilingi **Trilioni 31.95** na deni la nje lilikuwa shilingi **Trilioni 64.93**. Uchambuzi wa Kamati umebaini kwamba mpaka sasa Deni la Serikali ni himilivu kwa kipindi kifupi, cha kati na kirefu. Ongezeko la deni limesababishwa na kushuka kwa thamani ya shilingi pamoja na kupokea mikopo mipya kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo.

**Kielelezo Namba 3: Mwenendo wa Deni la Serikali**




**Chanzo:** Wizara ya Fedha

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** licha ya kwamba Deni la Serikali ni himilivu kwa muda mfupi, wa kati na mrefu, Kamati inaishauri Serikali kufanya yafuatayo ili kuhakikisha deni hili linaendelea kuwa himilivu:-

(i) Kuongeza wigo na ukusanyaji wa mapato ya ndani ili yawe na uwezo wa kugharamia deni;

(ii) Mikopo yote inayopatikana ni vema Serikali ikaielekeza katika miradi inayochochea kasi ya ukuaji wa uchumi na mauzo ya bidhaa na huduma nje ya nchi, ili kuhakikisha kwamba hatufiki kwenye ukomo wa ulipaji wa deni la nje kwa uuzaji wa bidhaa nje ambao hivi sasa tupo **asilimia 11.1** na ukomo ni **asilimia 15**;

(iii) Kutoa kipaumbele kwa mikopo yenye masharti nafuu na yenye masharti ya kati ili kupunguza mzigo wa riba pamoja na muda mfupi wa neema ambao unaambatana na mikopo ya kibiashara; na

(iv) Kutafuta vyanzo vingine bunifu vya mapato kama vile hatifungani za kijani, diaspora, manispaa na miundombinu.

### *2.5. Hali ya Umaskini na Maendeleo ya Watu*

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Dira ya Maendeleo ya Taifa ya 2025 ilibainisha kwamba ili Tanzania iondokane na umaskini ni lazima uchumi ukue kwa **asilimia 8** hadi **10**. Kamati inaipongeza Serikali kwa kuendelea kutekeleza Sera, programu na miradi mbalimbali yenye lengo la kupunguza umaskini na kuchochea maendeleo ya watu.

Hata hivyo, Kamati inaishauri Serikali masuala yafuatayo:-

(i) Sekta ya kilimo ina uhusiano mkubwa na hali ya umaskini nchini ambapo jumla ya watu **milioni 28** sawa na **asilimia 45.9** ya watu wote Tanzania wanajishughulisha na sekta ya kilimo. Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kwamba inakamilisha miradi yote ya kilimo kwa wakati ili kupunguza hali ya umaskini nchini. Mfano, mradi wa Kujenga Kesho iliyo

Bora (Building a Better Tommorow - BBT) na ujenzi wa mabwawa ya umwagiliaji;

(ii) Kamati inaishauri Serikali kutenga bajeti kwa mwaka wa fedha 2025/26 kwa ajili ya kufanya utafiti wa mapato na matumizi ya kaya ili kupata takwimu ya hali ya umaskini nchini kwa kuangalia viashiria vyote 17. Taarifa iliyopo hivi sasa ya hali ya umaskini ni ya mwaka 2017/18, hivyo imepitwa na wakati; na

(iii) Kwa mujibu wa Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2022, idadi ya watu ilikuwa ni 61,741,120 mwaka 2022 na inakadiriwa kuwa, ifikapo mwaka 2035 idadi ya watu nchini itakuwa 87,509,630 kutokana na ongezeko la watu la **asilimia 3.2** kila mwaka. Ongezeko hili la idadi ya watu nchini haliendani na ukuaji wa uchumi. Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kwamba ongezeko la watu linaendana na ukuaji wa uchumi kwa sababu hivi sasa kati ya watu **100** watu **87** ni tegemezi**;** na

(iv) Kutoa ruzuku ya kipekee kwa watu wenye ulemavu ili kuweka usawa wa fursa na kujitegemea kiuchumi;

## 3.0. MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO YA MPANGO KWA MWAKA 2023/24 NA ROBO YA KWANZA YA MWAKA 2024/25

### 3.1. UCHAMBUZI KUHUSU MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, Kamati imefanya uchambuzi wa utekelezaji wa Vipaumbele vya Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano katika Mwaka 2023/24 na Utekelezaji katika Kipindi cha Robo ya Kwanza Mwaka 2024/25. Miradi iliyofanyiwa uchambuzi ni miradi 17 inayolenga kuleta matokeo katika maeneo 5 ya kipaumbele ya mpango wa Tatu wa Maendeleo, malengo hayo ni:-

(i) Uchumi shirikishi na shindani;
(ii) Kuongeza uzalishaji viwandani na utoaji wa huduma;

(iii) Kukuza uwekezaji na biashara;
(iv) Maendeleo ya watu; na
(v) Kuendeleza rasilimali watu.

**3.1.1. Uchambuzi wa utekelezaji wa miradi**

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, uchambuzi wa miradi ya kipaumbele kwa kina ni kama ifuatavyo:-

**3.1.1.1. Ujenzi wa Madaraja Makubwa ya juu**

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, miundombinu ina mchango mkubwa katika kuchochea uzalishaji na usafirishaji wa bidhaa. Kamati imechambua ujenzi wa daraja la Kigongo – Busisi ambalo utekelezaji wake umefikia **asilimia 93** na linatarajiwa kumalizika mwaka 2025 pamoja na madaraja ya juu jijini Dar es Salaam. Kukamilika kwa madaraja haya kutaongeza ufanisi katika shughuli za kiuchumi, kukuza biashara na kuvutia uwekezaji.

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Kamati inaipongeza Serikali kwa kutekeleza miradi hiyo. Hata hivyo, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha daraja la Kigongo - Busisi linakuwa la kulipia (toll bridge) ili kupata fedha zitakazotumika katika kufanya ukarabati wa daraja hilo. Aidha, Serikali iandae Sera ya tozo kwa ajili ya matumizi ya madaraja (toll bridge) ili kuvutia uwekezaji wa sekta binafsi. Vilevile, fedha zitakazokusanywa katika tozo ziwekwe katika Mfuko Maalumu utakaolindwa (Ring Fenced Fund) ili zitumike kwa malengo yaliyokusudiwa.

**3.1.1.2. Ujenzi wa Reli ya Kisasa kwa Kiwango cha Kimataifa (SGR):**

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, Kamati imefanya uchambuzi kuhusu utekelezaji wa mradi huu na kubaini masuala yafuatayo:-

(i) Serikali itumie mpango wa kufadhili ujenzi wa Reli ya Kisasa ya SGR kwa kutumia ECGA (Export Credit Guarantee Agency) ili kukamilisha vipande vyote vilivyobaki kwa haraka hususan vipande vya Uvinza - Malagarasi- Msongati na Kaliua- Mpanda- Karema;

(ii) Serikali itumie fursa ya uwepo wa Sheria ya mfumo wa kukaribisha sekta binafsi kutumia miundombinu ya reli kwa makubaliano ya malipo (*Open Access*) ili kuvutia wawekezaji katika reli ya SGR;

(iii) Reli ya MGR itafutiwe uwekezaji ili iendeshwe kwa ufanisi;

(iv) Kutenganisha usimamizi wa reli ya Kisasa ya SGR na reli ya MGR na kulifanya Shirika la TRC kuwa Shirika Hodhi linalosimamia Mashirika mawili. Shirika linalosimamia reli ya SGR na lingine linalosimamia reli ya MGR;

(v) Ujenzi wa reli uende sambamba na ujenzi wa bandari kavu katika maeneo mbalimbali ili mizigo inapotoka bandarini ihifadhiwe kwenye bandari kavu na hivyo kuongeza ufanisi wa bandari; na vi. Ujenzi wa vituo vya reli uende sambamba na ujenzi wa miundombinu ya kuziunganisha na barabara ili kurahisisha usafiri wa abiria.

**Jedwali Namba 4: Uchangiaji wa SGR kwenye Pato la Taifa ukilinganisha Tanzania, Kenya na Ethiopia mwaka 2023**

| Na. | Nchi | Pato laTaifa(%) | Maelezo |
|---|---|---|---|
| 1. | Kenya | 1.5 | Hii imetokana na usafirishaji wa mizigo kutoka bandari ya Mombasa hadi maeneo mengine ya ndani. |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 2. | Ethiopia | 1 | Reli ya kisasa inachangia kwa ufanisi katika usafirishaji wa bidhaa za kimataifa kupitia bandari ya Djibouti, hivyo kusaidia uchumi wa nchi. |
| 3. | Tanzania | 0.3 | Mchango wa SGR ulikuwa mdogo kwa sababu ya kutosafirisha mizigo |

**Chanzo:** *Taarifa za Mashirika ya Reli ya Kenya, Ethiopia na Tanzania*

**3.1.1.3. Ununuzi wa Meli na Ujenzi wa Bandari ya Uvuvi**

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, Kamati imefanya uchambuzi kuhusu mradi wa ujenzi wa bandari ya uvuvi ambao umefikia **asilimia 70** na ununuzi meli za uvuvi. Kwa upande wa ununuzi wa meli, hatua iliyofikiwa ni kukamilika kwa upembuzi yakinifu wa uendeshaji wa meli za uvuvi. Kamati inaipongeza Serikali kwa kuwa na mikakati ya kukuza sekta ya uvuvi ili nchi inufaike na rasilimali za bahari kwa lengo la kukuza uchumi wa buluu. Baada ya uchambuzi Kamati ina ushauri ufuatao:-

(i) Ujenzi wa bandari ya uvuvi uende sambamba na kuweka mazingira ya biashara nyingine zinazoendana na Bandari ya uvuvi kama vile maeneo ya kuchagulia (*sorting area)*, kuhifadhia na kuchakata samaki. Aidha, ujenzi wa bandari uende sambamba na ujenzi wa miundombinu ya Kanda maalumu ya mauzo nje (EPZ na SEZ) ili kusaidia usindikaji wa mazao ya samaki na kuyauza nje;

(ii) Serikali iharakishe ununuzi wa meli za uvuvi ili ujenzi wa bandari utakapokamilika meli nazo ziwe tayari kutumika; na

(iii) TAFICO isitegemee fedha za Serikali pekee katika kununua meli na badala yake ishirikishe Sekta binafsi, kununua meli nyingi zaidi kwa kupitia mfumo wa Ubia baina ya Sekta Binafsi na Sekta ya Umma *(Public Private Partnership)*.

### 3.1.1.4. Kuboresha Shirika la Ndege

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, Kamati imefanya uchambuzi wa mradi wa kufufua Shirika la ndege la Tanzania na kubaini kwamba hadi mwaka 2023/24, ndege 16 kati ya 19 zimenunuliwa, sawa na **asilimia 84.2** ya lengo. Uwekezaji wa ATCL una faida kubwa kwa Taifa kama vile kukuza usafirishaji wa watalii pamoja na usafirishaji wa mazao ya kilimo na bidhaa nyingine. Kamati imebaini kwa mwaka 2023 mchango wa ATCL kwenye Pato la Taifa ni chini ya **asilimia 1**, ikilinganishwa na nchi nyingine kama Kenya ambapo Shirika la Ndege la Kenya linachangia **asilimia 3** na Ethiopia **asilimia 5.7**.

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Kamati inaishauri Serikali, kuongeza safari za ndege kwenye maeneo ambayo tuna uhusiano mkubwa wa kibiashara sambamba na kuboresha viwanja vya ndege vya ndani kwa kuviwekea taa ili kuongeza idadi ya miruko ya ndege za ATCL ndani ya nchi. Vilevile, Serikali iongeze ndege ya mizigo ili kuongeza uhakika wa kusafirisha mizigo kwenda nje.

**Jedwali Namba 5: Mchango wa Sekta ya Anga kwenye Pato la Taifa**

| Na. | **Nchi** | **Mchango kwenye Pato la Taifa 2023** | **Sababu** |
|---|---|---|---|
| 1. | Ethiopia Airlines | 5.7% | i. Shirika lina uzoefu wa muda mrefu (miaka 78);<br>ii. Wingi wa ndege (146) na miruko;<br>iii. Matangazo mengi ya biashara. |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 2. | Kenya Airlines | 3% | i. Umri wa Shirika ni miaka 47;<br>ii. Ndege 36, miruko ya nje 54;<br>iii. Matangazo mengi. |
| 3. | ATCL | 1% | i. Umri mdogo wa Shirika (miaka 8);<br>ii. Ndege chache (16), ya mizigo 1 na miruko ya nje 12;<br>iii. Matangazo machache. |

**Chanzo**:*Taarifa za Mashirika ya ndege ya Ethiopia, Kenya na ATCL.*

**3.1.1.5. Miundombinu ya Nishati**

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, Kamati imefanya uchambuzi na kubaini kiwango cha matumizi ya umeme nchini kwa mtu mmoja kwa mwaka ni **kwh 108** ikilinganishwa na wastani wa nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara ambao ni **kwh 550** kwa mwaka na duniani ni **kwh 2500** kwa mwaka. Takwimu zinaonyesha kwamba wananchi wengi wanatumia umeme kwa ajili ya matumizi madogo ya nyumbani hususan kuwasha taa wakati wa usiku badala ya uzalishaji.

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Kamati inatambua juhudi zinazofanywa na Serikali katika kuongeza uzalishaji wa umeme nchini ikiwa ni pamoja na kukamilisha ujenzi wa mradi wa Bwawa la Umeme la Mwalimu Julius Nyerere ambalo hivi sasa linaingiza katika gridi ya Taifa **MW 1,175** na hivyo kufanya uzalishaji wa umeme nchini kufikia **Megawati 3,113.35** sawa na ongezeko la **asilimia 61**. Uchambuzi wa miradi katika sekta ya Nishati umebaini masuala yafuatayo ambayo Kamati imeyatolea mapendekezo:-

(i) Kamati inaishauri Serikali kupitia Shirika la TANESCO kutumia fursa ya uwekezaji kwa njia ya Ubia ili kuendeleza miradi kama ile ya Ruhudji (MW 358) na Rumakali (MW 222) kuliko kusubiria fedha za bajeti pekee.;

(ii) Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kwamba miundombinu ya usambazaji wa umeme inaimarishwa ili kuimarisha upatikanaji wa umeme kwa Wananchi. Hivi sasa Taifa lina

ziada ya umeme wa **Megawati 606.04**. Hata hivyo, ziada hiyo inaweza kuwa inatokana na wananchi wengi kutounganishwa kwenye gridi ya taifa na kutowafikia wananchi kutokana na ubovu wa miundombinu;

(iii) Kamati inaishauri Serikali kukamilisha mapema iwezekanavyo majadiliano na Kampuni za Kimataifa za Nishati (International Energy Companies- IECs) ili mradi wa LNG utekelezwe kwa wakati. Majadiliano ya miradi ya Kimkakati yanachukua muda mrefu jambo linaloongeza gharama za utekelezaji wa miradi na kuikosesha nchi fursa muhimu;

(iv) Serikali iongeze vituo vya kujaza gesi katika Jiji la Dar es Salaam, na kuendelea na mradi wa usambazaji wa gesi kwa matumizi ya nyumbani na viwandani;

(v) Serikali iwekeze katika vyanzo vingine vya nishati kama nishati ya joto ardhi (Geothermal) ili kuongeza kiwango cha nishati ya umeme;

(vi) Serikali iimarishe na kutekeleza miradi ya gridi imara ili kuboresha usafirishaji na usambazaji wa umeme;
Upotevu wa umeme hivi sasa ni asilimia 16 juu ya kiwango cha upotevu wa umeme kinachokubalika Kimataifa cha asilimia 4 hadi 10. Hivyo ni wazi kwamba upotevu huu unaliongezea shirika hasara jambo ambalo linaenda sambamba na umuhimu wa kuimarisha gridi ya umeme;

(vii) Kwa upande wa Mkakati wa Taifa wa Matumizi ya Nishati Safi ya Kupikia wa Mwaka 2024 – 2034, Kamati inatambua kwamba mitungi ya gesi zaidi ya 100,000 iligawiwa kwa wananchi. Hata hivyo, Kamati imebaini kwamba wananchi wengi hawana uwezo wa kumudu gharama za kujaza gesi na pia kuna baadhi ya maeneo vituo vya kujaza gesi vipo mbali na wananchi na hivyo kulazimika kutumia fedha nyingi kwenda kujaza gesi. Hivyo basi, ili mradi wa ugawaji wa mitungi uwe endelevu (sustainable), Kamati inashauri Serikali kufanya mapitio ya ada na tozo mbalimbali za gesi ili kupunguza gharama ya gesi ili wananchi waweze kujaza mitungi ya gesi kwa bei nafuu. vilevile, Serikali ipitie mfumo

mzima wa uagizaji na usambazaji wa ili kuhakikisha kwamba gesi inauzwa kwa bei nafuu; na

(viii) Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha wakandarasi wote wanaotekeleza miradi ya umeme vijijini wana uwezo wa kifedha kutekeleza miradi hiyo. Imebaini kuwa wakandarasi wengi wa ndani wana uwe uwezo mdogo wa kifedha na hivyo kuchelewesha utekelezaji wa miradi.

**3.1.1.6. Liganga na Mchuchuma**

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, Kamati ina taarifa kwamba Serikali inafanya majadiliano na mwekezaji wa Kampuni ya Sinchuan Hongda Group (SHG), Kamati inaishauri Serikali kukamilisha mazungumzo mapema na mwekezaji huyo ili mradi huo uanze kutekelezwa na Taifa linufaike.

**3.1.2. Kanda Maalum za Uchumi na Uwekezaji**

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, Kamati imefanya uchambuzi kuhusu maeneo huru ya uzalishaji kwa ajili ya mauzo nje ya Nchi na kubaini kwamba kati ya maeneo 17 yaliyotengwa nchi nzima kwa ajili ya maeneo huru ya uzalishaji (Special Economic Zone - SEZ) na maeneo huru ya uzalishaji kwa mauzo nje (Export Processing Zone – EPZ) ni maeneo mawili tu yameendelezwa, eneo la Bagamoyo na eneo la Benjamin Mkapa. Kamati inaipongeza Serikali kwa kuanza kulipa fidia ya **shilingi bilioni 9.9** katika maeneo mawili ya uwekezaji ya Nala- Dodoma na Songea- Ruvuma. Maeneo mengine 15 yaliyobaki ni mapori na fidia bado hazijalipwa. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali kulipa fidia maeneo hayo pamoja na kuweka miundombinu ya msingi hasa kwenye maeneo ya kimkakati ili yaanze uzalishaji kama ilivyokusudiwa. Vilevile Serikali ijifunze uzoefu wa nchi ya Ethiopia inavyoendesha kanda maalum za kiuchumi.

### 3.1.3. Programu na Miradi ya kimkakati ya kisekta

#### 3.1.3.1. Sekta ya Ujenzi

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** mtandao wa barabara zinazopitika wakati wote za kitaifa na mikoa umeongezeka kutoka **kilometa 32,074.99** mwaka 2021/22 hadi **kilometa 37,225.75** mwaka 2023/24 sawa na ongezeko la **kilometa 5,150.76**. Kamati imefanya uchambuzi na kubaini kuwa sekta ya ujenzi wa barabara inakabiliwa na changamoto zifuatazo:-

(i) Utekelezaji kutokuzingatia ujenzi wa barabara za kimkakati;

(ii) Kuanza ujenzi wa barabara nyingi kwa pamoja bila kuzingatia uwezo wa kifedha;

(iii) Malimbikizo ya madeni ya wakandarasi na kusababisha sehemu kubwa ya bajeti kutumika kulipa madeni ya miaka ya nyuma;

(iv) Uwezo mdogo wa kifedha wa wakandarasi wa ndani katika kushiriki kwenye ujenzi wa barabara unatokana na Serikali kutokulipa madeni au hati za malipo kwa wakati pamoja na riba kubwa ya mikopo inayotozwa na taasisi za kifedha nchini;

(v) Ukosefu wa fedha za kutosha za kufanya ukarabati na matengenezo ya barabara;

(vi) Barabara kujengwa chini ya kiwango, na hivyo kuharibika ndani ya muda mfupi;

(vii) Barabara nyingi hujengwa kwa vipande na hivyo kutokukamilika kwa wakati; na

(viii) Barabara nyingi za vijijini zinajengwa kwa udongo na hivyo kuathirika na mvua za msimu.

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Kamati inaishauri Serikali masuala yafuatayo:-

(i) Serikali kutoa kipaumbele katika ujenzi na ukarabati wa barabara za kimkakati na zenye manufaa makubwa kiuchumi;

(ii) Serikali kutenga fedha za kutosha kila mwaka kwa ajili kufanya ukarabati na matengenezo ya barabara kuu, barabara za mijini na vijijini;

(iii) Serikali irejeshe utaratibu wa zamani wa kuwa na timu za ukaguzi wa barabara mara kwa mara ili kurekebisha maeneo yanayoharibika ili kuzuia uharibifu mkubwa baadaye;

(iv) Serikali kutoa kipaumbele cha kulipa madeni ya wakandarasi wa barabara kwa wakati;

(v) Serikali kuhakikisha inawasilisha fedha zote zinazotokana na vyanzo mahususi *(earmarked sorce)* vya Mfuko wa Barabara kama vilivyokusanywa; na

(vi) Serikali kuhakikisha barabara zinajengwa kwa kuzingatia ubora na viwango vinavyokubalika.

**3.1.3.2. Sekta ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari**

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Kamati inatambua juhudi za Serikali za kuendeleza sekta ya habari na mawasiliano kwa kuanzisha mradi wa ujenzi wa minara 758 ambapo hadi kufikia tarehe 31 Mei, 2024 minara 295 ilijengwa sawa na **asilimia 39**. Hatua hii imewezesha watumiaji wa mtandao kuongezeka kutoka **asilimia 52.1** mwaka 2021/22 hadi asilimia **asilimia 61.2** mwaka 2023/24.

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Kamati inaishauri Serikali mambo yafuatayo:-

(i) Kukamilisha mradi wa ujenzi wa minara kwa wakati ili kuimarisha mawasiliano ya simu vijijini pamoja na kuongeza matumizi ya mtandao kwa ajili ya shughuli za kiuchumi na kijamii;

(ii) Kuongeza matumizi ya teknolojia ya akili bandia (Artificial

(iii) Intelligence-AI) katika Taasisi za Serikali;

(iv) Kukipatia Chuo cha TEHAMA na vifaaa vya kisasa ili kizalisha wataalamu wenye ujuzi shindani; na

(v) Serikali kushirikisha sekta binafsi katika kukamilisha ujenzi na usambazaji wa Mkongo wa Taifa ili kuongeza matumizi ya mtandao na kukuza uchumi wa kidigitali.

**3.1.3.3. Sekta ya Kilimo**

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Kamati imefanya uchambuzi na kubaini bajeti ya kilimo imeongezeka kutoka **shilingi bilioni 294.** mwaka 2021/22 hadi kufikia **shilingi trilioni 1.24** mwaka 2023/24. Ongezeko hili limechangia katika maeneo yafuatayo:-

(i) Kasi ya ukuaji wa sekta ya kilimo imeongezeka kutoka **asilimia 2.7** kwa mwaka 2020 hadi **asilimia 3.9** kwa mwaka 2023;

(ii) Mauzo ya mazao nje yameongezeka kutoka **dola za Marekani bilioni 1.2** hadi **dola za Marekani bilioni 2.3** sawa na ongezeko la **asilimia 99.67**; na

(iii) Utoshelevu wa chakula nchini umeongezeka kutoka **asilimia 114** kwa mwaka 2021/22 hadi **asilimia 140** kwa mwaka 2023/24.

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Kamati ilichambua viashiria na shabaha za sekta hii na kubaini kuwa Serikali haikuweza kufikia lengo la kuongeza hekta za umwagiliaji ambapo hadi 2024 zilikuwa **hekta 727,280.6** sawa na **asilimia 60.61** za lengo la **hekta 1,200,000** ifikapo mwaka 2025/26. Aidha kwa upande wa uzalishaji wa mbegu bora Serikali haikufikia lengo la uzalishaji, ambapo hadi mwaka 2024 **tani 71,356** zilizalishwa sawa na **asilimia 50.97** ya lengo la **tani 140,000**. Pamoja na changamoto hizi, sekta hii inakabiliwa na changamoto zifuatazo:-

(i) Tija ndogo katika uzalishaji;
(ii) Uzalishaji wa kukidhi mahitaji ya chakula kuliko biashara;
(iii) Kilimo cha kutegemea mvua;
(iv) Teknolojia duni katika shughuli za kilimo;
(v) Upungufu wa mbegu bora;
(vi) Matumizi hafifu ya mbolea;
(vii) Kukosekana kwa masoko ya uhakika; na
(viii) Ukosefu wa huduma za ugani.

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** ili kukabiliana na changamoto hizo, Kamati inashauri Serikali masuala yafuatao:-

(i) Serikali isimamie vyema miradi ya ujenzi wa mabwawa makubwa kwa ajili ya umwagiliaji na kuhakikisha yanakamilika na kutumika ili kuwe na tija iliyokusudiwa. Hivi sasa Serikali ina jumla ya miradi ya mabwawa 18 na kati ya hayo yaliyokamilika ni mabwawa matatu;

(ii) Miradi mingi ya Jenga Kesho iliyo Bora (BBT) bado haijakamilishwa, licha ya miradi hiyo kuwa na umuhimu kwa maendeleo ya Taifa;

(iii) Kutafuta masoko ya uhakika na yanayotabirika, sambamba na kutafuta ithibati kwa mazao yanayohitaji ithibati ili yauzwe nje ya nchi kwa mfano Kahawa;

(iv) Serikali iongeze uzalishaji wa pembejeo bora za kilimo ili kuongeza uzalishaji.

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, vilevile ni vyema Serikali ikafanya tathmini ya ongezeko la Bajeti ya kilimo kwa miaka miwili ili kubaini mchango wa bajeti iliyoongezeka katika kukuza uchumi.

**Jedwali Namba 6: Utekelezaji wa Sekta ya Kilimo mwaka 2023/24**

| Na. | Aina ya utekelezaji | Hali halisi(%) 2023/24 | Lengo(%)2025/26 |
|---|---|---|---|
| 1. | Mchango wa kwenye pato la Taifa | 26.5 | 23.4 |
| 2. | Mchango wa Mauzo nje | 16.1 | 19.0 |
| 3. | Kiwango cha ajira | 65.6 | 60 |
| 4. | Ukuaji wa sekta | 4.2 | 6.1 |

***Chanzo*:** Wizara ya Mipango (2024)

### 3.1.3.4. Sekta ya Mifugo

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Sekta ya mifugo ilikua kwa **asilimia 5** na kuchangia **asilimia 6.2** ya Pato la Taifa katika mwaka 2023 na ikilinganishwa na lengo la ukuaji wa **asilimia 6.8** ifikapo mwaka 2025/26. Ili kuondokana na changamoto zinazoikabili sekta ya mifugo, Kamati ina ushauri ufuatao kwa Serikali:-

(i) Serikali iboreshe malisho ya mifugo, kurahisisha upatikanaji wa virutubisho na kutenga maeneo ya mifugo ili kupunguza ufugaji wa kuhama hama. Hatua hii itasaidia kuongeza uzalishaji wa maziwa kwa ng'ombe wa asilia kutoka **lita 0.8** kwa siku ilivyo sasa hadi **lita 4** kwa siku ifikapo mwaka 2025/26;

(ii) Serikali kuweka vivutio kwa wenye viwanda vya kuchakata maziwa ili kuongeza uzalishaji na kupunguza upotevu wa maziwa. Hatua hii itasaidia Serikali kufikia lengo la **asilimia 14** ya uzalishaji wa maziwa yaliyochakatwa ifikapo 2025/26 ikilinganishwa na uzalishaji wa sasa wa **asilimia 2.2**;

(iii) Serikali kuboresha mazingira ya wafugaji kwa kuongeza ranchi na kupunguza gharama za malisho kwenye ranchi za

Serikali. Hatua hii itasaidia kupunguza changamoto ya uhaba wa malisho; na

(iv) Serikali ilijiwekea lengo la kuchakata ngozi hadi kufikia kiwango cha "*wet blue*" kwa tani 9,210.6 ifikapo mwaka 2025/26. Hata hivyo, hadi kufikia mwaka 2024 tani zinazochakatwa ni 2,900. Aidha, Serikali ipitie upya vivutio vilivyowekwa katika uchakataji wa ngozi hadi kufikia hatua ya "*wet blue*";

(v) Serikali iboreshe mazingira ya machinjio. Jambo hili litasaidia nyingi nje ya nchi;

(vi) Serikali ihamasishe wananchi katika ufugaji wa ng,ombe, mbuzi, kondoo, kuku, bata na kware ili kuongeza upatikanaji wa nyama; na

(vii) Kuimarisha huduma za uhimilishaji wa wanyama ili kupata mbegu bora na zenye uwezo wa kupambana na magonjwa.

### 3.1.3.5. Sekta ya Uzalishaji Bidhaa Viwandani

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Kamati imefanya uchambuzi na kubaini ukuaji wa sekta ya viwanda ulifikia **asilimia 4.3** ikilinganishwa na lengo la **asilimia 6.8** mwaka 2025/26 na mchango katika mapato ya mauzo nje ulifikia **asilimia 17.7** ikilinganishwa na lengo la **asilimia 19** mwaka 2025/26. Hata hivyo, Sekta ya viwanda inakabiliwa na changamoto zifuatazo:-

(i) Baadhi ya bidhaa kutokuwa na ubora na hivyo kushindwa kushindana kwenye masoko ya kimataifa;

(ii) Wingi wa mamlaka za usimamizi na udhibiti inazosababisha urasimu;

(iii) Ukosefu wa malighafi za viwandani;

(iv) Matumizi ya teknolojia ya zamani katika uzalishaji;

(v) Taasisi moja ya Umma kukwamisha uwekezaji wa Taasisi nyingine kwa kudai ada za leseni mfano Mradi wa Magadi Soda wa Engaruka unaotekelezwa na NDC;

(vi) Ukosefu wa rasilimali watu wenye ujuzi; na vii. Ukosefu wa mitaji ya kuanzisha na kuendeleza viwanda pamoja na gharama kubwa za mikopo.

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, Kamati inaishauri Serikali masuala yafuatayo:-

(i) Kuendelea kuboresha mazingira ya uwekezaji;
(ii) Kuweka madirisha maalumu ili kusaidia upatikanaji wa mitaji kwa ajili ya ujenzi na uendelezaji wa viwanda;
(iii) Kuendeleza viwanda vya usindikaji na kuongeza thamani ya mazao ya kilimo; na
(iv) Kuendelea kuboresha utolewaji wa mikopo kwa vyuo vya ufundi na stadi za kazi.

**3.1.3.6. Sekta ya Madini**

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** ukuaji wa sekta ya madini ulifikia **asilimia 11.3** mwaka 2023 sawa na **asilimia 93.9** ya lengo la **asilimia 11.6** ifikapo mwaka 2025/26. Mchango kwenye Pato la Taifa ulifikia **asilimia 9.0** mwaka 2023 sawa na **asilimia 80.35** ya lengo la **asilimia 11.2** ifikapo mwaka 2025/26. Aidha, mapato ya fedha za nje zinazotokana na sekta hii ni dola za **Marekani milioni 3,551.4** wakati lengo ni kufikia **dola za Marekani milioni 3,760.4**.

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Kamati inaona kwamba sekta ya madini inaweza kupunguza nakisi kwenye urari wa malipo endapo kuna mzingira mazuri ya uwekezaji utafanyika ili kuvutia wawekezaji hasa katika madini ya kimkakati. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali kuendelea kuboresha mazingira wezeshi ili kuchochea uwekezaji katika sekta hii .

**3.1.3.7. Sekta ya Utalii**

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Kamati imefanya uchambuzi na kubaini kwamba, kiwango cha mchango wa sekta ya utalii katika

kuliingizia Taifa fedha za kigeni ulifikia **asilimia 25** ikilinganishwa na lengo la **asilimia 27** ifikapo mwaka 2025/26, na idadi ya watalii imeongezeka kufikia watalii **3,784,214** kati ya watalii hao watalii wa ndani walikuwa ni **1,976,009** na wa nje ya nchi ni **1,808,205**, mwaka 2023/24, ikilinganishwa na lengo la watalii **5,000,000** ifikapo mwaka 2025/26.

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Kamati imebaini kwamba sekta hii inakabiliwa na changamoto zifuatazo:-

(i) Ubovu na ukosefu wa miundombinu ya msingi kwenye maeneo ya hifadhi na mapori tengefu;
(ii) Uwekezaji hafifu wa miundombinu katika kanda ya Kusini;
(iii) Bajeti ndogo kwa ajili ya kutangaza fursa za utalii nchini;
(iv) Gharama kubwa ya sekta ya utalii wa uwindaji ikilinganishwa na mataifa mengine;
(v) Ukosefu wa malazi ya kutosha;
(vi) Gharama kubwa za huduma za utalii ukilinganisha na nchi jirani; na
(vii) Eneo kubwa la mwambao lenye ufukwe wenye urefu wa kilomita 800 halijatumika kwa ujenzi wa hoteli;

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Kamati inaishauri Serikali masuala yafuatayo:-

(i) Kujenga na kukarabati miundombinu ya msingi katika hifadhi, mbuga na mapori tengefu;
(ii) Kuwekeza na kuendeleza maeneo ya kanda ya Kusini; iii. Kutenga bajeti ili kutangaza maeneo na vivutio vipya vya utalii kama vile utalii wa kitamaduni, utalii wa mazingira, utalii wa fukwe, utalii wa afya, utalii wa michezo na utalii wa mikutano; na
(iii) Kuiongezea fedha Bodi ya Utalii Tanzania (TTB) ili iweze kutangaza fursa na vivutio vya utalii.

### 3.1.3.8. Sekta ya Kukuza Uwekezaji na Biashara

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Kamati imefanya uchambuzi na kubaini, miradi 9,678 ya uwekezaji yenye thamani ya **dola za Marekani milioni 8,658** imesajiliwa katika kipindi cha mwaka 2023 ikilinganishwa na **miradi 8,401** yenye thamani ya **dola za Marekani**

**milioni 5,658.47** kwa mwaka 2022. Kamati inaona kigezo cha kupima uwekezaji kwa kuangalia ongezeko la usajili wa miradi uliofanyika nchini hakina uhalisia. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali kwenye mpango wa mwaka ujao ni vema Serikali ikajipima kwa kulinganisha miradi iliyosajiliwa, miradi iliyotekelezwa na ajira zilizopatikana.

### 3.1.3.9. Sekta ya Diplomasia ya Uchumi

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Kamati imefanya uchambuzi wa misingi ya dhana ya Diplomasia ya uchumi ili kubaini endapo Tanzania imepiga hatua katika utekelezaji wake. Misingi iliyochambuliwa ni ifuatayo:-

(i) Kukuza na kuvutia uwekezaji na biashara baina ya mataifa katika sekta mbalimbali ;

(ii) Kuleta teknolojia mpya kupitia ushirikiano kati ya nchi na nchi;

(iii) Kutafuta masoko ya bidhaa na huduma zinazozalishwa na kutolewa nchini kwa mataifa mengine;

(iv) Kutanganza fursa za utalii wa Tanzania nje ili kuwavutia wageni kutembelea nchini; na

(v) Kuongeza ushawishi wa Tanzania kwenye medani za Kimataifa.

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Kamati imefanya uchambuzi wa changamoto zinazokabili diplomasia ya uchumi nchini na kubaini yafuatayo:-

(i) Mabalozi kutokuwekewa vipimo vya utendaji kazi;

(ii) Watanzania wengi kutojua fursa za ajira zinazopatikana nje ya nchi;

(iii) Ofisi za balozi kutokuwa na fedha za kutosha kwa ajili ya kutekeleza diplomasia ya uchumi;

(iv) Taifa kupokea kiasi kidogo cha miradi ya uwekezaji kutoka kwa Watanzania wanaoishi ughaibuni kama inavyoonekana katika jedwali namba 7 hapo chini;

(v) Kukosekana kwa ofisi za kibalozi katika baadhi ya nchi za kimkakati, uchakavu wa miundombinu ya ofisi za balozi pamoja na baadhi ya balozi kupanga katika majengo binafsi; na

(vi) Tanzania haijatumia vizuri fursa ya kusafirisha walimu na wataalam wa kiswahili nje yua nchi.

**Jedwali Namba 7: Fedha zilizotumwa na Diaspora Nchi za Afrika Mashariki**

| **Nchi** | **Kiasi (TZS Trilioni)** |
|---|---|
| Burundi | 0.12 |
| Tanzania | 0.83 |
| Rwanda | 1.38 |
| South Sudan | 2.11 |
| Uganda | 3.24 |
| DR Congo | 3.40 |
| Kenya | 10.53 |

***Chanzo:*** Taarifa ya Mifumo ya Kitaifa ya benki kuu ya Tanzania (BOT) ya mwaka 2022

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** kufuatia changamoto hizo Kamati inaushauri mambo yafuatayo:-

(i) Serikali ianzishe mfumo ya kupima na kutathmini utendaji kazi wa mabalozi kwa kutumia kigezo cha nchi wanazowakilisha;

(ii) Mabalozi kuwa na utaratibu wa kutangaza fursa za ajira na masomo ya kimkakati katika nchi wanazowakilisha;

(iii) Serikali kutenga bajeti ya kutosha kwa ajili ya uendeshaji, ukarabati na ujenzi wa miundombinu ya balozi;

(iv) Kuboresha na kuimarisha mfumo wa kusajili diaspora na sehemu waliyopo; na

(v) Benki Kuu kuweka vigezo na mifumo rahisi ya kutuma fedha nchini ili kurahisisha zoezi la ufanyaji wa malipo ya Kimataifa.

### 3.1.3.10. Sekta ya Elimu na Maendeleo ya Ujuzi

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Kamati inatambua jitihada mbalimbali zinazofanywa na Serikali ili kukuza sekta ya elimu kwa kuajiri jumla ya walimu 37,879 kwa kipindi cha miaka 4. Hata hivyo, bado sekta hii inakabiliwa na changamoto zifuatazo:-

(i) Uhaba wa walimu katika shule za sekondari na msingi ambapo viwango vya kimataifa vinaelekeza uwiano wa mwalimu 1 kufundisha wanafunzi 45 ila uwiano wa walimu na wanafunzi uko juu kwa Tanzania;

(ii) Uhaba wa vitendea kazi vya kufundisha na kujifunzia;

(iii) Changamoto ya miundombinu mashuleni kama vile madarasa, mabweni, vyoo na maabara za kisasa;

(iv) Wataalam wanaozalishwa na mfumo wa elimu kutoendana na mahitaji ya soko la ajira; na

(v) Matumizi madogo ya teknolojia ya kisasa katika ufundishaji (online platforms) ili kukabiliana na tatizo la uhaba wa walimu

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** kufuatia changamoto hizo, Kamati inaishauri Serikali masuala yafuatayo;

(i) Kuajiri walimu wa kutosha katika ngazi zote, pamoja na kutenga bajeti kwa ajili ya vitendea kazi pamoja na maabara za kisasa;

(ii) Kutoa elimu na mafunzo yanayokuza ujuzi ili kukidhi mahitaji halisi ya soko la ajira;

(iii) Kuimarisha miundombinu ya kujifunza na kujifunzia kwa vyuo vya ufundi na vyuo vya kati kama VETA na SIDO;

(iv) Kuanzisha kozi fupi za ufundi na mafunzo ya amali kama vile simu, useremala, ujenzi na umeme;

(v) Kuharakisha utekelezaji wa mtaala mpya wa elimu ambao unajumuisha fani za masuala mbalimbali mfano, useremala, uashi, ushonaji, umeme, ufugaji wa kuku, samaki, na mifugo mingine kwa njia za kisasa;na

(vi) Serikali ianze kutumia madarasa janja ili kupunguza changamoto ya uhaba wa walimu katika mafunzo.

**3.1.3.11. Sekta ya Afya**

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Kamati imefanya uchambuzi na kubaini kuwa sekta hii ina changamoto zifuatazo:-

(i) Uhaba wa wataalamu wa afya, vifaa tiba na madawa hasa katika maeneo ya vijijini;

(ii) Ukosefu wa miundombinu ya msingi kama umeme na maji katika vituo vya afya;

(iii) Ukosefu wa huduma za msingi;

(iv) Uhaba wa vifaa tiba na madawa katika baadhi ya vituo vya afya, zahanati na hospitali za wilaya;

(v) Uwepo wa madeni ya washitiri na wazabuni; na

(vi) Wananchi wengi kushindwa kumudu gharama za matibabu.

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Kamati inaishauri Serikali kuongeza idadi ya wataalamu wa afya, kujenga nyumba za madkatari, kuongeza **vifaa** tiba pamoja na kutoa huduma bora za afya kwa

wananchi. Aidha, mchakato wa bima ya afya kwa wote uanze ili kuwapa wananchi matibabu nafuu.

### 3.1.3.12. Sekta ya Mipango Miji, Nyumba na Maendeleo ya Makazi

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Kamati imefanya uchambuzi na kubaini kwamba, ardhi iliyopimwa imefikia asilimia 26 mwaka 2023/24 ikilinganishwa na lengo la **asilimia 37.0** ifikapo mwaka 2025/26. Manufaa ya kupima ardhi ni kuwezesha wamiliki wa viwanja na mashamba kuwa na hati miliki itakayowasaidia kukopa kwenye taasisi za fedha na benki za kibiashara kwa kuweka dhamana ardhi waliyonayo ili kutekeleza miradi ya maendeleo pamoja na kupunguza migogoro. Aidha, kutopanga na kutokupima ardhi kunaweza kusababisha changamoto zifuatazo: -

i. kuongezeka kwa migogoro ya ardhi;
ii. kukosa mapato yanayotokana na kodi ya pango la ardhi;
iii. kuongezeka kwa makazi holela; na
iv. uharibifu wa mazingira na vyanzo vya maji.

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Kamati inaishauri Serikali iweke utaratibu wa kurejesha asilimia 30 ya mapato yanayotokana na kodi ya pango la ardhi ili fedha hizo zitumike kwenye kupima ardhi na kupanga miji. Hatua hii itapunguza migogoro ya ardhi nchini. Vilevile, Wizara ya ardhi iboreshe mfumo wa kuwakumbusha wamiliki wa ardhi kulipa kodi ya pango la ardhi kwa wakati.

## 4.0. UGHARAMIAJI WA MPANGO WA MAENDELEO KWA MWAKA 2025/26

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** katika mwaka wa fedha 2025/26, Serikali imepanga kutumia jumla ya **shilingi trilioni 16.32** kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo, sawa na **asilimia 29.89** ya bajeti yote ya mwaka 2025/26 ambapo, imeshuka ukilinganisha na asilimia 32.32 ya bajeti ya maendeleo ya mwaka jana. Aidha, bajeti ya Maendeleo imeongezeka kutoka **shilingi trilioni 15.33** mwaka 2024/25 hadi **shilingi trilioni 16.46** mwaka 2025/26 sawa na ongezeko la **asilimia 7.44 (Trilioni 1.14)**.

**Jedwali Namba 8: Asilimia ya Bajeti ya Maendeleo kwa Bajeti nzima ya Serikali**

| Mwaka | Bajeti Maendeleo ya | Jumla kuu ya Bajeti | Asilimia |
|---|---|---|---|
| 2022/23 | 15.006 | 41.48 | 36.18 |
| 2023/24 | 14.077 | 43.34 | 32.48 |
| 2024/25 | 15.325 | 47.42 | 32.32 |
| 2025/26 | 16.46 | 55.06 | 29.89 |

## 5.0. MAENEO YA KIPAUMBELE YA MPANGO KWA MWAKA 2025/26

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Serikali imeendelea kutekeleza vipaumbele vilivyoainishwa katika Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/22-2025/26 ambavyo ni kuchochea uchumi shindani na shirikishi, kuimarisha uwezo wa uzalishaji viwandani na utoaji huduma, kukuza uwekezaji na biashara, kuchochea maendeleo ya watu na kuendeleza ujuzi.

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Kamati imefanya uchambuzi kwenye maeneo ya kipaumbele na kubaini masuala yafuatayo;

### *5.1. Uzalishaji viwandani*

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, kwa mwaka 2023 mchango wa sekta ya uzalishaji viwandani katika pato la taifa ni **asilimia 7** ikiwa ni chini ya lengo la **asilimia 12.5** ifikapo 2026. Kamati inaishauri serikali masuala yafuatayo:-

(i) Kutekeleza Mpango wa Kuboresha Mazingira ya Uwekezaji Nchini ili kuvutia wawekezaji katika maendeleo ya viwanda. Aidha, katika kipindi ambacho UNCTAD inasimamisha utoaji wa Taarifa yake ya *Doing Business* Mwaka 2020 Tanzania ilikuwa nchi ya 141 kati ya nchi 190;

(ii) Serikali kupitia viashiria vya kiushindani vya kimataifa ili kuweza kutambua viashiria ambavyo Tanzania haifanyi vizuri na kuweka mikakati ya kuvirekebisha;

(iii) Serikali kulinda viwanda vilivyopo katika maeneo huru ya uzalishaji kwa ajili ya mauzo nje ya nchi (Special Economic Zone-SEZ) ili kuongeza uwezo wa viwanda hivyo kuuza bidhaa nje ya nchi na kuongeza fedha za kigeni;

(iv) Serikali kurejesha mpango wake wa "*Road Map For Improvement of Bussiness Enviroment in Tanzania*" ili kuendelea kujipima na kuboresha mazingira ya Biashara;

(v) Serikali kuweka vivutio vya uwekezaji kwenye maeneo ambayo Tanzania ina nguvu ya ushindani katika jumuiya ya Afrika Mashariki na SADC kama vile madini, utalii, kilimo na gesi asilia; na

(vi) Serikali kuharakisha majadiliano ya mikataba ya uwekezaji hasa kwenye miradi mikubwa ya LNG, Mchuchuma na Liganga.

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, moja ya changamoto kubwa inayoikabili maeneo huru ya uzalishaji kwa ajili ya mauzo nje *(SEZ na EPZ)* ya nchi ni kutolipwa kwa fidia kwa maeneo yaliyotwaliwa na Serikali. Mfano maeneo yaliyopo Mererani- Mkoa wa Manyara na Kahama Mkoa wa Shinyanga. Hivyo Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kwamba fidia katika maeneo husika inakuwa ni kipaumbele katika mwaka wa fedha 2025/26.

***5.2. Kukuza Sekta ya fedha***

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** uchambuzi wa Kamati umebaini tangu kutungwa kwa Sheria ya Sekta Ndogo Sura ya 407 kumekuwa na usimamizi hafifu wa utekelezaji wa Sheria hiyo na kusababisha matatizo makubwa katika jamii. Hivyo, Kamati inaitaka Serikali kuhakikisha kwamba inasimamia masharti ya Sheria ya Sekta ndogo ya fedha kuwa jambo la kipaumbele ili kupunguza malalamiko ya wananchi.

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Benki kuu ya Tanzania imeanzisha sera mpya ya fedha ambayo inalenga riba ya Benki kuu inayoitwa *Central Bank Rate - CBR*. Lengo la Sera hiyo ni kutumia nyenzo ya riba kusimamia Sera ya Fedha ili kurahisisha mikopo baina ya

mabenki. Hivi sasa CBR imepanda kutoka asilimia **asilimia 5.5** hadi **asilimia 6** hivyo mikopo baina ya mabenki ni kati ya asilimia 4 na 8. Hatua hii imesaidia kushusha kwa riba za mikopo kwa kiwango kidogo kutoka wastani wa asilimia **asilimia 16.04** mwaka 2022/23 hadi **asilimia 15.47** mwaka 2023/24.

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** kwa kuwa Sheria ya Benki Kuu inaipa mamlaka Taasisi hiyo kufanya mapitio ya gharama za huduma za Benki, Kamati inaishauri Serikali kupitia Taasisi hiyo kufanya mapitio ya gharama za uendeshaji wa benki za kibiashara ili kubaini sababu na vihatarishi vinavyosababisha riba za mikopo kuendelea kuwa juu nchini. Vilevile, Serikali inashauriwa kuangalia uwezekano wa kupunguza riba za dhamana za muda mrefu ili kupunguza gharama za mikopo kwa sekta binafsi.

***5.3. Uendeshaji wa Sekta ya Madini***

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, uendelezaji wa sekta ya madini ni moja ya eneo lilipewa kipaumbele katika bajeti ya mwaka 2025/26 kwa kuendeleza miradi ya madini ya mkakati ikiwemo mradi wa magadi soda Engaruka. Kamati imebaini mradi huu umeshindwa kuanza utekelezaji wake kufuatia Shirika la Maendeleo Tanzania (NDC) kushindwa kumaliza kulipa kiasi cha **dola za Marekani 194,360** kati ya **dola za Marekani 447,600** kama ada ya mwaka ili kupata leseni ya uchimbaji kutoka Tume ya madini.

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Kamati inaishauri Serikali kufanya mapitio ya Sheria mbalimbali zilizopo katika sekta ya madini pamoja na kutoa msamaha wa ada ya mwaka ya leseni kwa NDC ili kuhakikisha kwamba NDC inatekeleza majukumu yake kama ipasavyo. Mfano, Mradi wa Magadi soda wa Engaruka pamoja na sababu nyingine umekwama kuanza utekelezaji wake kutokana na Wizara ya Madini kudai ada ya Leseni kwa Shirika la Taifa la Maendeleo (NDC).

***5.4. Uendelezaji wa Miradi ya Maji.***

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, Kamati imefanya uchambuzi wa utekelezaji wa miradi ya maji nchini na kubaini changamoto zifuatazo:-

i. Taarifa ya Serikali inaonyesha kwamba katika mwaka 2023/24 idadi ya wananchi waishio vijijini wanaopata maji safi imeongezeka kufikia **asilimia 79.6** ikilinganishwa na **asilimia 70** ya mwaka 2019/20, na kwa maeneo ya mijini idadi hiyo imefika **asilimia 90** ikilinganishwa na **asilimia 84** ya mwaka 2019/20. Hata hivyo, Kamati imebaini kuwa takwimu zilitolewa ni za kihandisi ambapo zinakokotolewa kwa kuangalia idadi ya miradi iliyotekelezwa na idadi ya watu waliolengwa na haiakisi mahitaji na upatikanaji wa maji bila kuangalia ni watu wangapi wanatumia mradi huo na endapo mradi huo bado unafanya kazi.

**Jedwali Namba 9:** Utekelezaji wa miradi ya maji kwa mwaka 2023/24

| Na. | Kigezo | Hali halisi 2023/24 (%) | Lengo (2025/26) |
|---|---|---|---|
| 1. | Watu vijijini wanaopata maji ya bomba/salama | 79.6 | 85.0 |
| 2. | Kaya vijijini zenye miundombinu bora ya usafi wa mazingira | 77.5 | 60.0 |
| 3. | Watu Dar es Salaam wanaopata maji ya bomba/salama | 92.5 | 95.0 |
| 4. | Watu katika makao makuu ya mikoa wanaopata maji ya bomba/salama | 90.0 | 95.0 |
| 5. | Kaya makao makuu ya mikoa zenye mfumo rasmi wa maji-taka | 14.0 | 30.0 |

***Chanzo:*** *Taarifa ya Mpango wa Bajeti kwa Mwaka 2025/26*

ii. Madeni ya wazabuni na wakandarasi wa miradi ya maji kutokulipwa na hivyo kusimamisha utekelezaji wa miradi ya maji;

iii. Baadhi ya wakandarasi kutokuwa na uwezo wa kutekeleza miradi ya maji;

iv. Baadhi ya vyanzo vya maji kukauka au kutokufanya kazi lakini bado Serikali inavijumusha katika takwimu zake kama vyanzo vinavyosambaza maji;

v. Mitambo ya kuchimba visima na mabwawa kutotumika kikamilifu kutokana na ukosefu fedha za kuiendesha; na

vi. Fedha za mfuko wa maji kutokuwasilishwa katika mfuko huo kama Sheria inavyoelekeza.

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** kutokana na changamoto zinazoikumba sekta ya maji nchini, Kamati inaishauri Serikali yafuatayo:-

(i) Kufanya tathmini ya upatikanaji wa maji nchini kuanzia ngazi ya Vijiji, Kata, Tarafa, Wilaya, na Mkoa ili kupata hali halisi ya upatikanaji na uhitaji wa maji. Tathmini hiyo itatoa majibu sahihi yatakayowezesha kuandaa mpango wa utekelezaji wa miundombinu ya maji;

(ii) Kamati inaishauri Serikali kuweka mikakati ya kuendeleza miundombinu ya maji safi na salama sambamba na miundombinu ya maji taka. Kamati imebaini kuwa Serikali inawekeza zaidi katika miundombinu ya maji safi na salama, na kuweka mkazo mdogo katika miundombinu ya maji taka ili kulinda usafi wa mazingira. Jedwali Na.8 linaonyesha utekelezaji wa miradi ya maji kwa mwaka 2023/24;

(iii) Kulipa madeni ya wakandarasi na wazabuni ambayo 2024 Juni, yalikuwa yana thamani ya **shilingi bilioni 415;**

(iv) Kuwasilisha fedha za mfuko wa maji kama zilivyo kusanywa kutoka kwenye chanzo;

(v) Kuhakikisha seti tano za kuchimba mabwawa na visima zinapata fedha za kutosha za uendeshaji; na

(vi) Kuhakikisha miradi ya maji inatekelezwa na wakandarasi wenye uwezo.

### *5.5. Kuongeza wigo wa kinga ya jamii*

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, Serikali imelenga kutoa kinga ya jamii kwa makundi yaliyo katika hali hatarishi ili kuhakikisha ustawi wa jamii yote na kutoa kipaumbele katika utekelezaji wa mpango wa bima ya afya kwa wote. Chanzo kimoja cha mfuko wa bima ni **asilimia 2** ya mapato ya ushuru wa bidhaa utakaokusanywa kutoka bidhaa za urembo, vinywaji laini (carbonated drinks) na vileo (bia na pombe kali).

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Kamati ina taarifa kwamba Mapato yaliyokusanywa kwa kipindi cha robo ya kwanza ya mwaka 2024/25 kwa ajili ya mfuko wa bima ya afya kwa wote yalikuwa **Shilingi 22,947,920,370.78** ambapo **Shilingi 4,735,239,870.78** zilitokana na **asilima 2** ya mapato ya ushuru wa bidhaa na **shilingi 18,212,680,500** ni **asilimia 100** ya makusanyo yanayotokana na ushuru wa bidhaa kwenye *undenatured ethyl alcohol*. Aidha, fedha hizi tayari zimepelekwa kwenye Mfuko.

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** kwa kuwa Bima ya Afya kwa wote bado haijaanza kutekeelezwa na kwa kuwa bado kuna changamoto kubwa ya vifaa tiba, Kamati inaishauri Serikali kutumia fedha hizi ili kupunguza changamoto ya vifaa tiba katika Hospitali za Mikoa na Wilaya zilizojengwa nchini.

## 6.0. MAKADIRIO YA BAJETI 2025/26

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** katika mwaka wa fedha 2025/26 Serikali imekusudia kukusanya jumla ya **Shilingi trilioni 55.06** sawa na ongezeko la **asilimia 11.58**, la **shilingi trilioni 5.72** ukilinganisha na Bajeti ya Mwaka ya Mwaka 2024/25 iliyokuwa na jumla ya shilingi trilioni 49.35

### *6.1. Mapato ya Ndani*

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** uchambuzi wa Kamati umebaini kwamba mapato ya ndani yanayokusanywa na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Serikali za Mitaa, Maduhuli ya Wizara, Idara na Wakala pamoja na Mapato ya Msajili wa Hazina yanatarajiwa kuongezeka kwa **asilimia 12.57** sawa na **Shilingi trilioni 4.351**. Aidha, mikopo kwa ajili ya kudumisha deni la ndani *(Roll over)* malipo yameshuka kwa **asilimia 17.32** kutokana na kupungua kwa kiasi kinacholipwa *(Redemption Profile)* Jedwali Na. 10. Linaonyesha makadirio ya bajeti ya Serikali kwa mwaka 2025/26. Uchambuzi wa Kamati umebaini kwamba ukuaji wa uchumi unatarajiwa kukua kwa **asilimia 5.8** pamoja na mfumuko wa bei usiozidi **asilimia 5** ni wazi kwamba kuna uwezekano mkubwa wa Serikali kufikia malengo ya makusanyo kwa **asilimia 2 hadi 3** kulingana na mwenendo wa miaka iliyopita.

**Jedwali Namba 10: Makadirio ya Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2025/26.**

| | **2024/25 Bajeti iliyoidhinish wa** | **2025/26 Makadirio ya Bajeti** | **Tofauti** | **Ukuaji** |
|---|---|---|---|---|
| **JUMLA YA MAPATO** | **49,345.69** | **55,061.61** | **5,715.92** | **11.58** |
| Mapato ya Ndani ikijumuisha mapato ya Halmashauri | 34,610.65 | 38,962.49 | 4,351.84 | 12.57 |
| Misaada na Mikopo Nafuu ya Kibajeti | 1,489.77 | 1,741.02 | 251.25 | 16.87 |
| Misaada na Mikopo Nafuu ya Miradi | 3,461.95 | 4,761.17 | 1,299.22 | 37.53 |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| Misaada na Mikopo Nafuu ya Mifuko ya Kisekta | 178.89 | 189.74 | 10.85 | 6.07 |
| Mikopo ya Ndani Kulipa Mtaji Deni la Ndani (Rollover) | 4,022.37 | 3,325.56 | -696.81 | -17.32 |
| Mikopo ya Ndani ya Kibiashara (NDF) | 2,595.42 | 2,952.63 | 357.21 | 13.76 |
| Mikopo ya Nje ya Kibiashara | 2,986.64 | 3,129.01 | 142.37 | 4.77 |

***Chanzo:*** Mwongozo wa Mpango na Bajeti

***6.2. Mwenendo wa Utekelezaji wa Bajeti ya Serikali kuanzia mwaka 2020/21-2025/26***

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, Kamati imefanya uchambuzi wa utekelezaji wa bajeti kwa kipindi cha miaka mitatu (2020/21-2025/26) kwa kuangalia ukuaji wa bajeti ya Serikali kwa kipindi husika pamoja na utekelezaji wake, ukilinganisha na malengo. Kamati imebaini yafuatayo:-

(i) Bajeti ya Serikali imekua kwa wastani wa **asilimia 9.6**. Aidha, kwa kipindi cha miaka miwili (2024/25 na 2025/26) bajeti imeongezeka kwa wastani wa **asilimia 11.38**. Ukuaji huu unamaanisha kuwa mahitaji ya rasilimali fedha yanaendelea kuongezeka mwaka hadi mwaka.

(ii) Bajeti imekuwa ikitekelezwa kwa wastani wa **asilimia 95.14** katika kipindi cha mwaka 2020/21 hadi 2023/24 ambapo katika miaka miwili, 2021/22 na 2023/24 bajeti ilitekelezwa kwa wastani wa **asilimia 97**. Mwenendo huu unaashiria kwamba Serikali ina uwezo wa kukusanya fedha kutoka vyanzo mbalimbali kwa ajili ya kutekeleza mipango iliyojiwekea.

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, Kamati inaipongeza Serikali kwa hatua hii, hata hivyo Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kuwa mipango na bajeti yake zinagharamiwa zaidi na mapato ya ndani na sio kutegemea mikopo. Hivyo kuna haja ya Serikali kuongeza mapato yake ya ndani kuweza kufikia walau **asilimia 85** ya bajeti. Hivi sasa mapato ya ndani yanagharamia bajeti kwa wastani wa **asilimia 70** na **asilimia 30** ni mikopo.

## 7.0. USIMAMIZI WA VIHATARISHI VYA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI

### *7.1. Madeni Sanjari*

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, Madeni sanjari ni mikopo iliyochukuliwa na Taasisi, Wakala au Makampuni ya Umma kwa kudhaminiwa na Serikali kuu chini ya Sheria ya Mikopo, Misaada na Dhamana, Sura 134. Mikopo hii inakuwa kihatarishi pindi mkopaji anaposhindwa kulipa, na hivyo kulazimika kulipwa na Serikali kutoka mfuko mkuu. Aidha, uzoefu unaonesha kwamba mashirika na makampuni ya umma hayafanyi vizuri kulinganisha na makampuni binafsi ambayo yapo kwenye sekta moja. Uchambuzi huu unaashiria kwamba hakuna uwajibikaji na usimamizi mzuri kwa sababu mashirika hayo yanapokea ruzuku na mitaji kutoka Serikalini.

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Kamati inaipongeza Serikali kwa kuanza utaratibu wa kuorodhesha Mashirika ya Umma kwenye masoko ya mitaji ambapo Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Tanga imekuwa taasisi ya kwanza ya Serikali kutumia utaratibu huo kwa kutoa hatifungani yenye thamani ya **shilingi bilioni 53.1**. Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha Mashirika yanayojiendesha kibiashara yajiorodheshe katika masoko ya mitaji ili kupunguza wajibu wa Serikali kudhamini Mashirika hayo.

### *7.2. Madeni ya Wazabuni, Wakandarasi na watoa huduma*

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, uchambuzi wa Kamati umebaini kwamba hadi Juni, 2023 jumla ya madeni yaliyohakikiwa yalikuwa ni **shilingi trilioni 3.30** na kiasi cha madeni ambayo hayajahakikiwa ni **shilingi bilioni 64.72.** Hata hivyo, Serikali haijabainisha endapo madeni ya Wazabuni, Wakandarasi na Watoa Huduma ni kihatarishi. Kihatarishi hiki kinaweza kisikidhi tafsiri sahihi ya

kihatarishi ila kinaathiri utekelezaji wa Bajeti ya Serikali kila mwaka. Mfano, Sekta ya barabara, maji, kilimo na mifugo imekuwa vigumu kutekeleza miradi mipya kwa sababu ya madeni haya. Mwaka 2023 Serikali kupitia Katibu Mkuu Hazina ilitoa Waraka ujulikanao kama ***The Treasury Circular No. 2 of 2022/23 on Government Domestic Expenditure Arrears and Other Outstanding Obligations*** kwa lengo la kuendelea kusimamia na kutekeleza Mkakati wa Kudhibiti na Kuzuia Malimbikizo ya Madeni hata hivyo, Kamati imebaini kwamba waraka huu haujaweza kudhibiti malimbikizo ya madeni.

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** kati ya maeneo muhimu yanayopaswa kuzingatiwa na Maafisa masuuli wakati wa upangaji wa bajeti ni pamoja kutenga bajeti ya ulipaji wa madeni kwa kuzingatia umri wa madeni na kutoa kipaumbele kwenye madeni yenye riba na adhabu. Hivyo, Kamati inashauri Mwongozo huu uweke wazi kiasi ambacho kitatengwa na Serikali kwa ajili ya ulipaji wa madeni ya wakandarasi na wazabuni wa ndani.

## 8.0. MAONI YA UJUMLA KUHUSU MWONGOZO WA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA 2025/26.

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** uchambuzi wa Kamati umebaini masuala mbalimbali kama ifuatavyo:-

### *8.1. Ratiba ya Maandalizi ya Mpango na Bajeti*

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, kwa mujibu wa ratiba ya mpango, Serikali inawaelekeza Maafisa Masuuli kuandaa Mpango na Bajeti ya Muda wa Kati (MTEF) mara baada ya Mwongozo huu kuidhinishwa. Aidha, vitabu vya MTEF viwasilishwe Tume ya Mipango na Wizara ya Fedha wiki ya nne ya mwezi Januari, 2025 baada ya kuidhinishwa na Mamlaka husika. Hata hivyo, uzoefu unaonyesha, ukomo wa bajeti kwa mafungu huwasilishwa kati ya mwezi Januari hadi Februari na Maafisa Masuuli kuwasilisha randama kabla au ifikapo tarehe 10 Machi. Muda huo ni mchache kwa maafisa masuuli kufanya marekebisho kulingana na ukomo wa bajeti hasa pale wanapopaswa kupunguza bajeti.

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Kamati inaishauri Serikali, kuhakikisha ukomo wa Bajeti kwa Mafungu uende sambamba na uidhinishwaji wa mwongozo wa bajeti ili kuwapa Maafisa masuuli nafasi ya kuandaa bajeti inayoendana na ukomo wa bajeti. Vilevile, kwa mahitaji maalum yanayohitaji nyongeza ya bajeti, maombi hayo yafanyike mapema. Kamati inapendekeza kufanya mabadiliko kwenye ratiba kama ifuatavyo:-

**Jedwali Namba 11: Ratiba ya Maandalizi ya Mpango na Bajeti**

| | |
|---|---|
| Novemba, 2024 | Usambazaji wa Mwongozo wa Mpango na Bajeti ya Serikali ***pamoja na Ukomo wa Mafungu*** |

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, hatua hii itasaidia Serikali za Mitaa kupanga bajeti zao kwa kuzingatia ukomo, na endapo kuna mabadiliko yawe ni ya kuongeza ukomo na si kupunguza ili Mabaraza ya Madiwani na Vikao vya Ushauri wa Mkoa vipitishe bajeti yenye uhalisia.

***8.2. Bajeti ya Maendeleo***

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Kamati inapendekeza mapendekezo yaliyopo katika aya ya (v) ambayo inawaelekeza Maafisa Masuuli kuzingatia "Mwongozo wa uandaaji Miradi na Majadiliano ya Mikopo, Dhamana na upokeaji wa Misaada wa mwaka 2020 kuhusu hatua za upokeaji wa mikopo, dhamana na misaada" yaondolewe kwa sababu ya uwepo wa Sheria ya Mikopo, Dhamana na Misaada ya Serikali Sura 134, inayosimamia masuala yote ya ukopaji wa Serikali.

***8.3. Mkakati wa Kuongeza Fedha za Kigeni***

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, katika kukabiliana na changamoto ya ukosefu wa fedha za kigeni, Serikali imependekeza "***Kuhakikisha mikataba mipya inayoingiwa inatumia shilingi ya Tanzania kwa lengo la kupunguza uhitaji wa matumizi ya fedha za kigeni yasiyo ya lazima. Pia, kuhakikisha mikataba ya zamani iliyoingiwa kwa fedha za kigeni inafanyiwa mapitio"***.

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, pendekezo hili lina nia njema, ila utekelezaji wake una kasoro kwa sababu ya faida na hasara zinazotokana na ubadilishaji wa fedha *(exchange loss and gain)*. Ili pendekezo hili litekelezeke Kamati inaishauri Serikali, kwa mikataba inayohusisha ununuzi wa bidhaa na huduma ndani ya nchi, itumike shilingi na kwa mikataba inayohusisha ununuzi wa bidhaa nje ya nchi zitumike fedha za kigeni ili kuepusha hasara kwa pande zote. Vilevile, namna nyingine ya kuondokana na changamoto hii, ni Serikali kuruhusu mikataba iwe na kipengele cha kufanya mabadiliko ya kiwango cha kubadilisha fedha.

***8.4. Maelekezo kwa Ofisi za Wakuu wa Mikoa***

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, Serikali imetoa maelekezo kwa ofisi za Wakuu wa mikoa kuzingatia usimamizi, uandaaji na utekelezaji wa Mpango wa Wajibu wa Makampuni katika Jamii *(Corporate Social Responsibility- CSR)* wakati wa maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Mwaka 2025/26. Hata hivyo, Kamati inashauri Serikali Kuu na Serikali za Mitaa kuandaa mwongozo wa CSR kwa sekta zote ili uwe nyezo kuu ya namna ya kuomba, kupokea, kutumia, kusimamia na kufuatilia matumizi ya CSR ili kuepusha matumizi mabaya ya fedha hizo. Vilevile, Kamati inaishauri Serikali kufanya tathmini ya miradi inayotekelezwa kupitia mapato ya Halmashauri pamoja na mkakati wa kufuatilia miradi ya Serikali za Mitaa inayotekelezwa na Serikali kuu.

***8.5. Maelekezo Mahsusi kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa***

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, Mwongozo unaelekeza Serikali za mitaa kutenga bajeti kwa ajili ya kukamilisha miradi viporo hususan maboma yaliyoanzishwa kwa nguvu za wananchi. Aidha, jukumu hili limekuwa linatekelezeka kwa kasi ndogo kutokana na ufinyu wa bajeti za Serikali za Mitaa. Hadi kufikia machi, 2024 mahitaji ya ujenzi na ukamilishaji wa maboma ya zahanati, vituo vya afya, maabara na madarasa yaliyokuwepo ni **shilingi bilioni 267.66,** kiasi hicho cha fedha ni kikubwa kwa Serikali za Mitaa kukitenga kwa mapato ya ndani. Itakumbukwa kwamba katika mwaka wa fedha 2023/24 jambo hili lilijadiliwa katika kikao cha Kamati ya Uongozi ambapo Serikali iliahidi kutoa fedha kwa ajili ya kukamilisha maboma hayo. Licha ya ahadi ya Serikali, Mwongozo

unaelekeza Mamlaka za Serikali za Mitaa kutenga fedha kutoka mapato ya ndani ili kukamilisha maboma hayo.

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, uchambuzi wa Kamati umebaini kwamba itachukua takribani miaka 9 na miezi mitatu kwa Serikali za Mitaa kukamilisha maboma kulingana na bajeti wanazotenga kila mwaka. Hivyo, Kamati inaitaka Serikali kutenga fedha kupitia ruzuku ya Maendeleo (General Purpose Grant- GPG) inayotegemewa kurejeshwa kwa mwaka wa fedha unaokuja.

***8.6. Ushirikiano wa Kikanda na Kimataifa.***

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, katika kuimarisha ushirikiano wa kimataifa na kikanda. Kamati inaushauri ufuatao kwa Serikali:-

(i) Kupitia upya Mikataba yote ya Utozaji wa Kodi Mara Mbili *(Double Taxation Agreement- DTA)* ambayo hivi sasa iko 17 ili kubaini Mikataba ipi ina manufaa ili Taifa liendelee nayo na ipi haina manufaa Taifa liachane nayo. Ushauri huu wa Kamati unaenda sanjari na hatua ambazo Serikali tayari imeanza kuzichukua kwa kufanya mapitio ya mikataba minne baina ya Tanzania na Zambia wa mwaka 1963; Italia wa mwaka 1973; Canada wa mwaka 1995; na Africa Kusini wa mwaka 2005;

(ii) Kujenga majengo ya ubalozi kwenye nchi ambazo Tanzania ilipewa viwanja kwa ajili ya ujenzi. Suala la ujenzi wa balozi limekuwa ni la muda mrefu hadi kusababisha baadhi ya nchi kutishia kuyachukua maeneo hayo. Ikumbukwe kuwa ujenzi wa majengo ya balozi unaweza kutumika kama kitega uchumi na kuongeza mapato ya balozi. Kamati inashauri Serikali suala la ujenzi wa Balozi katika nchi ambazo Tanzania ilipewa viwanja lipewe kipaumbele. Aidha, Wizara ya Mambo ya nje iandae mkakati wa kutumia sekta Binafsi kuendeleza majengo ya ubalozi nje ya nchi.

***8.7. Uchumi wa buluu***

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Serikali imeelekeza Maafisa Masuuli kutekeleza Sera ya Uchumi wa Buluu ya mwaka 2024 ili kuibua na

kutumia fursa zitokanazo na rasilimali za maji bahari na baridi kwa lengo la kukuza uchumi na kuchochea maendeleo ya Taifa. Kamati inashauri maelekezo ya Serikali yaelekezwe moja kwa moja kwa Maafisa Masuuli wa Sekta husika au ambao katika maeneo yao kuna fursa za uchumi wa Buluuu. Vilevile, Serikali itoe elimu ya kutosha kuhusiana na uchumi wa buluu ukizingatia kuwa uchumi huu unajumuisha uvuvi wa bahari kuu na katika maji mafupi, usalama wa bahari, mazao ya bahari, usafiri wa majini pamoja na utalii kwenye maeneo ya mwambao kwa sababu bado nchi haijaweza kutumia fursa hizo kikamilifu.

### *8.8. Uchumi wa Kidigitali*

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, katika kukuza uchumi wa kidigitali, Serikali imewaelekeza Maafisa Masuuli kutekeleza Mkakati wa Taifa wa Uchumi wa Kidigitali 2024–2034. Kamati inaipongeza Serikali kwa kuanza utekelezaji wa Sera hiyo, hata hivyo inaishauri Serikali kuelekeza kwa Afisa Masuuli wa Mamlaka ya Serikali Mtandao (eGA), kwa kuwa ndiyo mamlaka inayohusika na mifumo ya Serikali. Hii itarahisisha mifumo itakayoundwa kusomana na kutotawanya rasilimali fedha katika mafungu mbalimbali ambazo kimsingi zinaenda kutekeleza shughuli ambayo ingeweza kutekelezwa na Mamlaka ya Serikali Mtandao ambayo ndiyo yenye jukumu hilo.

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, matumizi ya teknolojia ya akili bandia (AI) kwa sasa ndio inayokua kwa kasi duniani. Hata hivyo, Kamati imebaini, matumizi ya teknolojia hii nchini ni hafifu, ambapo mpaka sasa Ofisi ya Mahakama ndio imepiga hatua katika matumizi hayo. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali kuweka mkakati wa kuendeleza matumizi ya akili bandia (AI), katika Sekta ya Umma ili kuchochea ufanisi wa utekelezaji wa shughuli za Serikali.

### *8.9. Mazingira na Mabadiliko ya Tabianchi*

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, katika kukabiliana na changamoto ya mazingira na mabadiliko ya tabianchi, Serikali imewaelekeza Maafisa Masuuli kuibua miradi ambayo inaweza kupata fedha kutoka kwenye mifuko ya kimataifa inayosaidia nchi zinazoendelea katika kuhimili na kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi na uhifadhi wa mazingira.

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, Kamati imebaini Tanzania haipati fedha kutoka mifuko ya kimataifa ya kupambana na uharibifu wa mazingira kwenda kwenye Mfuko wa Taifa wa Mazingira kutokana na sababu zifuatazo:-

(i) Bodi ya mfuko huo ni bodi ya Ushauri sio Bodi ya uendeshaji;
(ii) Mfuko huo uko chini ya Idara iliyopo katika Ofisi ya Makamu wa Rais Mazingira na si chini ya Mamlaka au Wakala;
(iii) Fedha za mfuko hujumuishwa kwenye Bajeti ya mfuko mkuu na hivyo kutokuwa na uhakika kwamba zitaelekezwa kwenye Shughuli ya mazingira;
(iv) Mfuko kutokuwa na chanzo cha fedha cha uhakika; na
(v) Mfuko kutokuwa na watumishi wa kutosha kutokana na muundo wake.

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Kamati inaitaka Serikali kufanya mapitio ya Muundo wa Usimamizi wa Mfuko pamoja na kutafuta chanzo kwa ajili ya mfuko wa Mazingira kwa sababu athari za mazingira sio kihatarishi tena bali imekuwa janga. Serikali ione haja ya kutenga walau **asilimia 1** ya mapato yanayotokana na biashara ya hewa ukaa *(Carbon Credit)* ili yaelekezwe kwenye Mfuko wa Mazingira.

### *8.10. Ufuatiliaji, Tathmini, na Utoaji Taarifa za Utekelezaji wa Mpango na Bajeti*

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, ili kuboresha shughuli za ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa mpango na bajeti, Serikali imetoa maelekezo kwa Maafisa Masuuli. Hata hivyo, kufuatia mapungufu ya mwongozo ikiwemo kukosekana kwa vipengele vya kuwajibisha waliotenda makosa katika usimamizi na ufuatiliaji badala yake umeunda Kamati katika ngazi za Kijiji, Mkoa, Wizara na Tume ili kufanya ufuatiliaji. Kamati ililekeza Serikali kuandaa Sera na Sheria ya Ufuatiliaji na Tathmini ifikapo 2024/25 na 2025/26 mtawalia. Kamati imebaini hadi sasa Serikali haijakamilisha Sera ya ufuatiliaji na tathmini. Kutokukamilika kwa Sera hii kutaathiri utekelezaji wa ufuatiliaji na tathmini na hivyo, kutofikia malengo yaliyokusudiwa. Aidha, Tanzania haitakuwa nchi ya kwanza Duniani kuwa na Sera pamoja na Sheria ya Ufuatiliaji na Tathmini.

Nchi za Uganda, Afrika Kusini, Mexico, Mali, Columbia na Srilanka zina mfumo huo.

**Mheshimiwa Mwenyekiti**, pamoja na kuwepo na idara ya tathmini na ufuatiliaji katika OR-Mipango na Uwekezaji, Kamati haioni kama idara hii inatosha kutekeleza majukumu haya na badala yake ianzishwe Mamlaka ya Tathmini na Ufuatiliaji chini ya Sheria ya Tathmini na Ufuatiliaji.

## 9.0. MAONI YA UJUMLA.

### 9.1. Kukamilisha mifumo ya Ukusanyaji wa Mapato ya Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) sambamba na Ununuzi wa Midaki (Cargo Scanner) ya Kukagulia mizigo;

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** ili mfumo wa usimamizi wa kodi uwe na ufanisi unatakiwa kuepusha masuala makuu ambayo ni:- moja, kuondoa ugumu wa kulipa kodi, pili ni kuepusha matumizi ya fedha tasilimu katika kulipa kodi na tatu, ni kuondoa muingiliano kati ya mlipa kodi na mkusanya kodi. Njia pekee na inayoweza kuleta matokeo ya haraka ni matumizi ya mifumo ya kisasa. Kamati inatambua kwamba Mamlaka ya Mapato imekuwa ikiendeleza ujenzi na matumizi ya mifumo kama *e-filling*, IDRA, ITAX, ETS na TANCIS. Hata hivyo, Kamati imebaini mamlaka ilihitaji shilingi Bilioni 400 kwa ajili ya kukamilisha mifumo. Katika kipindi cha miaka mitatu (3) Serikali imekuwa haitengi Bajeti ya kutosha ili kukamilisha zoezi hilo. Hivyo, Kamati inaitaka Serikali kuhakikisha kwamba katika Mwaka wa Fedha 2025/26 suala la kukamilisha mifumo ya ukusanyaji mapato linapewa kipaumbele ili kuongeza mapato ya Serikali.

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Midaki katika mipaka yetu hasa ya mizigo imekuwa ni changamoto kubwa. Pamoja na athari za kiusalama zinazoweza kujitokeza kutokana na kukosekana kwa midaki, kukosekana kwa vifaa hivyo kumesababisha Maafisa wa forodha kulazimika kukagua mizigo kwa kufungua na kuangalia hali ambayo inawakutanisha walipa kodi na kufanya majadiliano na hivyo kufungua mwanya wa kuomba rushwa. Hivyo, Kamati inataka Serikali kuhakikisha kwamba katika mwaka wa fedha

2025/26 ni lazima Serikali itenge bajeti kwa ajili ya ununuzi wa midaki ya mizigo.

**9.2. Kupunguza matumizi ya Serikali yasiyo ya Lazima**

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** ni muda sasa Serikali imekuwa ikitanabaisha dhamira yake ya kupunguza matumizi ya Serikali yasiyo ya lazima. Hata hivyo, uchambuzi wa Kamati umebaini kwamba hakuna maelekezo yoyote mahususi kwa Maafisa masuuli ya kupunguza matumizi yasiyo ya lazima. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali kuunda Timu chini ya Wizara ya Fedha itakayohusisha wataalamu kutoka Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi, Tume ya Mipango na Ofisi ya Waziri Mkuu pamoja Wizara, Idara au Mamlaka yeyote kadri itakavyoonekana inafaa ili kupitia matumizi ya Serikali na kutoa mapendekezo ni matumizi yapi yanaweza kupunguzwa bila kuathiri utendaji kazi wa Serikali.

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Tanzania haitakuwa nchi ya kwanza kufanya mapitio ya Matumizi ya Serikali. Nchi ya Afrika Kusini inatekeleza sera ya kupunguza matumizi ya Serikali yaani *Fiscal Consolidation* kwa muda wa miaka mitano (5) sasa.

**9.3. Kufanya mapitio ya Mgawanyo wa Watumishi wa Umma na kuleta ulinganifu katika kuwagawanya;**

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** moja ya jambo ambalo Kamati imelibaini kuna mgawanyo usio sawa kwa watumishi wa umma. Ambapo kuna baadhi ya maeneo watumishi ni wengi ukilinganisha na maeneo mengine. Mfano, maombi mengi ya watumishi kuhama ni kutoka maeneo ya vijijini kwenda maeneo ya mijini au kutoka Wilaya za pembezoni kwenda wilaya za mijini. Ni haki ya mtumishi kuhama lakini tujiulize ni kwanini uhamisho ni kutoka maeneo ya vijijini na Wilaya za pembezoni kuelekea mijini na si vinginevyo? Hivyo, Kamati inaishauri Serikali kuweka utaratibu wa mikataba pale ambapo mtumishi amepelekwa katika kituo kwa mara ya kwanza alazimike kukaa walau miaka mitatu hadi mitano kabla ya kuomba uhamisho. Aidha tathmini iliyofanyika kupitia Mfumo wa Tathmini ya Rasilimali *(HR assessment System)* itumike sasa kutawanya watumishi watumishi kulingana na mahitaji.

### 9.4. Serikali kupunguza gharama ya kupata Taarifa kwenye Taasisi zake

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Kamati imechambua baadhi ya ada na tozo zinazotozwa kwa Taasisi moja ya Serikali inapoombwa taarifa kwa matumizi rasmi na Taasisi nyingine na kubaini ni kubwa. Mfano, ili kupata taarifa za Kampuni kwa ajili ya matumizi ya kiofisi kutoka Wakala wa Usajili Biashara na Leseni *(Bussiness Registration and Licencing Authority –BRELA)* inatakiwa kulipa shilingi 22,000 kwa mara moja. Kamati inaishauri Serikali kupunguza gharama hizo kwa taasisi za Serikali ili kurahisisha upatikanaji wa taarifa kwa gharama nafuu.

### 9.5. Serikali kuwekeza katika Kilimo cha Nazi

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Nazi ni zao la biashara nchini ambalo hulimwa na kustawi zaidi katika ukanda wa pwani ya Tanzania. Tanzania ni nchi ya kumi duniani na ya kwanza Barani Afrika kwa uzalishaji wa nazi wa **tani 530,000** kwa mwaka ikifuatiwa na Ghana ambayo huzalisha wastani wa **tani 366,183** kwa mwaka. Hata hivyo, bado Serikali haijaweka kipaumbele katika uendelezaji wa zao hili. Minazi ina manufaa mbalimbali kama vile kuzalisha tunda la nazi, Mafuta ya kupaka na kupikia, unga lishe, kutengeneza karatasi, dawa za kuulia wadudu warukao, samani, dawa za ngozi pamoja na kutengeneza sabuni. Aidha, mafuta ya nazi kwa ajili ya kupikia yanauzwa kwa wastani wa **Shilingi 30,000** kwa lita, bei ambayo ni ya juu kuliko mafuta mengine yanayozalishwa nchini na yanayoingizwa kutoka nje ya michikichi. Hivyo zao hili likiendelezwa vizuri linaweza kuwa ni chanzo cha mapato kinachowanufaisha Watanzania wengi hasa wa ukanda wa pwani.

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** Kamati inaishauri Serikali kutenga Bajeti ya kutosha katika mwaka wa fedha 2025/26 ili Taasisi ya utafiti wa kilimo Tanzania *(Tanzania Agricultural Research Institute · TARI)* ifanye utafiti wa kina wa mbegu bora ili kuimarisha kilimo cha nazi nchini.

Hatua hii iende sambamba na uanzishwaji wa mashamba makubwa ya minazi katika mikoa iliyo katika ukanda wa pwani ili Tanzania inufaike kikamilifu na uzalishaji wa zao hili.

## 10.0. HITIMISHO

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** naomba nitumie fursa hii kukupongeza kwa namna unavyoiwakilisha Tanzania kwenye medani za Kimataifa ukiwa Rais wa Umoja wa Mabunge Duniani (IPU), hakika umethibitisha uwezo wako kwa Taifa na Kimataifa katika kusimamia shughuli za Kibunge. Aidha, napenda kumshukuru Mhe. Mussa Azzan Zungu, Mb na Naibu Spika kwa ushirikiano wake na Kamati katika kipindi chote cha utendaji kazi wake. Vilevile, nitumie fursa hii kumpongeza Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa, Mb Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, pamoja na Mhe. Dkt. Doto Mashaka Biteko Naibu Waziri Mkuu kwa namna wanavyosimamia utendaji kazi wa Serikali.

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** kwa namna ya kipekee naomba niwashukuru Mhe. Prof. Kitila Mkumbo, Mb Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Mipango na Uwekezaji, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba Mb, Waziri wa Fedha pamoja na Mheshimiwa Hamad Hassan Chande, Mb Naibu Waziri wa Fedha kwa ushirikiano wao na Kamati. Aidha, Kamati inampongeza Mhe. Stanslaus Nyongo, Mb na Naibu Waziri wa Ofisi ya Rais Mipango na Uwekezaji kwa kuteuliwa kuwa Naibu Waziri. Vilevile, Kamati inawashukuru Dkt. Tausi Kida, Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Mipango na Uwekezaji, Ndg. Jenifa Omolo, Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Fedha, Dkt Mursaly A. Milanzi, Kaimu Katibu Mtendaji wa Tume ya Mipango, pamoja na watendaji wa Tume ya Mipango na Wizara ya fedha kwa kushirikiana na Kamati wakati wa majadiliano ya Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo ya Taifa wa mwaka 2024/25 pamoja na Mwongozo wa Uandaaji wa Mpango na Bajeti kwa mwaka wa fedha 2024/25.

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** naomba kuwapongeza Wajumbe wa Kamati wakiongozwa na Mhe. Twaha Ally Mpembenwe, Mb Makamu Mwenyekiti wa Kamati kwa umahiri na ushirikiano wao katika kuchambua Mpango na Mwongozo ili kuuboresha hadi kufikia hatua hii. Naomba kuwatambua

Wajumbe hao kama ifuatavyo: -

1. Mhe. Oran Manase Njeza, Mb Mwenyekiti
2. Mhe. Twaha Ally Mpembenwe, Mb M/Mwenyekiti
3. Mhe. Shamsi Vuai Nahodha, Mb Mjumbe
4. Mhe. Mariam Madalu Nyoka, (Mb) Mjumbe
5. Mhe. Dkt. Charles Stephen Kimei, (Mb) Mjumbe
6. Mhe. Josephat Sinkamba Kandege, (Mb) Mjumbe
7. Mhe. Leah Jeremiah Komanya, (Mb) Mjumbe
8. Mhe. Juma Hamad Omar, (Mb) Mjumbe
9. Mhe. Subira Khamis Mgalu, (Mb)Mjumbe
10. Mhe. Shally Josepha Raymond, (Mb) Mjumbe
11. Mhe. Stella Alex Ikupa, (Mb) Mjumbe
12. Mhe. Jonas William Mbunda, (Mb) Mjumbe
13. Mhe. Bahati Ndingo, (Mb) Mjumbe
14. Mhe. Kwagilwa Reuben Nhamanilo, (Mb) Mjumbe
15. Mhe. Bahati Khamis Kombo, (Mb) Mjumbe
16. Mhe. Vedastus Manyinyi Mathayo, (Mb) Mjumbe
17. Mhe. Omar Ali Omar, (Mb) Mjumbe
18. Mhe. Zaytun Seif Swai, (Mb) Mjumbe
19. Mhe. Rashid Abdallah Rashid, (Mb) Mjumbe
20. Mhe. Joseph Zacharius Kamonga, (Mb) Mjumbe

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** kwa namna ya kipekee nimshukuru pia Ndg. Baraka Ildephonce Leonard Katibu wa Bunge kwa niaba ya watumishi wote, kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kikamilifu.

**Mheshimiwa Mwenyekiti,** naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja.

Oran Manase Njeza,
**MWENYEKITI**
**KAMATI YA BUNGE YA BAJETI**
01 Novemba, 2024

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, Mwenyekiti amezungumza haya kwa niaba ya Bunge kwa maana ya kupitia Kamati ya Bajeti. Kwa hivyo, hoja ni za hawa Mawaziri wawili. Kwa

hivyo, nimeona kuna Wabunge wamesimama kuunga mkono hoja ya Mwenyekiti. Yeye alikuja hapa kutushawishi kwamba tuunge mkono hoja ambayo imetolewa na hawa wawili.

Waheshimiwa Wabunge, mnivumilie kidogo kwa dakika chache. Mwenyekiti, keti kidogo hapo.

Waheshimiwa Wabunge, tumesikia hoja hizi mbili ambazo huwa zinajadiliwa kwa pamoja kutoka kwa Mawaziri wetu hawa wawili, lakini pia tumesikia maoni ya Kamati. Kwa utaratibu wa kawaida tunapaswa sasa kuanza uchangiaji, lakini naona muda wetu umesogea. Kwa hiyo, mengine nitayasemea pale kwenye Bunge. Ila wale ambao walikuwa na vitabu, sijajua kwenye vishikwambi ni ukurasa wa ngapi?

Mwenyekiti, kwenye sehemu ya 4.0, Ugharamiaji wa Mpango wa Maendeleo kwa mwaka 2025/2026, Mwenyekiti atakwenda kutazama hizi takwimu hapa na maneno yaliyoandikwa. Ikiwa ataona kwamba kuna mahali panahitaji marekebisho, ataleta *addendum* ili iwe sehemu ya hii taarifa ya Kamati. Haya, Katibu.

**NDG. BARAKA I. LEONARD – KATIBU WA BUNGE:** Bunge linarejea.

*(Bunge Lilirejea)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tuketi. Vinginevyo ningewaacha msimame, lakini nimeona mketi kwa sababu Mheshimiwa Waziri wa Fedha leo kuna watu amewaita wazee humu ndani, nikaogopa wanaweza kusimama muda mrefu halafu ikawa mtihani. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, niwakumbushe kwamba tunakwenda sasa kwenye semina ambayo itaanza baada ya nusu saa tukishaahirisha Bunge hapa. Hata hivyo, kwa kuangalia muda ulioombwa na wawasilishaji kule, lakini pia kwa kuangalia idadi yetu tulivyo humu ndani, inawezekana muda wetu wa kurejea Bunge la jioni tutakuwa bado tunatoa maoni kule na nisingependa tuwakatishe watu kwa sababu wanaweza kuwa na

hoja nzito. Pia, hata wao wanapowasilisha kule, huenda ikawa ngumu kusema mtu apewe dakika tatu kwa sababu wanachangia kuhusu Dira ya Taifa. Kwa hiyo, kila mtu atapewa muda kwa kadri alivyojiandaa kwa ajili ya kuchangia.

Kwa hiyo, saa 11.00 tunaweza kuwa hatujamaliza lile zoezi la kuchangia ile Dira yetu ya Taifa ili tuipe muda wa kutosha, lakini pia Waheshimiwa Wabunge mpate muda wa kutosha wa kuwasilisha mawazo yenu ninyi kama wananchi lakini mawazo yenu kama wawakilishi wa wananchi.

Kwa kusema hivyo, mjadala wetu ama michango yetu kama Wabunge kuhusu hoja zilizowasilishwa hapa Bungeni tutaanza siku ya Jumatatu na hatutaanza leo. Sasa, hii pia inatoa fursa kwetu kupitia vizuri hoja hizi mbili na kuona ni hoja zipi tutataka ziwe sehemu ya Mwongozo, lakini pia ziwe sehemu ya Mapendekezo ya Mpango yaliyotolewa hapa ili bajeti yetu ya mwakani iende vizuri.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo naahirisha shughuli za Bunge mpaka Jumatatu saa 3.00 asubuhi.

*(Saa 7.00 Mchana Bunge Liliahirishwa hadi Siku ya Jumatatu, Tarehe 4 Novemba, 2024 Saa Tatu Asubuhi)*